UCHANGANUZI WA MTINDO KATIKA MUZIKI WA BENGA WA JAMII YA WAKAMBA: MKABALA WA UMTINDO

CAROLYNE MUTHINI MUTUKU

TASNIFU HII YA UTAFITI IMEWASILISHWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA KISWAHILI KATIKA CHUO KIKUU CHA EMBU

AGOSTI, 2025

UNGAMO

Tasnifu hii ya utafiti ni kazi yangu asilia na haijawahi kuwasilishwa kwingine kwa mahitaji ya shahada au tuzo nyigine yoyote.

Sahihi..... Tarehe.....

Carolyne Muthini Mutuku

E556/1369/2020

Tasnifu hii ya utafiti imewasilishwa kwa madhumuni ya kutahiniwa kwa idhini yetu kama Wasimamizi wa Chuo Kikuu.

Sahihi..... Tarehe.....

Dkt. John Khaisie Wanyama

Idara ya Masomo ya Jamii

Chuo Kikuu cha Embu

Sahihi……. Tarehe.....

Dkt. Timothy Kinoti M'Ngaruthi

Idara ya Masomo ya Jamii

Chuo Kikuu cha Embu

TABARUKU

Kazi hii naitabarukia wale wote walioniunga mkono na kunitia moyo katika safari hii. Kwa familia yangu, kwa upendo wao wa dhati, subira na imani yao kwangu hata katika nyakati za changamoto nyingi; msaada wenu wa mara kwa mara umekuwa himizo kwangu.

SHUKRANI

Ningependa kumshukuru kwa dhati Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya bora na kunipa nafasi ya kipekee ya kuendeleza masomo yangu hadi kiwango hiki. Bila uwezo wake singefika nilipo sasa. Neema zake zimekuwa nguzo yangu katika kila hatua.

Pia, ningependa kutoa shukrani kwa Chuo Kikuu cha Embu, kwa kufadhili masomo yangu ya uzamili katika Idara ya Elimu ya Jamii. Usimamizi wenu wa kipekee na msaada endelevu umeniwezesha kufikia hatua hii. Mchango wenu katika kukuza elimu ni wa kipekee na umeleta mabadiliko makubwa kwa wanafunzi wengi, nikiwa mmoja wao. Nikiwa sehemu ya familia hii, najivunia kuona matunda ya juhudi zenu kwangu na kwa jamii kwa jumla.

Vilevile, ninatoa shukrani zangu kwa wasimamizi wangu, Dkt.Timothy Kinoti M'Ngaruthi na Dkt. John Khaisie Wanyama kwa uelekezi wao usiokadirika, subira na kunitia motisha kila wakati. Maoni yao ya kina, utaalamu wao na kujitolea kwao kumekuwa na mchango mkubwa katika kufanikisha kazi hii. Pia ninatoa shukrani kwa idara ya masomo ya jamii katika Chuo Kikuu cha Embu ikiongozwa na Dkt. Lilian Omoke kwa uelekezi wa kuiboresha kazi hii.

Shukrani pia kwa wanafunzi wenza Bw. Brian Mulonzi, Bi. Faith Mbithe na Bi. Nanis Muthoni kwa uelekezi wenu muhimu katika kufanikisha kazi hii. Maoni yenu ya busara, mapendekezo na michango yenu imeboresha utafiti huu kwa kiwango kikubwa. Nawaombea ufanisi katika shughuli zenu za kila siku.

Shukrani za dhati kwa familia yangu kwa upendo, msaada na imani yao ambayo imekuwa nguzo yangu. Kwa wazazi wangu, kujitolea kwenu na motisha zenu kumefanya safari hii iwezekane, fadhila zenu kwangu ni deni daima. Kwa ndugu zangu Victoria Mueni na Jacob Nzangi, asanteni kwa kunihimiza kila wakati.

Shukrani za pekee kwa wafanyikazi wenza; Bi. Petronilla Chibole, Bi. Elizabeth Kawira na Bw. Kelvin Maina kwa kuwa mstari wa mbele katika kunisaidia na masuala ya kiufundi na kimazingira. Kazi hii haingekamilika bila msaada wenu wote. Asanteni sana!

YALIYOMO

UNGAMO ..... **ii**

TABARUKU ..... **iii**

SHUKRANI ..... **iv**

YALIYOMO ..... **v**

ORODHA YA VIAMBATISHO ..... **ix**

ORODHA YA VIFUPISHO ..... **x**

UFAFANUZI WA ISTILAHI ..... **xi**

ABSTRACT ..... **xiii**

IKISIRI ..... **xiv**

SURA YA KWANZA **1**

UTANGULIZI **1**

1.1 Usuli wa Mada 1

1.2 Suala la Utafiti 4

1.3 Madhumuni ya Utafiti 5

1.4 Maswali ya Utafiti 5

1.5 Sababu za Kuchagua Mada 5

1.6 Umuhimu wa Utafiti 6

SURA YA PILI **8**

MAPITIO YA MAANDISHI **8**

2.0 Utangulizi 8

2.1 Yaliyoandikwa kuhusu Mada ya Utafiti 8

2.1.1 Mikakati ya Uimbaji 8

2.1.2 Suala la Ujumi katika Muziki 11

2.1.3 Athari Lengwa za Matumizi ya Mikakati ya Kimtindo 13

2.2 Misingi ya Nadharia 15

2.2.1 Viwango vya Nadharia ya Umtindo 16

2.2.1.1 Kiwango cha Udhihirikaji 16
2.2.1.2 Kiwango cha Umbo 17
2.2.1.3 Kiwango cha Kisemantiki 20
2.2.1.4 Matawi Saidizi ya Isimu 21
2.3 Hitimisho 22
SURA YA TATU 23
MBINU ZA UTAFITI 23
3.0 Utangulizi 23
3.1 Muundo wa Utafiti 23
3.2 Eneo la Utafiti 23
3.3 Walengwa katika Utafiti 24
3.4 Mbinu za Usampulishaji 24
3.5 Mbinu za Ukusanyaji wa Data 26
3.6 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data 27
3.7 Maadili Yaliyozingatiwa 27
3.8 Hitimisho 27
SURA YA NNE 29
MATOKEO YA UTAFITI 29
4.0 Utangulizi 29
4.1 Mchakato wa Uchanganuzi 29
4.2 Mikakati ya Mtindo 30
4.2.1 Kiwango cha Grafolojia 30
4.2.1.1 Ugawaji wa Beti 30
4.2.1.2 Uakifishaji na Ugawaji wa Mishororo 32
4.2.2 Kiwango cha Fonolojia 34
4.2.2.1 Urudiaji 34
4.2.2.2 Uradidi 37
4.2.2.3 Urari wa Sauti 38
4.2.2.4 Takriri 40

4.2.3 Kiwango cha Umbo 42
4.2.3.1 Uhamishaji Msimbo 42
4.2.3.2 Msamiati wa Kukopa 45
4.2.3.3 Matumizi ya Visawe 47
4.2.3.4 Msamiati wa Kubuni 48
4.2.4 Kiwango cha Kisintaksia 50
4.2.4.1 Sentensi Ndefu 50
4.2.4.2 Sentensi Fupi 52
4.2.4.3 Sentensi Tongole 54
4.2.4.4 Sentensi za Maswali 56
4.2.4.5 Usambamba 57
4.2.4.6 Ukiushi wa Kisintaksia 59
4.2.5 Kiwango cha Semantiki 61
4.2.5.1 Tautolojia 61
4.2.5.2 Ukinzani 63
4.2.5.3 Kinaya 66
4.2.5.4 Paradoksia 68
4.2.5.5 Tamathali za Usemi 70
4.3 Ujumi Katika Muziki wa Benga wa Jamii ya Wakamba 74
4.3.1 Ujumi wa Kihalisia 75
4.3.2 Ujumi wa Kigothiki 79
4.3.3 Ujumi wa Kimapenzi 82
4.3.4 Ujumi wa Kitamaduni 84
4.3.5 Ujumi wa Kiishara 87
4.3.6 Ujumi wa Kisiasa 89
4.4 Athari Lengwa za Matumizi ya Mikakati ya Kimtindo 91
4.4.1 Uwasilishaji wa Masuala ya Wanawake 91
4.4.2 Kuwasilisha Jumbe za Kisiasa 94
4.4.3 Suala la Dawa za Kulevya 95
4.4.4 Kuwasilisha Hisia za Kibinafsi na Kijamii 98
4.4.5 Kuhamasisha kuhusu Maadili na Kuchochea Mabadiliko ya Kijamii 100

4.4.6 Kuendeleza Utamaduni 104

4.4.7 Kukuza Ushirikiano katika Jamii 106

4.5 Hitimisho 110

SURA YA TANO 111

MAJADILIANO, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO 111

5.0 Utangulizi 111

5.1 Majadiliano Kuhusu Matokeo ya Utafiti 111

5.1.1 Mikakati ya Kimtindo 111

5.1.2 Uimarishaji wa Ujumi 113

5.1.3 Athari Lengwa za Matumizi ya Mikakati ya Kimtindo 113

5.2 Hitimisho 114

5.3 Mapendekezo 115

MAREJELEO 117

VIAMBATISHO 125

ORODHA YA VIAMBATISHO

Kiambatisho cha I. Sikala Yakwa (Sigara Yangu) SY 125

Kiambatisho cha II. Munene Kowoolilwe? (Mkubwa Kwani Ulisahau?) MK.... 127

Kiambatisho cha III. Wasa Mbili (Rafiki Kupe) WM..... 128

Kiambatisho cha IV. Germany by Foot (Ujerumani Kwa Miguu) GF..... 129

Kiambatisho cha V. Wakatimba Kumbavu (Wakatimba Mpumbavu) WK..... 131

Kiambatisho cha VI: Raha Ndukauna (Raha Haisadii) RN 132

Kiambatisho cha VII: Amaitha (Maadui) AM 135

Kiambatisho cha VIII: Sio Mageni SM..... 136

Kiambatisho IX: Idhini ya Kukusanya Data (NACOSTI) 139

ORODHA YA VIFUPISHO

AM	Anaitha (Maadui)
BPS	Board of Postgraduate Studies (Bodi ya masomo ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Embu)
GF	Germany by Foot (Ujerumani kwa Miguu)
KIMB	Kiambatisho
MK	Munene Kowoolilwe (Mkubwa kwani Ulisahau)
MSH	Mshororo
NACOSTI	Tume ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Uvumbuzi
RN	Raha Ndukauna (Raha Haisaidii)
SM	Sio Mageni
SY	Sikala Yakwa (Sigara Yangu)
TUKI	Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili
UB	Ubeti
UK	Ukurasa
UNESCO	United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization (Shirika la Elimu, Sayansi na Utamaduni la Umoja wa Mataifa)
WK	Wakatimba Kumbavu (Wakatimba Mpumbavu)
WM	Wasa Mbili (Rafiki Kupe)

UFAFANUZI WA ISTILAHI

Athari Lengwa	Matokeo kusudiwa ambayo wasanii wa muziki wa Benga hulenga kufikia kwa hadhira lengwa kupitia uchaguzi wao wa mtindo.
Benga	Aina ya muziki maarufu nchini Kenya unaojulikana kwa mapigo ya haraka, ustadi wa gitaa na uimbaji wa mishororo yenye mizizi ya kitamaduni kwa lugha ya Kikamba.
Gothiki	Mtindo wa fasihi au sanaa unaotumia vipengele vya giza na hofu kuunda hisia za msisimko au tahadhari kwa hadhira.
Hadhira Lengwa	Wasikilizaji wa muziki wa Benga wa lugha ya Kikamba.
Kamba	Kabila la watu wanaopatikana katika eneo la Mashariki mwa nchi ya Kenya na ambao lugha yao ni Kikamba.
Mshororo	Mstari katika wimbo au ushairi. Katika utafiti huu istilahi hii imetumika kwa maana ya sentensi katika muziki wa Benga.
Mtindo	Upekee wa utunzi au uandishi wa kazi ya sanaa ambapo msanii huipa kazi yake sura ya kifani na kimaudhui inayoitofautisha na ya msanii mwingine.
Muziki	Mpangilio wa ala, midundo na sauti zinazotumiwa na wasanii wa Benga ya Kikamba kuwasilisha maana za kitamaduni na ujumbe wa kijamii.
Mwimbaji	Msanii ambaye ametunga na kuimba muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba.
N**yimbo**	Aina ya sanaa katika fasihi ambayo hutumia lugha teule, sauti na kiimbo maalum na huweza kutumia ala za muziki kama vile ngoma na gitaa. Katika utafiti huu istilahi hii imetumika kumaanisha muziki.
Paradoksia	Ni usemi unaopingana na mantiki lakini wenye ukweli au maana iliyofichika

Tautolojia	Matumizi ya maneno au misemo inayorudia wazo moja bila kuongeza maana mpya, hutumika kusisitiza ujumbe au kuongeza mvuto wa kifasihi.
Ujumi	Urembo au mvuto wa kisanaa unaotokana na matumizi ya mikakati ya kimtindo katika muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba
Umilisi	Ni ujuzi au uelewa wa kanuni zinazotawala lugha fulani ambazo kila mzungumzaji wa lugha asilia huwa nao.
Umtindo	Uchambuzi wa vipengele vya lugha, mbinu za kifasihi na mbinu za kisanaa zinazotumika katika muziki wa Benga ya Kikamba ili kuunda maana na kufikia madhumuni maalum ya kitamaduni na kijamii.

ABSTRACT

Music serves as a powerful medium of communication allowing people in the society to express and discuss various aspects of life such as love, death, politics and other societal issues. This study analyzed the employment of stylistic elements by Benga music artists of the Kamba community in communicating their messages. Drawing upon Geoffrey Neil Leech's stylistics theoretical framework, three levels of style namely realization, form and semantics were examined. Stylistics theory interprets and critiques texts from a linguistic perspective as a discipline closely related to literature. This study aimed to: identify the strategies used by Kamba Benga musicians to communicate their messages; analyze how they enhance aesthetic elements in their music; and examine the intended effects of their stylistic choices. Data collection for this research relied on textual analysis enabling a comprehensive examination of purposively selected Kamba Benga music compositions. Descriptive analysis, based on the levels of stylistics theory, served as the primary approach for analyzing the data for this research. Based on this study it was evident that Kamba community Benga musicians use various stylistic strategies such as repetition, rhyme, refrain and figures of speech to convey their messages. The study found out that these stylistic strategies are used to enhance realistic, gothic, romantic, symbolist, political and cultural aesthetics as well as achieving the musicians' intended effects to their target audiences. This research contributes new knowledge to stylistics by demonstrating how the unique linguistic and artistic features of Kamba Benga music construct meaning, preserve the indigenous language and reflect cultural identity, thus enriching the fields of linguistics, literature and African cultural studies. It positions Kamba Benga music as a valuable subject in literature and language research, while also guiding musicians to create socially relevant, aesthetically rich and emotionally impactful music.

IKISIRI

Muziki ni njia mojawapo ambayo watu katika jamii hutumia kuwasilisha masuala kama vile mapenzi, kifo na siasa. Utafiti huu ulichanganua jinsi waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba hutumia vipengele vya mtindo kuwasilisha jumbe. Kwa kuzingatia kielelezo cha nadharia ya umtindo ya Geoffrey Neil Leech, utafiti huu ulichunguza viwango vitatu vya mtindo ambavyo ni udhihirikaji, umbo na semantiki. Nadharia ya umtindo hufasiri na kuhakiki tungo kwa kuzingatia mtazamo wa kiisimu kama taaluma iliyo na uhusiano wa karibu na fasihi. Utafiti ulilenga: kubainisha mikakati ya kimtindo wanayotumia waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba kuwasilisha ujumbe; kuchanganua wanavyoimarisha ujumi katika muziki wao; kueleza athari lengwa ya uchaguzi wao wa kimtindo. Ukusanyaji wa data ulitegemea mbinu ya uchanganuzi matini ili kuwezesha uchunguzi wa kina wa nyimbo za muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba zilizoteuliwa kimakusudi. Data ilichanganuliwa kimaelezo kwa kurejelea mihimili ya nadharia ya umtindo. Kutokana na utafiti huu ilibainika kuwa Waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba hutumia vipengele vya kimtindo kama vile uradidi, urudiaji na tamathali za usemi kuwasilisha ujumbe. Vilevile utafiti uliweza kubaini kuwa waimbaji hao hutumia vipengele vya kimtindo kuimarisha ujumi wa kihalisia, kigothiki, kimapenzi, kisiasa na kitamaduni. Isitoshe, mikakati hii huwasaidia kufanikisha athari lengwa kwa hadhira zao. Utafiti huu unachangia maarifa mapya katika taaluma ya umtindo kwa kuonyesha jinsi vipengele vya kipekee vya lugha na usanii katika muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba vinavyojenga maana, kuhifadhi lugha za asili na kuakisi utambulisho wa kitamaduni. Unaimarisha vitengo vya isimu, fasihi na masomo ya tamaduni za Kiafrika. Pia, unatambulisha muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba kama mada yenye umuhimu katika utafiti wa fasihi na lugha, huku ukiwaongoza wanamuziki kutunga muziki unaoangazia masuala ya kijamii na ujumi wa kisanaa

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 Usuli wa Mada

Muziki ni njia mojawapo ambayo wanajamii hutumia kuwasiliana kuhusu masuala tofauti kama vile mapenzi, siasa, kifo na dini. Baadhi ya majukumu ambayo muziki hutekeleza ni kama vile; kupanua ujuzi wa kijamii, kukuza ushirikiano katika jamii, kukuza ubunifu na kuwasilisha hisia za wanajamii. Vilevile muziki husaidia kuelewa istilahi na dhana mpya, kuweka kumbukumbu za muktadha, kujifunza stadi za kucheza ala za muziki pamoja na mitindo ya unenguaji viungo vya mwili (Okal, 2020). Hata hivyo, mawasiliano haya hutofautiana katika jamii mbalimbali kwani mitindo wanayotumia hutofautiana kutegemea mahali wanapoishi, kiwango cha elimu, tofauti za kitamaduni na vyeo vya kijamii (Butler, 2004).

Kwa mujibu wa Okal (2020), muziki wowote uliotungwa vizuri huwa na mielekeo mitatu muhimu ambayo ni ujumi, ushirikishaji na uelekezaji wa kijamii. Ujumi unahusu urembo wa lugha na mvuto wa muziki pamoja na namna unavyopendeza hadhira. Ushirikishaji unahusu mazoea na desturi za binadamu zinazoongoza maisha yake ya kila siku. Uelekezaji wa kijamii unahusu faida ambazo binadamu huweza kupata kutokana na muziki. Faida hizo ni kama vile; kukuza ushirikiano wa jamii, kuimarisha hisia za kisaikolojia za binadamu pamoja na kuimarisha hadhi ya msanii katika jamii (Okal, 2020). Kulingana na Churukuguy (2020), nyimbo huwa katika tanzu mbalimbali kama vile nyimbo za kisiasa, nyimbo za dini na zilizopendwa. Nyimbo zilizoshughulikiwa katika utafiti huu zipo katika utanzu wa zilizopendwa na zinajulikana kama muziki wa Benga.

Muziki wa Benga ni aina ya muziki ambao huwasilishwa na waimbaji, wachezaji pamoja na ala za muziki kama vile gitaa na ngoma. Doyle (2017) anarejelea aina hii ya muziki kama ‘thieta ya muziki.’ Hii ni kwa sababu hujikita katika umbo la kimuundo linalohusisha kuimba, kunengua viungo vya mwili na dayolojia ili kueleza jambo kama linavyotokea katika maisha ya kila siku ya binadamu. Kwa mujibu wa Nketia (1974), muundo katika muziki wa Benga hujengwa kwa mwanzo, kati na mwisho. Vilevile huwa na wahusika ambao wanaimba au kuimbwa katika muziki wenyewe. Pia muziki wa Benga huwa na maudhui yanayozungumziwa pamoja na hatua zinazopaswa kuchukuliwa na wahusika baada ya kuimba au kusikiliza muziki.

Muziki wa Benga ni utanzu maarufu nchini Kenya na hujitambulisha kwa sifa ya mdundo na mapigo ya kasi pamoja na ustadi wa msanii wa kucheza gitaa kwa namna maalum (Red Bull Music Academy, 2019). Awuoda (2008) anasema kuwa umaarufu wa muziki wa Benga hutokana na kuchanganya mdundo maalum wa gitaa pamoja na sauti. Anaendelea kusema kuwa muziki wa Benga huweza kuchezwa kutokana na sifa yake ya tempo ya juu.

Kulingana na Senoga-Zake (1986), chimbuko la muziki wa Benga halijathibitishwa, ila muziki huu unaaminika kuingia nchini Kenya katika miaka ya 1950 kupitia kwa jamii ya Wadholuo kutoka eneo la Nyanza. Inaaminika kuwa baadhi ya wanajamii hawa walisafiri katika nchi ya Kidemokrasia ya Kongo kwa minajili ya kazi, biashara na matembezi. Baada ya muda walijifunza kucheza aina ya gitaa maarufu inayojulikana kama 'nyatiti'. Waimbaji wa eneo hili walijifunza kuimba kwa kuiga mapigo ya gitaa hiyo maaarufu. Kutokana na uigaji huo muziki wa Benga ukaibuka. Muziki wa Benga ulisambaa katika maeneo mengine nchini Kenya kutoka katika eneo la Nyanza ambapo kuna Benga ya Wagikuyu, Wakamba, Abaluhya na hata Wakisii (Senoga-Zake, 1986).

Kwa mujibu wa Stapleton & May (1987) matumizi ya kwanza ya neno 'Benga' katika kazi zilizorekodiwa yalikuwa katika wimbo ulioitwa 'Monica Odongo' ulioimbwa na kikundi cha vijana kilichojiita 'Ogara boys' mwaka wa 1963. Etimolojia ya neno 'Benga' ingali tata kwani kuna baadhi ya watu wanaoamini kuwa neno hilo lilitokana na jina 'obengore' ambalo lilikuwa jina la mamake mwimbaji maarufu aliyeitwa Daniel Owino Misiani. Hata hivyo, neno 'Benga' linarejelea vazi la sketi maarufu la wakati huo ambalo lilikuwa linampwaya mtu anapolivalia na lilijulikana kama 'ogara skirt' (Ochieng', 1971). Kwa hivyo, Benga ni utanzu wa sanaa ya muziki ambao huwasilishwa kwa njia ya uimbaji unaoendana na mpangilio maalum wa mapigo ya sauti na ala za muziki.

Kulingana na Muema (2019), muziki wa Benga nchini Kenya umegawika kulingana na maeneo. Kuna Benga ya Magharibi, ya Kati na Mashariki mwa nchi ya Kenya. Ni katika eneo la Mashariki ambapo muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba unapatikana. Muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba umekuwepo tangu miaka ya sitini ambapo kulikuwepo na waimbaji maarufu kama vile, Kakai Kilonzo na Bosco Mulwa. Kufikia sasa idadi ya waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba

imeongezeka. Waimbaji wa kisasa katika jamii ya Wakamba ni kama vile Alphose Kioko, Alex Kasau na Ben Mbatha. Muziki wa waimbaji hawa huchezwa kila siku katika vipindi vya redio na runinga za jamii hii ya Wakamba (Mutio, 2023). Kama anavyodokeza Kithome (2012) alipokuwa akichunguza shughuli za muziki wa kijamii miongoni mwa jamii ya Wakamba, sababu kuu inayochangia idadi kubwa ya wasikilizaji wa redio za jamii hiyo kujivunia na kushabikia vipindi vyao ni muziki wa Benga.

Anudo na Awuor (2018) wanadokeza kuwa, uwasilishaji wa maudhui katika muziki huweza kufichwa kwa kutumia mitindo mbalimbali ya utunzi. Kusudi la kutumia mitindo fiche ni kuifanya hadhira kufikiria zaidi ndiposa iweze kutambua maana inayopitishwa. Hata hivyo, wanasema kwamba si nyimbo zote hutumia mitindo fiche; zipo pia nyimbo nyingine ambazo hutumia lugha rahisi na wazi na zinaweza kueleweka na wasikilizaji moja kwa moja bila kutegemea fasiri za ndani za maana fiche. Kwa mujibu wa Leech (1969), dhana ya mtindo haiwezi kutokea katika ombwe tupu bali hupata maana wakati lugha inapotumika kuwasilisha ujumbe. Wasanii hutumia mtindo katika tungo zao hasa mashairi na nyimbo kwa kusudi la kupata athari za kiujumi.

Kwa mujibu wa Timu ya Historia ya Kenya (2025), mvuto katika muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba husababishwa na matumizi ya mikakati ya kipekee ya mtindo. Hii ni pamoja na mapigo ya gitaa yenye mdundo maalum na mchanganyiko wa lugha ya asili na maudhui ya kijumla. Muema (ameshatajwa) anadokeza kuwa vipengele vya mikakati ya kimtindo hutumika kama chombo cha kusimulia hadithi, kuhifadhi utamaduni na masuala ya kijamii. Ni katika misingi hii ambapo utafiti huu umechanganua mtindo katika muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba. Mtafiti alikusudia kubaini namna wasanii wa muziki huu wanavyotumia viwango mbalimbali vya mitindo ya isimu kuwasilisha jumbe zao.

Historia Fupi ya Jamii ya Wakamba

Jamii ya Wakamba inaishi katika eneo la Mashariki mwa nchi ya Kenya mahali panapojulikana kama Ukambani (Mathooko, 2014). Jamii ya Wakamba ni jamii mojawapo ya makundi kadhaa ya Wabantu. Kundi la Bantu ndilo kubwa nchini Kenya na huwa na kabila tofauti zenye uhusiano wa karibu (King'ei, 1992).

Wanahistoria wameelezea kuwa Wakamba walihamia nchini Kenya kutoka eneo la Shungwaya, lililokuwa kaskazini mwa Kenya na kusini mwa Somalia, na wakatua maeneo ya Mlima Kilimanjaro katika karne ya kumi na nne. Wakamba walikuwa wawindaji na wafugaji. Kufikia mwishoni mwa karne ya kumi na sita, Wakamba walianza kuhama kutoka sehemu zilizokuwa karibu na mlima Kilimanjaro kutokana na matatizo kama vile uvamizi na ukame (Ndeti, 1972). Kwa sasa Wakamba wanaishi katika kaunti za Machakos, Kitui na Makueni nchini Kenya (Stanley Kiwia, 2018). Hata hivyo, kulingana na Kieti na Coughlin (1990), kuna Wakamba ambao wanapatikana katika sehemu nyingine nchini Kenya kama vile Embu, sehemu za Taita Taveta, Mwea na Mombasa.

Wakamba huzungumza lugha ya Kikamba ambayo ina uhusiano wa kimsamiati na lugha nyingine za Kibantu kama vile Kimeru, Kiembu na Kikuyu. Kulingana na Mulatya (2013), lugha ya Kikamba imegawanyika katika lahaja tatu za kimaeneo. Ya kwanza ni lahaja ya Machakos inayozungumzwa katika Kaunti ya Machakos na baadhi ya sehemu za kaunti ya Makueni. Lahaja ya pili ni ya Kitui inayozungumzwa katika sehemu za Kitui na Mwingi zilizoko katika kaunti ya Kitui. Mwisho, ni lahaja ya Kilungu ambayo huzungumzwa katika maeneo ya vilima vya Kilungu katika Kaunti ya Makueni.

Historia hii ni muhimu katika utafiti huu kwani ilimwezesha mtafiti kueleza muktadha wa jamii, utamaduni na lugha unaojitokeza katika mtindo wa muziki wa Benga wa jamii hii.

1.2 Suala la Utafiti

Muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba ni maarufu na hutumika kama nyenzo ya kupitisha ujumbe muhimu katika nyanja mbalimbali za maisha ya jamii. Hata hivyo, licha ya ustadi wa matumizi ya mtindo katika muziki huu, bado kuna pengo la kitaaluma kuhusiana na uchanganuzi wa kina wa vipengele vya kimtindo. Kulingana na ufahamu wa mtafiti, tafiti za awali kuhusu muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba hazijalenga uchanganuzi wa mtindo kwa kuegemea mkabala wa kiisimu kwa kina, bali zimejikita zaidi katika maudhui na vipengele vya utendaji wa muziki huo. Jambo hili linaacha pengo katika kuelewa jinsi uchaguzi wa kimtindo unaofanywa na waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba unavyochangia katika kuibua

ujumi na kuendeleza utamaduni wa jamii hii. Ni katika msingi huu ambapo utafiti huu ulilenga kuchanganua mtindo katika muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba.

1.3 Madhumuni ya Utafiti

Madhumuni yafuatayo yaliundwa ili kuelekeza mchakato mzima wa utafiti na kumwezesha mtafiti kuziba pengo lililobainishwa.

1. Kubainisha mikakati ya kimtindo wanayotumia waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba kuwasilisha ujumbe.
2. Kuchanganua jinsi waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba wanavyotumia mikakati ya kimtindo kuimarisha ujumi kwenye muziki wao.
3. Kueleza athari lengwa za mikakati ya kimtindo wanayotumia waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba.

1.4 Maswali ya Utafiti

Maswali ya utafiti yaliundwa kwa kuzingatia madhumuni ya utafiti kama yafuatayo:

1. Waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba hutumia mikakati ipi ya kimtindo kuwasilisha ujumbe?
2. Waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba hutumia mikakati ya kimtindo vipi ili kuimarisha ujumi katika muziki wao?
3. Mikakati ya kimtindo wanayotumia waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba hulenga athari gani?

1.5 Sababu za Kuchagua Mada

Utafiti huu unahusu uchunguzi wa tofauti za kiisimu na vipengele vya kimtindo vinavyotumika katika muziki wa Benga, hususan katika jamii ya Wakamba. Kwa kuchunguza mtindo wa muziki huu, utafiti unatoa mwanga kuhusu uchaguzi wa kimtindo unaofanywa na wasanii. Hii inasaidia kuelewa jinsi lugha inavyotumika kama chombo cha ubunifu na utambulisho wa kitamaduni pamoja na mchango wake katika kuhifadhi na kuendeleza lahaja au mitindo ya mawasiliano ya jamii husika.

Muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba una seti yake ya vipengele vya lugha mahususi vinavyohusiana na utanzu huu pekee, ambavyo huchangia katika mtindo na utambulisho wake wa kipekee. Utafiti huu umechanganua na kubainisha vipengele hivi mahususi vya lugha, kama vile msamiati na miundo maalum ya sentensi ambayo hutofautisha muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba na aina nyinginezo za muziki.

Hatua hii ililenga kuonyesha jinsi vipengele hivi vinavyotumika kama njia ya kudumisha utamaduni na kuendeleza mawasiliano ya jamii ya Wakamba.

Mkabala wa umtindo huchunguza jinsi lugha inavyotumiwa kwa ubunifu na uwazi katika miktadha mbalimbali. Katika muktadha wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba, utafiti huu ulilenga kuonyesha namna ambavyo wanamuziki hutumia vipengele vya lugha kuwasilisha maana, mihemko na tofauti za kitamaduni. Kupitia uchunguzi wa tamathali za usemi na mbinu nyinginezo za kishairi, utafiti huu ulitazamia kubainisha jinsi mbinu hizi zinavyoimarisha nguvu za kujieleza na kuupa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba utambulisho wa kipekee.

Pia, mkabala wa umtindo huchunguza dhana ya uamilishi inayoangazia kile ambacho matini hunukuu, kurejelea au kuathiriwa nacho kutoka kwa matini nyingine. Utafiti huu ulichunguza mahusiano yaliyopo baina ya nyimbo mbalimbali na wasanii tofauti. Aidha, uliangalia jinsi vipengele vya lugha kutoka kwa mapokeo mengine ya muziki au utamaduni maarufu vinavyojumuishwa katika muziki wa Benga. Pia, uliangazia namna ambavyo vipengele hivyo huchangia kuunda mtindo na kuchochea mabadiliko yake. Hivyo basi, mada hii inatoa nafasi ya kubaini ubunifu na mnyambuliko wa lugha na sanaa katika kutunza na kuendeleza utambulisho wa jamii.

Uchaguzi wa kiisimu unaofanywa katika muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba unaathiri namna hadhira inavyoupokea na kuufasiri muziki huu. Utafiti huu uliangazia jinsi waimbaji wa muziki wa Benga wanavyotumia vipengele vya lugha kuathiri ushiriki wa kihisia wa hadhira, kuonyesha utambulisho wa kitamaduni na kujenga tajriba ya kisanaa. Kwa hivyo, mada hii ni muhimu katika kufafanua nafasi ya lugha kama nyenzo ya usanii, mawasiliano na uhifadhi wa utamaduni katika muziki wa Benga.

1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu una umuhimu katika nyanja za kitaaluma, kijamii na kisanii. Kwanza, katika taaluma ya isimu na fasihi, matokeo yake yanachangia kuendeleza uelewa wa matumizi ya mtindo katika muziki wa Benga na nyimbo za jamii kwa ujumla. Hii inasaidia kupanua wigo wa tafiti za Kiswahili kwa kuhusisha muziki kama nyenzo muhimu ya kisanaa na kifasihi. Pili, utafiti huu unaongeza thamani ya kitaaluma kwa kuwa kielelezo cha jinsi mbinu za kiisimu zinavyoweza kutumika katika uchambuzi wa muziki na hivyo kuchochea tafiti zaidi katika maeneo yanayohusiana.

Vilevile, katika muktadha wa kijamii, matokeo ya utafiti huu yanasaidia kuelewa nafasi ya muziki wa Benga katika maisha ya jamii ya Wakamba, hususan uhusiano wake na sherehe, hafla na mienendo ya kijamii. Kwa kufanya hivyo, utafiti huu unasaidia katika kuhifadhi na kuthamini urithi wa kitamaduni unaoonyeshwa kupitia muziki wa Benga. Aidha, kwa upande wa kisanaa, utafiti huu ni muhimu kwa waimbaji na watunzi wa muziki wa Benga kwani unawawezesha kuelewa kwa kina mbinu za kimtindo zinazoongeza mvuto, ujumi na athari ya kijamii ya kazi zao. Maarifa haya yanaweza kuwasaidia kuboresha ubunifu, kuongeza hadhi ya muziki wao na kuutumia kama jukwaa la mawasiliano yenye maana katika jamii. Hatimaye, matokeo ya utafiti huu yanachangia kukuza hadhi ya muziki wa Benga kama utanzu wa kifasihi na kisanaa katika Kiswahili.

1.7 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulichanganua mtindo katika muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba kwa kuzingatia mkabala wa kiisimu na kifasihi. Mtafiti alichanganua viwango vya mtindo vinavyoambatana na kielelezo cha nadharia ya umtindo ya Leech (1969) pekee. Ingawa utafiti huu haukulenga moja kwa moja kuchunguza maudhui, baadhi yake yalijitokeza katika muktadha wa kueleza athari lengwa ya wasanii wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba. Vipengele vingine vya muziki kama vile miondoko, mdundo na ala za muziki ambavyo ni muhimu katika taaluma ya muziki havikushughulikiwa katika utafiti huu, kwa kuwa upeo wake uko ndani ya taaluma ya lugha na fasihi. Hivyo basi, vipengele vya lugha pekee ndivyo vilivyoshughulikiwa katika utafiti huu, jambo lililoendana na malengo ya tasnifu hii na muda uliohitajika kukamilisha utafiti.

Ili kufanikisha uchambuzi huu, mtafiti alisikiliza muziki wa waimbaji wa Benga wa jamii ya Wakamba na kuteua nyimbo nane zenye vipengele vya kimtindo. Nyimbo hizo ziliteuliwa kulingana na uwezo wake wa kumwezesha mtafiti kufikia malengo ya utafiti na kujibu maswali ya utafiti huu. Kwa hivyo, utafiti huu unajikita katika taaluma ya isimu na fasihi na unachangia katika uwanja wa mtindo.

SURA YA PILI

MAPITIO YA MAANDISHI

2.0 Utangulizi

Katika sura hii yaliyoandikwa yalihakikiwa kwa misingi ya madhumuni ya utafiti. Pia, nadharia ya utafiti ilielezwa kwa kina ambapo waasisi walirejelewa pamoja na kufafanua mihimili ya nadharia kwa kurejelea viwango vyake mahususi.

2.1 Yaliyoandikwa kuhusu Mada ya Utafiti

Sehemu hii ilitathmini mchango wa kazi zinazohusiana na mada ya utafiti pamoja na kuweka wazi tofauti iliyopo kati ya tafiti hizo na utafiti huu.

2.1.1 Mikakati ya Uimbaji

Mikakati ya Kimtindo ina nafasi ya kipekee katika kufanikisha maana na madhumuni ya msanii (Leech, 1969). Mikakati hii hurejelea mbinu mbalimbali za kimakusudi za lugha na fasihi ambazo waandishi, washairi na wanamuziki hutumia ili kuunda maana, kuchochea hisia na kufanikisha athari mahususi za mawasiliano (Graebner, 1992). Kwa mujibu wa Leech (keshatajwa), vipengele hivi vya kimtindo haviboreshi tu mvuto wa kazi ya fasihi, bali pia vinaelekeza mwitikio wa hadhira na kuathiri namna kazi inavyofasiriwa. Hivyo basi, kwa kuchunguza kwa kina mikakati kama vile sitiari, taswira, urudiaji na mkengeuko wa kisarufi, mtafiti aliweza kubaini jinsi lugha inavyotumika kama chombo cha ushawishi, urithishaji wa tamaduni na uwasilishaji wa ujumi wa kisanaa.

Syahrina (2019) alichunguza mtindo wa lugha katika nyimbo za Katty Perry zinazojulikana kama *witness*. Alitumia Nadharia ya umtindo iliyoasisiwa na Leech na Short inayohusu uchunguzi wa kiisimu kuhusu mtindo wa lugha. Pia, alitumia nadharia ya lugha ya kitamathali ya Laurence Perrine. Alitumia mbinu ya kimaelezo pamoja na uchanganuzi matini kuchanganua data zake. Aligundua kuwa lugha ya kitamathali iliyotumika katika nyimbo hizo ni pamoja na tashbihi, sitiari, ishara, chuku na majazi. Hata hivyo alibaini kuwa mbinu ya sitiari ilitawala katika nyimbo hizo kwa kiwango kikubwa. Matumizi ya sitiari katika muziki huo yalilenga kuinua hadhi ya mwanamke katika siasa za Amerika wakati huo. Utafiti wake ulishughulikia vipengele vya tamathali za lugha kama vile sitiari, kinaya na tashihisi pekee ilhali utafiti huu ulishughulikia vipengele vingine vya mitindo ya kiisimu katika muziki wa

Benga wa jamii ya Wakamba. Hata hivyo utafiti wa Syahrina ulimsaidia mtafiti katika kuchanganua data zake kwa kuongozwa na nadharia ya umtindo.

Putra (2017) alitumia mbinu ya kimaelezo kuchunguza maana ya leksimu katika nyimbo za *Scorpion*. Alizingatia nadharia ya semantiki ya kiisimu yake Lyon 1981 kuchanganua data zake. Ilibainika kuwa maana ya kileksimu inayojitokeza katika nyimbo za *scorpion* ni pamoja na sinonimu, haiponimu, tashbihi, chuku, sitiari, majazi na antonimu. Hata hivyo, sinonimu ilitumika zaidi katika nyimbo za *scorpion* ambapo misamiati tofauti ilitumika kurejelea maana moja. Mchango wa Putra ulikuwa muhimu katika utafiti huu kwani ulimsaidia mtafiti kufafanua mikakati ya kimtindo wanayotumia waimbaji wa Benga ya jamii ya Wakamba. Kwa kuwa utafiti wake ulichunguza maana ya leksimu pekee, utafiti huu uliangazia vipengele vingine vya kiisimu katika muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba.

Vilevile, utafiti wa Chimbarange (2019) ulionyesha kuwa waimbaji hutumia sitiari kuunda, kusisitiza na kuendeleza maoni na misimamo yao kuhusu masuala ya kijinsia, ambapo matokeo yalionyesha kuwa sitiari hizo mara nyingi humtukuza mwanamume huku zikimdhalilisha mwanamke. Matokeo haya yalisaidia kutoa mwongozo wa utafiti huu kwa kuwa yalibainisha nafasi ya sitiari kama mkakati wa kimtindo katika muziki. Hata hivyo, kuna pengo la kimaudhui na kijiografia kati ya tafiti hizi mbili: Chimbarange alishughulikia nyimbo za Kishona za Zimbabwe na alijikita katika mkakati wa sitiari pekee, ilhali utafiti huu unashughulikia muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba nchini Kenya na unapanua wigo kwa kuchunguza si tu matumizi ya sitiari, bali pia mikakati mingine ya kimtindo kama urudiaji na takriri. Hivyo basi, utafiti huu unalenga kuziba pengo hilo kwa kuonyesha namna mitindo ya kiisimu inavyotumika kwa upana zaidi katika muziki wa Benga wa Wakamba.

Timmamy (2010) alifanya uchunguzi wa kimtindo katika lugha inayotumika katika nyimbo za harusi za wanawake wa Mombasa. Utafiti wake ulilenga kuchunguza mtindo katika viwango vya fonolojia, leksimu, sintaksia na semantiki kwa kutumia mtazamo wa umtindo wa Leech 1969. Aligundua kuwa nyimbo za harusi za wanawake wa Mombasa zimetawaliwa na urudiaji wa maneno na leksimu kwa kiwango kikubwa. Vilevile alibaini kuwa ishara za lugha zenye maana fiche zimetumika katika nyimbo hizo za harusi pamoja na kuchanganya msimbo ambapo maneno ya Kiingereza yametumika kwa wingi. Kwa sababu utafiti wake

ulishughulikia nyimbo za harusi za wanawake wa Mombasa, ni tofauti na utafiti huu ambao ulishughulikia mtindo katika nyimbo za Benga za jamii ya Wakamba. Utafiti huu ulifaidika kutokana na nadharia ya umtindo kama ilivyotumika katika utafiti wake kwa kuongoza mtafiti katika kutambua viwango vya mtindo vinavyopatikana katika muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba.

Mwangi na Munyao (2016) walichunguza mtindo na maudhui katika Nyimbo za Kisiasa za Msanii John De'Mathew nchini Kenya. Walifafanua vipengele vya mtindo vinavyotumika katika nyimbo za kisiasa za msanii huyo kama vile tanakali za usemi, jazanda, balagha, tashihisi na chuku. Walibaini kuwa vipengele hivi vya kimtindo hutumika ili kuwezesha wanasiasa kuwasilisha malengo yao kwa hadhira lengwa. Matokeo ya utafiti wa Mwangi na Munyao ni muhimu katika utafiti huu kwani yalimwongoza mtafiti katika kutambua mikakati ya kimtindo inayotumika katika muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba. Kinyume na utafiti wao uliochunguza nyimbo za mwimbaji wa jamii ya Gikuyu, utafiti huu ulichunguza waimbaji wa muziki wa jamii ya Wakamba.

Motanya na wenzake (2021) walichanganua ukiushi kama elementi ya kimtindo katika baadhi ya riwaya za Ken Walibora. Utafiti huu ulionyesha jinsi chaguo za lugha zinazofanywa na wasanii zinavyowezesha kupitisha masuala ya kijamii, maana na athari lengwa kwa hadhira. Kazi ya Motanya na wenzake ni muhimu katika utafiti huu kwani ilimwongoza mtafiti kuchanganua mikakati ya ukiushi katika muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba. Isitoshe, utafiti wao ulichunguza mtindo katika riwaya ambayo ni kazi ya fasihi andishi ilhali utafiti huu ulishughulikia muziki ambao ni kazi ya fasihi simulizi.

Mue na wenzake (2024) walichunguza mkakati wa jazanda katika nyimbo za kiasili za Kikamba. Walibaini kuwa matumizi ya jazanda katika nyimbo za kiasili za Kikamba huzua urembo wa kisanaa wa lugha. Mkakati huu huzifanya nyimbo za kiasili za Kikamba zipendeze hadhira na kuivutia kuzisikiliza. Utafiti wao ulimwongoza mtafiti kufahamu sababu zinazopelekea waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba kutumia mikakati ya kimtindo. Tofauti na utafiti wao ulioshughulikia mkakati wa jazanda pekee, utafiti huu ulibainisha aina nyingine za mikakati ya kimtindo katika muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba.

Kipkirui (2021) alitathmini tafsida zinazohusiana na mapenzi katika muziki maarufu wa jamii ya Kipsigis akitumia muundo wa nadharia ya upole. Aligundua kuwa wasanii hujaribu kujiepusha na aibu kwa kutumia maneno na dhana za kitafsida. Utafiti wa Kipkirui ulitoa mwongozo wa utafiti huu katika kuchanganua mikakati wanayotumia waimbaji wa muziki wa Benga kupitisha ujumbe wao. Utafiti wa Kipkirui umeangazia nyimbo za Kipsigis kwa kuzingatia nadharia ya upole tofauti na utafiti huu ambao ulishughulikia muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba kwa kuongozwa na nadharia ya umtindo.

Muema (2019) na Wathome (2013) wamechangia katika utafiti wa mitindo ya lugha katika nyimbo za jamii ya Wakamba. Muema (ametajwa) alijikita katika uchunguzi wa tafsida katika muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba. Kwa kutumia nadharia ya urejeleo alibaini kuwa uelewa wa muktadha huwezesha wasikilizaji kutafsiri tafsida kwa usahihi. Utafiti wake ulilenga tafsida pekee, hivyo kutoa nafasi kwa utafiti huu kupanua upeo kwa kutumia mkabala wa umtindo kuchunguza aina nyingine za mitindo ya lugha katika muziki wa Benga wa Kikamba. Vilevile, Wathome (keshatajwa) alitafiti mtindo katika nyimbo za tohara za jamii ya Wakamba. Alibaini nyimbo hizo zilitawaliwa kwa kiasi kikubwa na tamathali za usemi. Ingawa utafiti wake ulilenga nyimbo za kitamaduni, matokeo yake yalitoa mwanga kuhusu matumizi ya lugha ya kitamathali ambayo pia hutumika katika muziki wa Benga. Tofauti na tafiti hizi mbili, utafiti huu unazingatia mkabala wa umtindo kudhihirisha viwango mbalimbali vya lugha vinavyojitokeza katika muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba, hasa katika nyimbo zilizopendwa.

2.1.2 Suala la Ujumi katika Muziki

Uchunguzi wa ujumi wa kisanaa katika muziki huhusisha uchambuzi wa jinsi vipengele vya kisanaa vilivyo ndani ya tungo za muziki vinavyochochea hisia, kufikisha maana za kitamaduni na kuunda mtazamo wa hadhira. Sifa za kiujumi kama vile wizani, melodi, mdundo na lugha ya kishairi si mapambo tu, bali ni nguzo kuu zinazotoa nguvu ya mawasiliano katika nyimbo (Leech, 1969; Scruton, 1997). Kwa mujibu wa Tagg (2012), ujumi katika muziki hufanya kazi kama jambo la kawaida na la utamaduni mahususi, ambapo wasikilizaji hufasiri kazi za muziki kupitia ishara na mitindo inayotambulika kijamii. Katika muktadha wa Kiafrika, Stapleton & May (1987) waliangazia jinsi muziki wa Benga unavyopata mvuto wake wa kiujumi kupitia muungano wa lugha za asilia, midundo ya kitamaduni na ustadi wa kupiga

gitaa kwa ubunifu. Utafiti huu unalingana na utafiti wao kwa kuwa unazingatia muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba ulio katika muktadha wa Kiafrika. Utafiti huu unapanua mkabala wa umtindo kwa kuangazia jinsi vipengele vya lugha na mtindo vinavyobadilika na kuakisi utambulisho wa jamii ya Wakamba.

Afipah na wenzake (2022) walifanya uchanganuzi hakikifu wa diskosi katika wimbo wa Justin Bieber unaojulikana kama *Lonely*. Kwa kuzingatia nadharia ya Van Dijk ya uchanganuzi wa diskosi. Waligundua kuwa maneno yaliyotumika katika wimbo huo yalikuwa sahili na yaliambatana na ishara za lugha ambazo ni rahisi kueleweka na hadhira lengwa. Sababu kuu ya mwimbaji kutumia maneno sahili na ishara hizo za lugha, ilikuwa ni kuivutia hadhira yake. Tofauti na utafiti wao, utafiti huu ulijikita katika mkabala wa umtindo kuchanganua vipengele vya mtindo vilivyotumika katika muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba. Hata hivyo utafiti wao ni muhimu katika utafiti huu kwani ulikuwa mwongozo wa kufahamu aina za maneno wanazotumia wasanii wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba ili kufanikisha ujumi.

Laswai (2015) alichunguza ujumi katika muziki wa densi wa nyimbo teule za Marijani Rajabu na Ally Choki. Alizingatia nadharia ya Kimaksi kuthibitisha iwapo taaluma ya ujumi ina nafasi kubwa katika kazi za muziki wa densi. Kutokana na utafiti wake, ilibainika kuwa uzuri hutambulika kwa namna tofauti katika jamii mbalimbali. Kwa mfano katika baadhi ya jamii uzuri hujengwa kupitia sifa za mwonekano wa kimwili kama umbo au rangi ya ngozi, ilhali katika jamii nyingine uzuri huweza kuhusishwa na maadili mema, ujuzi wa sanaa au kipaji cha muziki. Pia, kuna jamii zinazotambua uzuri kupitia mavazi ya kitamaduni na mapambo ya kifani, wakati zingine huelekeza uzuri katika nafasi na heshima ya kijamii anayoshikilia mtu. Aidha, alionyesha kuwa matumizi ya vipengele vya kiujumi katika fani na maudhui ya nyimbo huchangia kuburudisha, kuelimisha, kuonyesha nafasi ya mwanamke katika jamii na kuutambulisha utamaduni wa jamii husika. Matokeo yake yalitoa mwongozo muhimu kwa utafiti huu katika kuchunguza nafasi ya ujumi. Hata hivyo, tafiti hizi zinatofautiana kwa kuwa Laswai alijikita katika muziki wa densi na akatumia misingi ya nadharia ya Kimaksi, ilhali utafiti huu ulishughulikia muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba kwa mwongozo wa nadharia ya umtindo.

Bitabaje (2017) alizingatia nadharia ya upokezi kutathmini hali ya kupendwa kwa nyimbo za injili za Christina Shusho kama fasihi pendwa. Alibaini kuwa nyimbo za injili huwa na wapenzi wengi katika jamii. Hii ni kutokana na haiba ya mwimbaji, jinsi anavyoimba pamoja na maudhui yanayowasilishwa ambayo huivutia jamii. Utafiti huu ulitoa mwongozo wa kuchanganua namna waimbaji wa muziki wa jamii ya Wakamba huimarisha ujumi katika muziki wao. Utafiti huu ni tofauti na utafiti wa Bitabaje kwa kuwa alishughulikia nyimbo za injili za Christina Shusho ilhali utafiti huu ulihusisha muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba.

Mutisya na Muhoro (2022) walichunguza thamani ya ujumi na utendaji katika nyimbo za michezo za watoto wa jamii ya Wakamba. Walitumia nadharia ya ethno-poetiki yake Hymes (1991) kama mwongozo wa uchambuzi. Kwa kutumia mbinu ya uchunzaji walibaini kuwa nyimbo hizi zimejikita kwa kina katika tamaduni za jamii ya Wakamba na hutumika kama vyombo vya kuwasilisha thamani muhimu za ujumi wa kisanaa. Hasa, nyimbo hizo zinasisitiza thamani za ujumi wa masuala halisi kama vile; urafiki na umoja, uwajibikaji, ufahamu wa masuala ya mazingira, uhusiano wa ukoo, tamaduni na thamani ya bidii kazini na kukwepa uvivu. Utafiti wao unaonyesha jinsi ujumi unavyoimarishwa katika nyimbo hususan za watoto wa jamii ya Wakamba. Hata hivyo, mtazamo wao umesalia katika nyimbo za michezo ya watoto pekee na haujapanuliwa kujumuisha aina nyingine za muziki wa kisasa kama vile muziki wa Benga, ambao umeibuka kama njia yenye ushawishi mkubwa wa uelezaji wa kitamaduni miongoni mwa jamii ya Wakamba. Hivyo basi, kuna pengo katika kuelewa jinsi wasanii wa Benga wa jamii ya Wakamba wanavyotumia mikakati ya kimtindo kuimarisha ujumi katika nyimbo zao. Utafiti huu ulijishughulisha na kuziba pengo hili kwa kuchanganua jinsi waimbaji wa muziki wa Benga jamii ya Wakamba wanavyotumia mikakati ya kimtindo kuimarisha ujumi.

2.1.3 Athari Lengwa za Matumizi ya Mikakati ya Kimtindo

Dhana ya “athari lengwa” inahusiana na matokeo kusudiwa ambayo wasanii wa muziki na watungaji wa nyimbo hulenga kufikia kupitia uchaguzi wao wa mtindo, iwe ni hisia, utambuzi au masuala ya kijamii. Kwa mujibu wa Juslin na Västfjäll (2008), athari lengwa ni majibu ya hisia za kisaikolojia zinazokusudiwa na ambazo huibuka miongoni mwa wasikilizaji kutokana na ishara za muziki na mbinu za mtindo. Uchunguzi wa athari lengwa za mikakati ya mtindo ni muhimu katika kuelewa jinsi muziki unavyofanya kazi kama njia ya mawasiliano na jinsi unavyoathiri mtazamo na

tabia za wasikilizaji. Sehemu hii inapitia tafiti zilizopo kuhusu jinsi mbinu mbalimbali za mtindo zinavyotumika kuzalisha athari maalum.

Jumbe (2015) alizingatia nadharia ya umuundo kuchunguza matumizi ya lugha katika muziki wa kizazi kipya akirejelea mifano katika nyimbo za mapenzi za wasanii inspekta Haroun na Mwanafalsafa. Alibaini kuwa matumizi ya lugha katika muziki wa kizazi kipya hasa tungo za kimapenzi hutokana na sababu kama vile kuonyesha hisia za kimapenzi kwa wapendanao na kuwezesha wasanii kudhibiti soko la muziki. Vilevile aligundua kuwa tija zinazotokana na matumizi ya lugha katika muziki huo ni pamoja na kuburudisha jamii, kudumisha mahusiano ya kijamii na kutajirisha msamiati wa lugha. Hata hivyo alibaini kuwa matumizi ya lugha katika muziki wenye vionjo vya kimapenzi huweza kuleta madhara katika jamii. Madhara haya ni pamoja na utovu wa maadili, kujiingiza katika mahusiano ya kimapenzi katika umri mdogo na kudumaza ubunifu. Kwa kuwa utafiti wa Hussein umeshughulikia muziki, ulimwongoza mtafiti kuchunguza athari lengwa za wasanii wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba. Utafiti huu unatofautiana na utafiti wake kwa kuwa ulichanganua mtindo wa lugha kwa kuzingatia viwango vya nadharia ya umtindo ilihali wa Hussein ulizingatia nadharia ya umuundo.

Mukandabvute na Gores (2021) walichunguza athari za kimaadili zinazotokana na nyimbo za muziki wa Sing'eli nchini Tanzania. Nadharia ya muziki simulizi na nadharia ya uhalisia wa kiafrika zilitumika kuchanganua data za utafiti wao. Waligundua kuwa zipo nyimbo za muziki wa Sing'eli zenye athari chanya na athari hasi. Athari hizo ni kama vile, kudumisha umoja, kukemea ushirikina, kuchochea ugomvi na unyanyasaji wa kijinsia. Utafiti huu ulimwelekeza mtafiti kueleza athari lengwa za wasanii wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba katika kuendeleza maudhui. Watafiti hawa wameshughulikia nyimbo za muziki wa Sing'eli nchini Tanzania, jambo ambalo ni tofauti na utafiti huu ambao umeshughulikia muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba nchini Kenya.

Saad (2014) alichunguza dhima za matumizi ya ufutuhi katika nyimbo za sherehe za unyago za Wazaramo. Misingi ya nadharia ya uhalisia iliongoza uchanganuzi wa data zake. Alishughulikia vijenzi vya ufutuhi kama vile kejeli, balagha, dhihaka na vijembe. Utafiti wake ulionyesha kuwa hali ya hofu, utani na sababu za kihistoria ndizo huwafanya Wazaramo kutumia tungo za kifutuhi katika sherehe zao za unyago.

Watunzi wa futuhi hizo hulenga kuchochea fikra na hisia za hadhira lengwa. Vilevile ilibainika kuwa ufutuhi huchopekwa katika tungo ili kuifanya hadhira kuzielewa kwa njia ya ucheshi na tabasamu. Utafiti huu ulimwongoza mtafiti kutambua athari lengwa ya mitindo ya kiisimu wanayotumia waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba. Utafiti wa Saad unatofautiana na utafiti huu kwa kuwa ameshughulikia ufutuhi katika nyimbo za sherehe za unyango za wazaramo ilhali utafiti huu unahusu mtindo wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba.

Nduku (2020) alichunguza jinsi ubabedume unavyochorwa katika muziki maarufu wa jamii ya Wakamba. Aliongozwa na nadharia ya utendaji, nadharia ya ufeministi na nadharia ya ethnopoetiki. Aligundua kuwa uchaguzi wa lugha wanazotumia wasanii wa nyimbo hizo kulichangia katika kuwasilisha jenda zote mbili kwa hali tofauti na za kiubaguzi. Lugha ya kuvutia ilitumika kuwasilisha mwanaume huku lugha ya kudunisha ikitumika kuwasilisha mwanamke. Vilevile ilibainika kuwa ujumi ulitumika kama mbinu muhimu ya kuendeleza utambuzi wa kijenda. Pia aligundua kuwa wanawake wenyewe walichangia katika udunishaji wao wa kijenda kupitia miondoko yao ya kimapenzi katika uchezaji wa miziki hiyo maarufu. Kwa kuwa utafiti wa Nduku umejikita tu kwenye uchoraji na uendelezaji wa hejimonia ya ubabedume pekee, kuna haja ya kuchunguza jinsi mtindo unavyochorwa katika muziki huu maarufu wa jamii ya Wakamba ili kuendeleza maudhui mengine. Utafiti wake ulikuwa muhimu katika utafiti huu kwani umechunguza nyimbo za jamii ya Wakamba ambazo ndizo nguzo kuu ya utafiti huu.

2.2 Misingi ya Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya umtindo kama ilivyoelezwa na Geoffrey Leech (1969). Chimbuko na historia ya nadharia ya umtindo linaonyesha kwamba dhana hii ilianza kutumika kwa mara ya kwanza mwaka 1882 katika Kamusi ya Kiingereza ya Oxford ikimaanisha sayansi ya mtindo wa uandishi au fasihi (Zhukovska, 2010). Asili yake ilihusiana na balagha na mashairi ya kale ambapo mtindo ulionekana kama njia ya pekee ya kujieleza na kupamba mawazo kupitia kanuni za upangaji wa maneno na matumizi ya tamathali. Baada ya hapo, mbinu ya kawaida iliibuka, ikijaribu kutathmini namna lugha ya kitaifa inaweza kutumika kitaalamu, kama ilivyoonekana katika kazi ya Spenser (1852). Hatimaye, mwaka 1909 Charles Bally alipinga mtazamo wa ukawaida na kusisitiza umuhimu wa mtindo katika kuonyesha hisia na mawasiliano, hatua iliyoanzisha umtindo kama taaluma huru ya isimu katika karne ya

ishirini. Kwa sasa, umtindo unafafanuliwa kama tawi la isimu linalochunguza athari za uchaguzi wa lugha katika mawasiliano, huku uhusiano wake na balagha ukionekana katika matumizi ya vipengele vya kimtindo kufanikisha mikakati ya kushawishi na kufahamisha (Brewer, 2017).

Nadharia ya umtindo huchunguza matumizi ya lugha kwa mtazamo wa kiisimu na kifasihi. Inaangazia jinsi lugha inavyotumika katika muktadha maalum na kwa lengo maalum, ikisisitiza kuwa mbinu za lugha kama vile jazanda, sitiari na kinaya haziwezi kueleweka bila kurejelea muktadha wa kiisimu. Leech (1969) anaeleza kuwa, umtindo ni kiunganishi kati ya isimu na fasihi kwani huchunguza zaidi jinsi jambo linavyosemwa kuliko ujumbe wenyewe. Maoni haya yanaungwa mkono na Indangasi (1998), anayesisitiza kuwa umtindo hujihusisha na namna lugha inavyotumika kuleta mvuto wa kisanaa au ujumi. Wataalamu wengine walioshughulikia nadharia hii ni pamoja na Wamitila (2008), Miles (1971), Crystal & Davy (1969, 1981) na Saussure (1983).

2.2.1 Viwango vya Nadharia ya Umtindo

Nadharia ya umtindo ina viwango mbalimbali vinavyoweza kuchunguzwa kulingana na Leech na Short (1981). Viwango hivyo ni: kiwango cha udhihirikaji, kiwango cha umbo, kiwango cha semantiki na matawi saidizi ya isimu (Leech, 1969).

2.2.1.1 Kiwango cha Udhihirikaji

Kiwango hiki kinahusu jinsi maumbo ya lugha yanavyotamkwa (fonolojia) na kuandikwa (grafolojia). Leech (1969) anadokeza kuwa sentensi huweza kupitishwa kwa kuandikwa au kutamkwa. Kwa hivyo, mtu mwenye umilisi wa lugha fulani anatarajiwa kuzijua kanuni za utamkaji na uandishi wa lugha hiyo. Vipengele vinavyochunguzwa chini ya kiwango hiki ni pamoja na;

Grafolojia: kiwango hiki hujihusisha na mpangilio wa maumbo ya lugha iliyoandikwa. Khan na Jabeen (2015) wanakiona kiwango hiki kama utafiti wa mtaala mzima wa uandishi wa lugha fulani. Leech (1969) aligundua kuwa grafolojia ni zaidi ya othografia ya lugha fulani kwani grafolojia ni shughuli nzima ya mtaala wa uandishi wa lugha. Grafolojia ni kiwango cha uchanganuzi wa lugha kinachojishughulisha na mpangilio wa sauti katika maandishi, umbo na upana wa maneno pamoja na sifa zingine za othografia ya lugha fulani. Sifa zinazoshughulikiwa chini ya grafolojia ni pamoja na alama za uakifishaji, italiki, ugawaji wa aya na

ukubwa au udogo wa alama za kiothografia, viwango vya nafasi katikati mwa maneno na sentensi. Umuhimu wa grafolojia katika uandishi ni uchimuzaji ili kuvutia jicho la msomaji na kuonyesha lengo la mwandishi moja kwa moja.

Fonolojia: hiki ni kiwango kinachojihusisha na uchunguzi wa mtaala wa sauti za lugha fulani pamoja na kanuni zinazotawala utamkaji wa sauti za lugha hiyo (Khan na Jabeen ,2015). Kiwango hiki hujihusisha na jinsi vipengele vya sauti husaidia kupata umuhimu wa kimtindo katika tamko au maandishi. Kulingana na Alabi (2007), kiwango hiki kinahusu sauti au ujumlishaji wa sauti za lugha tofauti. Farinde na Ogunsiji (2015) wanadokeza kwa kuwa lugha kimsingi huwa ya kuzungumza, hivyo kiwango hiki ndicho muhimu zaidi katika uchanganuzi wa mkabala wa umtindo. Kwa mujibu wa Leech (1969) baadhi ya vipengele vya kimtindo vinavyochunguzwa chini ya fonolojia ni kama vile onomatopoeia, urudiaji wa vokali na konsonanti, uradidi, urari, utiliaji mkazo, wizani na toni. Leech (ameshatajwa) anaviona viwango vya grafolojia na fonolojia kama viwango vinavyoingiliana au kuhusiana, kwani grafolojia huiga fonolojia. Kiwango hiki kilimwongoza mtafiti kuonyesha vipengele vya grafolojia na fonolojia katika muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba.

2.2.1.2 Kiwango cha Umbo

Kiwango hiki kinahusu uteuzi wa msamiati na maneno maalum na jinsi msamiati huo unavyotumika kuunda sentensi. Leech (1969) alidokeza kuwa hiki ni kiwango cha kisintaksia kwani kinahusisha sarufi. Vipengele vifuatavyo ndivyo vinavyochunguzwa chini ya kiwango hiki:

Leksimu: kwa kawaida, leksimu hurejelea maneno katika lugha fulani. Hiki ni kiwango cha kimtindo kinachojihusisha na maneno, istilahi na dhana za lugha fulani; ni kiwango cha uteuzi wa msamiati. Utafiti wa mtindo wa leksimu hujihusisha na kuonyesha sifa za kimsingi za neno katika sentensi. Khan na Jabeen (2015) wanakiona kiwango cha uchanganuzi wa mtindo wa leksimu kama utafiti wa jinsi maneno yanavyopangiliwa katika miktadha mbalimbali. Kwa mujibu wa nadharia ya umtindo, kiwango hiki pia kinahusu kuchanganya ndimi au kuhamisha msimbo na matumizi ya maneno ya kigeni au ya kukopa, maneno ya kale na ya kubuni. Kwa mujibu wa Leech (keshatajwa) leksimu na lugha huwa na uhusiano kwani sentensi huundwa kwa kutumia maneno.

Katika kiwango hiki utafiti huu ulijishughulisha na kuchunguza vipengele vya uteuzi wa msamiati au leksia. Vilevile utafiti huu ulichunguza jinsi waimbaji wanavyorudia leksimu fulani ili kusisitiza ujumbe wao.

Mofolojia: huu ni uchunguzi wa jinsi maneno yanavyoumbwa au uchunguzi wa jinsi mofimu (kipengele kidogo cha neno) ziwe, huru au funge, zinavyounda maneno. Kwa mujibu wa Leech (ametajwa), kiwango hiki ni muhimu katika kuelewa jinsi muundo wa maneno unavyochangia katika mtindo na maana ya lugha. Ni uchunguzi wa muundo wa maneno yakijumuisha mizizi na viambishi. Mtazamo wa Leech kuhusu mofolojia unazingatia jinsi maumbo tofauti ya kimofolojia yanavyoweza kusababisha tofauti za maana, mtindo na mkazo katika lugha. Katika mtindo, mofolojia hutumiwa kuchanganua uchaguzi wa maneno, maumbo ya maneno na athari zake kwa toni, hisia na sajili. Leech (ametajwa) anafafanua vipengele muhimu vya mofolojia kama vifuatavyo;

Uundaji wa neno: katika kiwango hiki, Leech anaeleza jinsi maneno yanavyoundwa kupitia michakato mbalimbali kama vile unyambulishaji (kuongeza viambishi awali au viambishi tamati kwa mzizi wa neno), kuambatanisha (kuunganisha maneno mawili au zaidi pamoja) na ubadilishaji (kubadilisha kategoria ya kisarufi ya neno, kama kugeuza nomino kuwa kitenzi). Taratibu hizi husaidia kuunda maumbo tofauti ya maneno ambayo yanaweza kubadilisha jinsi sauti au maandishi yanavyosikika au kusomeka.

Uambishaji: kiwango hiki hurejelea mabadiliko katika umbo la neno ili kueleza vipengele vya kisarufi kama vile tenzi, umoja au wingi (kwa mfano, tembea → kutembea au mtoto → watoto). Leech (ametajwa) anadokeza kuwa viambishi huchangia muundo na mdundo wa sentensi, na kusaidia kubainisha wakati, kipengele au wingi, ambao huathiri moja kwa moja maana na mtindo.

Mofimu tanzu: hizi ni mofimu zinazoongezwa kwenye mzizi wa neno ili kuunda neno jipya. Mara nyingi hubadilisha maana ya neno au kategoria ya kisarufi. Kwa mujibu wa Leech (ametajwa), kipengele hiki husaidia kuchanganua jinsi viambishi fulani hubadilisha utendakazi wa neno na kuathiri hali au toni ya kazi ya sanaa.

Tofauti za kimofolojia/mifanyiko ya kimofolojia: nadharia ya umtindo inasisitiza matumizi ya maumbo mbalimbali ya kimofolojia ili kuunda athari za kimtindo. Kwa

mfano, katika matini za kifasihi, waandishi wanaweza kutumia maumbo adimu au rasmi ya maneno ili kuleta hali ya uchangamano, au wanaweza kutumia maumbo ya mazungumzo kuunda sauti za kawaida ama zinazofahamika zaidi. Kwa mujibu wa Jolayemi (2008) kuna aina tofauti za mifanyiko ya kimofolojia ila jambo muhimu zaidi katika mofolojia ni uumbaji wa maneno.

Sintaksia: kiwango hiki hujishughulisha na vipengele vya kimtindo vinavyojitokeza katika sentensi. Kwa kawaida mazungumzo huhusisha matumizi ya sentensi wala si maneno pweke. Jolayemi (2008) anadokeza kuwa sintaksia ni uchunguzi wa jinsi maneno yanavyopangiliwa kuunda tamko fulani au sentensi za lugha maalum. Hiki ni kiwango cha sarufi. Kulingana na Khan na Jabeen (2015), lengo la kiwango hiki ni kuchanganua muundo wa ndani wa sentensi katika lugha na umuhimu wa sentensi hizo zinapopangiliwa kwa mpangilio maalum (usambamba). Pia, kiwango hiki huchunguza matumizi ya nomino na vitenzi katika sentensi, dhana, maneno na istilahi zinazotumika. Kulingana na Jakobson (1960) usambamba ni ruwaza ambazo hutokea mahali ambapo kuna vokali au konsonanti zinazofuatana kwa mfululizo maalum.

Katika kiwango hiki ruwaza huchunguzwa katika sentensi kwa haja ya kuona kama kuna mfanano wa vitenzi katika sentensi zinazofanana na sentensi za kupingana. Kitengo hiki hutazama sentensi na mifumo yake. Tunaangalia sentensi ambazo hukiuka sheria na kaida za lugha kama matumizi ya parendesi na tanakuzi. Tunatalii ukiushi; tunachunguza urefu wa sentensi, sentensi fupi zinatazamwa kama sahili na ndefu kama changamano. Kutegemea umaratokezi wake tunazitaja kama ni kiushi au chimuzi. Leech (keshatajwa) anadokeza aina za ukiushi wa kaida za lugha ambazo hutokea katika mtindo wa kazi za fasihi. Aina hizo ni kama vile; ukiushi wa kifonolojia/grafolojia, kisarufi, kileksia, kilahaja/dialektolojia, kisemantiki, kimapisi na ukiushi wa sajili. Aina nyingine za sentensi zinazochunguzwa chini ya kitengo hiki ni pamoja na sentensi tongole, za maswali na sentensi zenye muundo huru.

Kiwango hiki kilimwelekeza mtafiti kutambua msamiati (wa kale au wa kisasa/msamiati wa kubuni) na aina za sentensi zinazotumika katika muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba. Pia kilimsaidia mtafiti kueleza jinsi waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba huimarisha ujumi katika muziki wao.

2.2.1.3 Kiwango cha Kisemantiki

Kiwango hiki kinahusu miundo na lugha ya kitamathali ambayo ni muhimu katika kuchunguza kazi ya fasihi kwa kuzingatia nadharia ya umtindo. Ni namna lugha inayotumiwa huathiri maana katika kazi ya fasihi. Kiwango hiki kinahusu matumizi ya maneno na jinsi maana za maneno hayo zinavyofasiriwa katika hali za kawaida. Vipengele vinavyochunguzwa katika kiwango hiki ni pamoja na:

Semantiki: hiki ni kiwango kinachojihusisha na maana ya maneno na sentensi za lugha fulani. Katika kiwango hiki maneno yanaweza kutumiwa kutabiri, kujenga maudhui au kuleta maana ya kimtindo kutegemea lengo la msemaji au mwandishi. Pia, kiwango hiki hujulikana kama "maana ya kimtindo." Leech (1969) anakiona kama kiwango cha utafiti wa maana. Kwa mujibu wa Leech (ametajwa) kuna aina mbili za maana zinazoweza kuchunguzwa chini ya kiwango hiki, maana ya kimsingi na maana ya kimtindo.

Maana ya kimsingi ni maana finyu, ya kimantiki au ya uashiriaji wa neno, dhana au tamko. Ni aina ya maana ambayo waandishi wa kamusi huzingatia. Maana hii inarejelea uwazi na ukweli wa usemi bila kuingiza hisia au athari za kimkutadha. Hii ndiyo maana kuu ya neno ambayo haibadiliki. Kwa mujibu wa Leech (ametajwa) aina hii ya maana ndiyo huwa lengo kuu katika mawasiliano ya kisayansi au kiufundi, bila nafasi ya maana nyingine zaidi.

Maana ya kimtindo ni maana pana zaidi na ya kina. Inajumuisha yale yote ambayo huwasilishwa na neno, dhana au kifungu, ikijumuisha sio tu maana ya kimsingi bali pia vipengele vya hisia, mitazamo na maudhui yanayohusika katika mawasiliano. Kwa mujibu wa Leech (ametajwa), aina hii ya maana ni muhimu hasa katika miktadha ya kazi za kubuni. Kwa mfano katika ushairi, vipengele vya kihisia na kifasihi vina mchango mkubwa katika kuunda umuhimu wa jumla wa shairi. Maana ya kimsingi katika ushairi, ingawa bado iko, mara nyingi huwa ni sehemu ndogo ya mawasiliano yote, ambayo pia huhusisha vipengele vya ishara, hisia na ujumi.

Indangasi (1988) anaangazia zaidi kiwango hiki kwa kubainisha aina mbalimbali za ukiushi wa kisemantiki kama vile; uziada, ubwege na utata wa maana. Chini ya uziada wa kisemantiki, anatambua vipengele kama vile tautolojia, ukinzani na kinaya. Matumizi ya oksimoroni na paradoksia yanatambulishwa kama vipengele vya ubwege wa kisemantiki. Kejeli za homofoni ni mfano wa utata wa kimaana.

Tamathali za usemi: lugha ya kitamathali ni matumizi ya maneno, vishazi au sentensi kwa namna inayozidi maana yake ya kawaida ili kuwasilisha mawazo changamano, ya kiishara au ya kufikirika. Tamathali hutumika kuimarisha ujumbe, kupamba kazi ya fasihi na kuongeza mvuto wa lugha. Mifano ya tamathali ni pamoja na kejeli, tashbihi, sitiari, jazanda, maswali ya balagha na taswira. Mara nyingi tamathali hutumika katika fasihi, mashairi na mawasiliano ya kila siku kueleza mawazo kwa njia ya kufikirika zaidi na ya wazi (Leech 1969). Tamathali za usemi ni maneno au sentensi ambazo wasanii hutumia kutilia nguvu maana wanayopitisha katika kazi zao. Senkoro (1998) anadokeza kuwa wakati mwingine tamathali za usemi hutumiwa kuipamba kazi ya msanii na kuongeza utamu wa lugha.

2.2.1.4 Matawi Saidizi ya Isimu

Kwa mujibu wa Leech (1969) kiwango hiki kinahusisha matawi matatu saidizi ya isimu ambayo ni; dialektolojia, sajili/ rejista na isimu ya kihistoria.

Dialektolojia: ni uchunguzi wa lahaja na inahusu jinsi lugha inavyotofautiana kulingana na watumiaji. Hii inaweza kuhusisha tofauti katika mifumo ya usemi, matamshi au msamiati kulingana na mambo kama vile eneo, kikundi cha kijamii au asili ya kabila.

Sajili au rejista: huangazia jinsi lugha inavyotofautiana kulingana na matumizi yake katika jamii. Dhana ya rejista hapa inafafanuliwa ili kujumuisha sio tu lugha rasmi au isiyo rasmi bali pia jinsi lugha inavyowasilisha hisia na mitazamo ya mzungumzaji.

Isimu kihistoria: hii ni aina ya isimu ambayo hufuatilia maendeleo ya lugha kiwakati. Inahusisha uchunguzi wa jinsi lugha zinavyobadilika, jinsi maneno mapya au miundo ya kisarufi hujitokeza na jinsi lugha hutofautiana au kugawanyika katika lahaja tofauti. Tawi hili linatoa mwanga katika historia ya lugha, wazungumzaji wake na utamaduni wao Leech (ametajwa).

Kwa mujibu wa Leech (keshatajwa), matawi haya mara nyingi hulingana kwa sababu yanahusisha ulinganisho wa jinsi lugha inavyotumika kwa namna tofauti kulingana na hali kama vile lahaja, mtindo au kipindi cha wakati. Kwa mfano, neno linaweza kuwa na maana au misimbo tofauti kulingana na lahaja (tofauti za kimaeneo), mazingira ya kijamii (rasmi au yasiyo rasmi), au kipindi cha kihistoria (kale au kisasa).

2.3 Hitimisho

Katika sura hii mapitio ya kazi tangulizi ambazo zimetoa picha kamili ya tafiti ambazo tayari zilikwishafanyika kuhusiana na mtindo katika muziki wa Benga kwa jumla yamehakikiwa. Kazi tangulizi ambazo zimepitiwa zinaonyesha kuwa hakuna watafiti wa awali waliowahi kutafiti huhusu mtindo katika muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba kwa kuzingatia mkabala wa umtindo. Pia katika sura hii, nadharia ya umtindo ambayo imetumika katika uchanganuzi wa data za utafiti huu imeelezwa kwa kina kwa kufafanua viwango vyake mahususi.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.0 Utangulizi

Sura hii ilishughulikia mbinu za utafiti zilizotumika katika kukusanya, kuchanganua na kuwasilisha data za utafiti huu. Muundo wa utafiti, eneo la utafiti, walengwa na maadili katika utafiti huu zimejadiliwa. Pia, utaratibu wa ukusanyaji wa data na jinsi data hizo zilivyochanganuliwa umeangaziwa kwa kina.

3.1 Muundo wa Utafiti

Kulingana na Creswell (2009) muundo wa utafiti ni mpangilio au ruwaza ambayo mtafiti hulenga kufuata anapofanya utafiti wake. Utafiti huu ulitumia muundo wa kimaelezo. Kulingana na Kothari (2010) muundo wa utafiti wa kimaelezo huhusisha kuchunguza jambo katika hali yake halisi. Utafiti wa kimaelezo hutambua na kueleza sifa za jambo maalum kama vile mtu, kikundi au jamii. Muundo huu wa utafiti huchunguza hali halisi ya kitu na kueleza miundo ya jamii pamoja na hafla au miktadha ya kijamii. Humwezesha mtafiti kubainisha, kueleza na kutambulisha masuala au tatizo la utafiti kupitia data iliyokusanywa kwa nia ya kuliweka wazi ili lieleweke vizuri (Wanyama na Wandera, 2018). Utafiti wa kimaelezo hutumika zaidi katika tafiti zinazohusu sayansi ya kijamii. Muundo huu wa kimaelezo ulitumika katika utafiti huu kwani ulihusu maelezo ya mtindo ya kiisimu unaotumika katika muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba.

3.2 Eneo la Utafiti

Kulingana na Kothari (2008) eneo la utafiti ni mahali maalum ambapo utafiti utafanyika kutegemea namna mtafiti anavyotarajia kupata data anayohitaji katika utafiti wake. Hili humwezesha mtafiti kupata majibu ya maswali yake ya utafiti. Eneo halisi la ukusanyaji wa data kwa ajili ya utafiti huu lilikuwa mtandao wa kijamii *YouTube*. Utafiti huu ulihusisha muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba uliotungwa kwa kuzingatia vipengele vya mtindo. Kwa kutumia mtandao wa *YouTube* kama eneo la utafiti, utafiti uliweza kupata mifano mbalimbali ya muziki wenye vipengele vya mtindo, hivyo kuwezesha uchambuzi wa kina kulingana na malengo ya utafiti. Eneo hili lilikuwa muhimu hasa katika kueleza athari lengwa ya mikakati ya kimtindo kwani mtafiti aliweza kurejelea baadhi ya maoni ya wasikilizaji walioandika katika mtandao huu baada ya kusikiliza nyimbo za muziki wa Benga.

3.3 Walengwa katika Utafiti

Kwa mujibu wa Robinson (2014), walengwa ni jumla ya vitu, viumbe au watu ambao mtafiti huchagua ili kupata data za utafiti wake. Enon (1998) anafafanua zaidi kwa kusema kwamba, kundi lengwa ni jumla ya watu wote ambao mtafiti amewalenga na ambao anawategemea kupata taarifa anazozihitaji kwa ajili ya utafiti wake. Kwa hivyo, walengwa katika utafiti ni kundi la watu, vitu au vifaa ambavyo sampuli huchukuliwa. Utafiti huu ulilenga muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba uliotungwa kwa kuzingatia vipengele vya kimtindo na ulioimbwa kwa lugha ya Kikamba.

3.4 Mbinu za Usampulishaji

Usampulishaji ni mchakato wa kuteua sehemu ya jamii kuwasilisha jamii nzima ya utafiti. Sampuli huwa ni jumla ya vitu, wanyama, mimea, matukio au watu mbalimbali ambao mtafiti huwateua ili kupata data za utafiti wake au kuwasilisha eneo nzima la utafiti ambalo mtafiti anakusudia kulitafiti (Robinson, 2014). Mtafiti huchagua sampuli ili kuweza kupata data anayokusudia kutoka kwa watafitiwa wachache ambao huwa sehemu ya jamii nzima ya walengwa. Sampuli wakilishi katika utafiti huu iliteuliwa kwa kutumia mbinu ya usampulishaji wa kimakusudi. Mugenda na Mugenda (1999) wameeleza kuwa uteuzi wa sampuli kimakusudi ni mbinu ambayo humwezesha mtafiti kupata data kutoka kwa watafitiwa kwa kutegemea malengo yake ya utafiti. Kwa mujibu wa Kombo na Tromp (2006) usampulishaji wa kimakusudi huchunguza na kuchuja data ili kupata sampuli iliyo na sifa zinazohitajika. Katika usampulishaji wa kimakusudi, uteuzi wa data hufanywa kwa kuegemea maamuzi ya kibinafsi kwa minajili ya uelewa wa kina wa kinachotafitiwa. Kwa hivyo, kutokana na nyimbo zilizosikilizwa, sampuli ilichaguliwa kimakusudi ili kuteua nyimbo za muziki zilizo na vipengele vya mtindo. Mbinu hii ilimwezesha mtafiti kujikita tu kwa muziki wa Benga ulio na vipengele vinavyohitajika kufikia malengo ya utafiti huu.

Mtafiti alichagua nyimbo nane (8) pekee kutokana na sababu za kitaaluma na mada ya utafiti. Kwanza, nyimbo hizi zilikuwa na vipengele vya kimtindo vilivyo wazi, jambo lililorahisisha uchambuzi wa kiusomi na kufanikisha malengo ya utafiti. Pili, uwakilishi wa kijinsia katika utafiti huu ulihakikishwa kwa kuchagua nyimbo sita (6) za waimbaji wa kiume na mbili (2) za waimbaji wa kike, ili kuonyesha mitazamo na mbinu za kimtindo kutoka kwa waimbaji wa jinsia zote. Uwiano huu ulidhihirisha hali halisi ya kihistoria na ya kisasa ambapo muziki wa Benga umetawaliwa zaidi na

waimbaji wa kiume, ingawa waimbaji wachache wa kike wameweza kujitokeza na kupata nafasi katika uwanja huu (*Music in Africa*, 2016). Kwa hivyo, kuingiza nyimbo za waimbaji wa kike kulikuwa muhimu ili kutoa mtazamo wa kijinsia na kuonyesha namna mbinu za kimtindo zinavyoweza kubadilika kulingana na nafasi ya msanii. Mfano mashuhuri ni Princess Jully, ambaye alichukua nafasi ya mumewe na kuibuka kama sauti kuu ya kike katika muziki wa Benga wa jamii ya Wadholuo (Wikipedia, 2023). Uwiano wa 2:6 ulihakikisha uwakilishi wa jinsia zote mbili huku ukidumisha kina cha uchanganuzi na kuzingatia mipaka ya muda na upeo wa utafiti.

Pia, kati ya nyimbo sita zilizoteuliwa tatu zilikuwa za mwimbaji Ken Maria. Mchango wa Ken wa Maria ulizingatiwa kwani alihusiana kwa karibu na maendeleo ya muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba na wanamuziki wengi waliokuwa sehemu ya bendi yake kabla ya kuanzisha bendi zao binafsi walitumia mbinu na mtindo wake (Muema, 2019). Kwa hivyo, kuchagua nyimbo tatu za Ken wa Maria kuliruhusu uchambuzi wa mtindo wa bendi zake na athari zake katika ukuzaji wa muziki wa Benga, jambo lililoifanya sampuli kuwa ya kimsingi na yenye maana ya kiusomi. Zaidi ya hayo, nyimbo zake zina umaarufu mpana nchini Kenya, na hivyo hubeba uzito wa kitamaduni na kijamii (SwahiliPod101, 2014; *Music in Africa*, 2016). Aidha, kazi zake zina utajiri wa kisanaa na kifasihi, jambo lililodhihirika katika tafiti za kitaaluma ambazo zimechambua matumizi ya mbinu za kimtindo kama vile tanakali za sauti na tamathali nyingine za usemi katika nyimbo zake (Mwongela, 2017). Mbili kati ya nyimbo za waimbaji wa kiume zilizotuliwa zililuwa za Ben Mbatha (Kativui) na Alex Kasau (Katombi), ambao waliwahi kuwa wanachama wa bendi ya Ken wa Maria kabla ya kuanzisha bendi zao binafsi (Hivisasa, 2018; Mdundo, 2023). Wimbo mwingine ulihusisha mwimbaji Bosco Mulwa, mmoja wa wanamuziki wa awali wa Benga wa jamii ya Wakamba, aliyefahamika kwa mtindo wa “one-man solo guitar,” ambao uliashiria upekee wa uimbaji na uchezaji wa ala katika kizazi cha awali cha muziki huu (Hivisasa, 2018). Uteuzi huu ulisaidia kuonyesha mabadiliko ya kimtindo yanayotokea baina ya waimbaji tofauti na kuruhusu ulinganisho wa vipengele vya kimtindo vya kizazi cha awali na vile vya kizazi cha sasa. Hali hii inatoa msingi imara wa kuelewa mwendelezo na mageuzi ya mtindo katika muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba

3.5 Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Data ilikusanywa kutoka katika nyimbo zilizorekodiwa na ambazo zilitumia vipengele vya kimtindo. Mtafiti alisikiliza nyimbo za muziki wa Benga kutoka kwa mtandao wa kijamii *YouTube.* Hili ni kwa sababu mtandao wa *YouTube* unatoa nafasi ya wasikilizaji kutoa maoni kuhusu muziki (Burges na Green 2018). Jambo hili lilimsaidia mtafiti kueleza athari lengwa za waimbaji wa muziki wa Benga kwa kuongozwa na maoni yaliyotolewa na wasikilizaji. Baada ya kusikiliza muziki, mtafiti alitumia mbinu ya usampulishaji wa kimakusudi kutambua muziki unaotumia vipengele vya mtindo. Mbinu ya uchanganuzi matini ilitumika kutambua vipengele vya mtindo katika muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba. Data ilikuwa maneno, dhana, kauli, virai na sentensi zinazotumiwa na waimbaji wa muziki huu zilizohusisha vipengele vya kimtindo. Muziki wa Benga ulisikilizwa mara kwa mara kisha kunakiliwa kwenye daftari. Kwa kutumia majedwali, mtafiti alinakili nyimbo za muziki wa Benga zilizoteuliwa. Data ilihamishwa kutoka matini sauti hadi matini andishi huku vipengele vya mtindo vikionyeshwa, kisha vikatafsiriwa kutoka lugha ya Kikamba hadi lugha ya Kiswahili huku maana ikizingatiwa kadri inavyowezekana. Tafsiri ya kisemantiki ilitumika kuhawilisha maana kutoka lugha ya Kikamba hadi ya Kiswahili. Kwa mujibu wa Catford (1965), tafsiri ya kisemantiki ni aina ya tafsiri inayojaribu kuhifadhi maana halisi ya muktadha wa maandishi ya asili kwa ukaribu kadri inavyowezekana, ndani ya mipaka ya lugha lengwa. Data iliyokusanywa iliwekwa katika viwango faafu kulingana na madhumuni ya utafiti huu. Nyimbo za muziki zilizoteuliwa ni: *Wakatimba Kumbavu (**WK**)*- Wakatimba Mpumbavu wake Ken Maria, *Sikala Yakwa (**SY**)* - Sigara Yangu wake Ben Mbatha, *Germany by Foot* **(GF***)*- Ujerumani kwa Miguu wake Ken Maria, *Munene ko Woolilwe?* (**MK) -** Mkubwa kwani Ulisahau? wake Ken Maria, Raha Ndukauna (**RN**) - Raha Haisaidii wake Bosco Mulwa na *Wasa Mbili* (**WM) -** Rafiki Kupe wake Alex Kasau. Nyimbo za Benga za waimbaji wa kike zilizoteuliwa ni: Amaitha **(AM)-** Maadui na Betty Young na Sio Mageni **(SM)** wake Anita Mwiitu wa Kitunguu. Mtafiti alizisimba nyimbo zilizoteuliwa kwa kutumia alama za kwanza za mada za nyimbo hizo ili kufanikisha uelezaji.

3.6 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data

Kulingana na Selinger na Shohamy (1990) uchanganuzi wa data huhusisha kufanya mukhtasari, upekuaji, kuratibu na kusanisi data ili kufikia matokeo na maoni yanayotokana na uzingatiaji wa suala nzima la utafiti.

Uchanganuzi wa maelezo ulitumika kuchanganua data za utafiti huu. Kwa mujibu wa Enon (1998), mkabala wa uchanganuzi wa maelezo ni mkabala usio wa idadi. Ni mbinu ya kuchanganua data ambayo mtafiti hueleza na kufafanua data zake kwa kutumia uelezaji. Uchambuzi huu hutegemea zaidi uchanganuzi wa mtafiti pamoja na ustadi wa ujumuishaji na ufahamu wa kibinafsi wa muktadha wa kijamii ambamo data hukusanywa. Mkazo katika utafiti wa aina huu unatiliwa katika kuelewa jambo badala ya kulitabiri au kulieleza. Mbinu ya ubunifu na uchunguzi inahitajika katika uchambuzi wa kimaelezo.

Hivyo, data ya utafiti huu ilichanganuliwa kimaelezo kwa kurejelea mihimili ya nadharia ya umtindo na kwa kuzingatia malengo ya utafiti huu. Matokeo ya uchanganuzi wa data za utafiti huu yaliwasilishwa kwa kuzingatia viwango vya nadharia ya umtindo kama vilivyoelezwa na (Leech, 1969).

3.7 Maadili Yaliyozingatiwa

Maadili ni dhana pana inayotumika katika mazingira fulani ambapo jamii imejiwekea kwa lengo la kulinda heshima ya amali zake. Maadili ni kama onyo au katazo kuhusu jambo fulani (TUKI, 2004). Kwa maana hiyo, maadili ya utafiti ni onyo linalotolewa kwa mtafiti asifanye mambo kinyume na mchakato au matarajio ya utafiti husika. Maadili katika utafiti huu yalizingatiwa kabla na baada ya kukusanya data. Mtafiti alihakikisha kuwa maarifa yaliyopatikana katika data ilizokusanywa yalitumika tu kwa lengo la kufikia madhumuni ya utafiti huu pekee. Isitoshe, mapendekezo ya tafiti za baadaye yalitolewa bila kudunisha juhudi zilizofanywa hapo awali kuhusiana na suala la utafiti. Mtafiti alipata idhini ya kukusanya data kutoka kwa Bodi ya Masomo ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Embu (BPS). Vilevile mtafiti alituma ombi na kupata kibali cha kukusanya data kutoka kwa Tume ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Uvumbuzi (NACOSTI).

3.8 Hitimisho

Sura hii imeeleza mbinu za utafiti zilizotumika katika kazi hii. Imeanza kwa kufafanua muundo wa utafiti ulioongoza mchakato mzima wa ukusanyaji na uchambuzi wa data,

kisha ikaeleza eneo la utafiti na sababu za kuteua eneo hilo kama sehemu mwafaka ya kupata data iliyohitajika. Aidha, sura hii imebainisha walengwa katika utafiti huu na vigezo vilivyotumika kuwachagua. Pia, imetoa maelezo ya mbinu za usampulishaji zilizowezesha kupata sampuli inayowakilisha kikamilifu jamii iliyolengwa. Mbinu za ukusanyaji data kama vile uchanganuzi matini zimefafanuliwa. Vilevile, imeelezwa jinsi data ilivyochanganuliwa na kuwasilishwa ili kutoa matokeo yanayoendana na malengo ya utafiti. Hatimaye, sura hii imejadili masuala ya maadili yaliyotiliwa maanani katika ukusanyaji na uchanganuzi wa data.

SURA YA NNE

MATOKEO YA UTAFITI

4.0 Utangulizi

Sura hii inajumuisha mjadala wa uchanganuzi wa data za utafiti huu. Uchanganuzi wa data uliongozwa na malengo ya utafiti kama yafuatayo: Kubainisha mikakati ya kimtindo wanayotumia waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba kuwasilisha ujumbe, kuchanganua jinsi waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba wanavyotumia mikakati ya kimtindo kuimarisha ujumi kwenye muziki wao na kueleza athari lengwa ya mikakati ya kimtindo wanayotumia waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba. Kwa hivyo, mjadala wa sura hii ulilenga kuonyesha namna mbinu mbalimbali za kimtindo kama vile tamathali za usemi, urudiaji, taswira na mikakati mingine ya lugha zinavyotumiwa na waimbaji ili kufikisha ujumbe wao kwa hadhira. Vilevile, inabainisha jinsi mikakati hiyo inavyochangia katika kutoa maana pana zaidi ya kijamii, kitamaduni na kihisia na hatimaye kueleza athari zinazokusudiwa kwa hadhira lengwa. Kwa njia hii, sura hii inamwezesha msomaji kufahamu mchango wa uchanganuzi wa kimtindo katika kueleza upekee na umuhimu wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba.

4.1 Mchakato wa Uchanganuzi

Lengo kuu katika sura hii lilikuwa kuchunguza jinsi waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba wanavyotumia vipengele vya mtindo ili kupitisha jumbe zao kwa hadhira lengwa. Mchakato wa ukusanyaji na uchanganuzi wa data ulihusisha: Kusikiliza nyimbo za muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba katika mtandao wa kijamii *YouTube*, kuzinakili nyimbo hizo katika majedwali, kubainisha vipengele vya mtindo katika muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba kwa kuzingatia nadharia ya umtindo, kutafsiri vipengele hivyo kutoka lugha ya Kikamba hadi lugha ya Kiswahili, kisha kueleza ujumi na athari za matumizi ya vipengele vya mtindo katika muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba.

Jumla ya nyimbo nane za muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba zilichunguzwa. Data za utafiti zilichanganuliwa na kuwasilishwa kimaelezo kwa kuzingatia mihimili ya nadharia ya umtindo kama ilivyofafanuliwa na (Leech,1969). Mtafiti alianza kwa kubainisha vipengele vya umtindo katika lengo la kwanza ambavyo vilijenga msingi wa uchanganuzi wa lengo la pili na lengo la tatu.

4.2 Mikakati ya Mtindo

Matokeo ya utafiti yalibainisha kuwa wanamuziki wa Benga wa jamii ya Wakamba hubuni muziki wao kwa kutumia mikakati ya kimtindo ili kuweka wazi ujumbe wao kwa hadhira lengwa. Hii ina maana kwamba vipengele vya mtindo huwa sehemu ya mawasiliano ya wanamuziki hawa. Sehemu hii ililenga kuchunguza vipengele vya kiisimu vinavyozingatiwa na waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba. Vipengele vya kiisimu huathiri uelewekaji wa ujumbe kwani humwelekeza msikilizaji kwenye maana inayokusudiwa au kuashiriwa na mwimbaji. Mtindo husababishwa na jitihada za kuleta uhusiano wa kimaana (Speber na Wilson 1995). Ifuatayo ni mikakati mbalimbali ya kimtindo inayotumiwa na waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba kulingana na viwango vya nadharia ya umtindo.

4.2.1 Kiwango cha Grafolojia

Vipengele vinavyoshughulikiwa chini ya grafolojia ni pamoja na alama za uakifishaji, italiki, ugawaji wa aya au beti, alama za kiothografia, viwango vya nafasi katika maneno na sentensi. Baadhi ya vipengele vya kigrafolojia vilivvyobainika katika muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba ni kama vifuatavyo:

4.2.1.1 Ugawaji wa Beti

Kipengele hiki kilihusisha kutazama jinsi waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba wanapangilia maneno katika beti tofauti ili kupitisha athari maalum kwa hadhira lengwa. Kwa mujibu wa Leech (1969), ugawaji wa beti hutumika kuunda na kupanga ujumbe kwa njia inayoweza kueleweka. Nafasi katika beti au aya zinaweza kuonekana kama njia ya kupanga na kuunda habari, hasa katika muktadha wa masimulizi na maelezo. Leech anaeleza kuwa kulingana na namna kazi ya sanaa inavyogawanywa (kama vile katika aya fupi au ndefu) inaweza kuathiri jinsi msikilizaji anavyoyaelewa maudhui. Kwa mfano, muziki **GF KIMB IV UK 129**; tazama beti zifutazo:

> *Niuka na maau, Germany Ruth sweetie* - Nitakuja kwa miguu, Ujerumani Ruth ‘sweetie.’
>
> *No mbaka ngwone, ngoo yakwa itulie* - Ni lazima nikuone, ili roho yangu itulie **UB 1 UK 129**

Ndisya kumiisya, mbaka wiuika we mbevi - Siwezi kuvumilia, hadi utakapokuja mpenzi.

Kita umbeteela Germany, niuka na mau - Nisubiri Ujerumani, nitakuja kwa miguu. **UB 6 UK 130**

Katika beti hizi mwimbaji ametumia vifungu vifupi vyenye mishororo miwili ili kutoa hisia za dharura zinazomsukuma kwenda kumwona mpenziwe aliye Ujerumani. Kulingana na Leech (ametajwa), mpangilio wa aya au beti huweza kuathiri mtiririko na ufasiri wa maana. Mapumziko katika beti yanaweza kutumika kimkakati kusisitiza mabadiliko katika mandhari, wakati, eneo au hali. Kwa mfano katika wimbo huu wa **GF KIMB IV UK 129;** mwimbaji anatumia aya fupi katika muziki mzima kisha anarefusha ubeti ufuatao:

Nio ngethe yakwa yi Germany, Ruth Mwende ke Germany, yu nikusitye Germany, syindu syakwa syi Germany, Nikusya nginya Germany, Niendete by foot nyie, Wanzanze mbike Germany - Nina mpenzi wangu aliye huko Ujerumani, Ruth Mwende yuko Ujerumani, sasa ninaenda Ujerumani, mali yangu iko Ujerumani, nitaenda hadi Ujerumani, ninaenda kwa miguu mimi, Wanzanze nifike Ujerumani **UB 7 UK 130**

Kwa kuwa huu ndio ubeti wa mwisho katika muziki huu mwimbaji anatumia aya ndefu kusababisha mabadiliko ya hisia na kusisitiza ujumbe. Matumizi ya ghafla ya aya ndefu yanampa msikilizaji nafasi ya kutafakari zaidi ujumbe unaopitishwa. Vilevile Leech (keshatajwa) anasisitiza kuwa ugawaji wa aya au beti hutumika kusababisha athari za kimdundo na wizani. Kwa mfano katika muziki **SY KIMB I UK 125** beti zifuatazo;

Ningwiwa muyo Kameneja, musasuko mwingi na raha - Ninafurahi mimi Kameneja, utamu mwingi na raha

Ngasyoka ngavewa mulamu, ila ni stimu swakwa nyie - Narudi kuhisi mvuto, wakati niko na stimu zangu mimi

Nikyongete na ngavya ngwai, Nithuanite na andu me mikwa - Nikitafuna miraa na kuvuta bangi, sina hamu ya watu wenye kisirani **UB 1 UK 125**

Kitumi ndyendete kelele, nivulanitye Matenzawa - Kwa maana sipendi kelele, nikiwa nimelewa Matenzawa

Stimu sya vangi kindingi, na milaa isilaa kimwe - Stimu za bangi, pombe na miraa zinafanana

I*yisene na miambile, syendete vandu vatulisu* - Hazijui kupiga mdomo, hupenda mahali tulivu **UB 2 UK 125**

Katika muziki huu ubeti wa pili unasisitiza mtiririko wa mawazo katika ubeti wa kwanza. Mwimbaji katika ubeti wa pili anaendelea kusifia hisia zake zinazotokana na matumizi ya mihadarati anayotaja katika ubeti wa kwanza. Beti hizi zinajenga wizani na mdundo wa muziki huu. Kwa mujibu wa Naseem na Talat (2021), ukiushi wa kigrafolojia wa kimakusudi hasa katika ugawaji wa beti hutumika kusisitiza maudhui na kuweka wazi masuala muhimu. Kama wanavyoeleza Crystal na Davy (2016) mbinu hii ya kigrafolojia ni muhimu katika kuimarisha maudhui na mada ya usimulizi kwani huleta tofauti baina ya sauti za lugha ya kawaida na lugha ya msisitizo katika tungo.

4.2.1.2 Uakifishaji na Ugawaji wa Mishororo

Kwa mujibu wa Leech (1969) uakifishaji na ugawaji wa mishororo ni sifa muhimu za kigrafolojia kwani huathiri muundo na mdundo wa kazi ya sanaa. Pia unaongoza ufasiri wa msikilizaji, mtiririko wa hisia na usimulizi wa kazi ya sanaa. Uakifishaji katika nyimbo huwa na jukumu la kujenga msisitizo, kuongeza wizani na kujenga hisia. Kulingana na Leech (keshatajwa), uakifishaji huathiri fasiri ya msikilizaji kwa kudhibiti mtiririko wa matini na kuashiria hali za hisia.

Katika muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba, mkakati wa uakifishaji umetumika ifuatavyo;

Muziki **MK KIMB II UK 127** tazama ubeti ufuatao;

Munene wambiiye tukambeini, nikenda kivila kyuke kwitu, Mkubwa uliniambia tupige kampeni, ndiposa kiti kije kwetu

Munene wambiiye we ukanzuvia, oila kivila kiuka kwitu - Mkubwa uliniambia wewe utanitunza, pindi tu kiti kitakapokuja kwetu

Kivila niwoosie, na nyie ndwanzuvia - Kiti ulichukua, na mimi haunitunzi,

Kivila ni twosie, na we mwa niwaie - Kiti tulichukua, na wewe ukapotea

Ninguseng'a na ngikulya ii, munene we kowolilwe?- Ninashangaa na kuuliza mkubwa kwani ulisahau **UB 1 UK 127**

Katika ubeti huu vipumuo vimetumika kutenganisha dhana na kuunda mtiririko wa kidrama wa muziki huu. Kwa mfano katika sentensi "*Kivila niwoosie, na nyie ndwanzuvia*- Kiti ulichukua, na mimi haunitunzi,*"* MSH 3. Matumizi ya kipumuo kabla ya kiunganishi "*na"* yanaonyesha hali ya kusitisha kwa muda mdogo. Hali hii inaruhusu msikilizaji kuhisi uzito wa hisia katika kifungu hiki kabla ya kuendelea na sehemu nyingine ya mshororo. Isitoshe mwimbaji huyu anatumia alama ya kiulizio mwishoni mwa ubeti huu anapouliza "*Ninguseng'a na ngikulya ii munene we kowolilwe?* -Ninashangaa na kuuliza mkubwa kwani ulisahau?" MSH 5. Swali hili linasisitiza ujumbe na kuongeza wizani katika muziki huu.

Vilevile katika muziki **GF KIMB IV UK 129** ubeti ufuatao;

Nio ngethe yakwa yi Germany, Ruth Mwende ke Germany, yu nikusitye Germany, syindu syakwa syi Germany, Nikusya ginya Germany, niendete by foot nyie, Wanzanze mbike Germany - Nina mpenzi wangu aliye huko Ujerumani, Ruth Mwende yuko Ujerumani, sasa ninaenda Ujerumani, mali yangu iko Ujerumani, nitaenda hadi Ujerumani, ninaenda kwa miguu mimi, Wanzanze nifike Ujerumani **UB 7 UK 130**

Neno "Germany" lililorudiwa katika sehemu za ubeti huu linaambatana na vipumuo katika muundo wa mishororo ya wimbo huu. Urudiaji huu pamoja na vipumuo katika muundo wa muziki huu, unasaidia kuleta taswira na kujenga hisia za kufadhaika zinazowasilishwa na mwimbaji kutokana na hali yake. Matumizi ya neno ”Germany,” linalofuatwa na kipumuo, yanachangia mtiririko wa kidrama wa muziki huu na kusababisha wizani kwa lengo la kuvutia hadhira lengwa. Katika ushairi na nyimbo, kuzingatia au kutozingatia kanuni za uakifishaji za lugha sanifu kunaweza kutumika kutanguliza maana na toni za kihisia. Haya yanaungwa mkono na utafiti uliofanywa na Maledo (2020) ambao ulichunguza jinsi uakifishaji, pamoja na vipengele vingine vya kisarufi kama vile ugawaji wa mishororo na mpangilio wa tungo, huchangia katika athari ya kimawasiliano ya ushairi. Ilibainika kwamba washairi hutumia uakifishaji kimkakati kudhibiti nafasi na mdundo, hivyo kuboresha kina cha maudhui na uzito wa kihisia wa kazi zao.

4.2.2 Kiwango cha Fonolojia

Kiwango hiki hujihusisha na uchunguzi wa mtaala wa sauti za lugha fulani pamoja na kanuni zinazotawala utamkaji wa sauti za lugha hiyo. Vipengele vya kifonolojia hutumika kusababisha athari za kiujumi na za kimawasilano (Leech, 1969). Kwa mujibu wa Verdonk (2002), mikakati ya kifonolojia kama vile urudiaji wa sauti au dhana huchangia kuvutia umakini kwa mada au mishororo mahususi na hivyo kuongeza msisitizo na kutilia mkazo usemi. Vipengele vya kifonolojia hufanya nyimbo kuwa rahisi kukumbukwa na kuweza kuenezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine (Finnegan, 1970). Mikakati ya kimtindo inayojitokeza katika muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba ni kama ifuatayo:

4.2.2.1 Urudiaji

Urudiaji ni kitendo cha kufanya au kusema kitu zaidi ya mara moja (Muathe, 2012). Urudiaji huweza kujitokeza katika viwango vya neno, maneno, kauli au sentensi. Silabi, maneno au sentensi zinaweza kurudiwa ili kusisitiza ujumbe na kuupa wimbo muundo.Leech (1969) anadokeza kuwa urudiaji ni aina ya mtindo inayoweza kutumika kuleta uziada.

Urudiaji wa maneno unajitokeza katika muziki **GF KIMB IV UK 129** ambapo neno, *Germany* (Ujerumani) limerudiwa katika kila mshororo wa ubeti huo.

> *Nio ngethe yakwa yi* ***Germany****, Ruth Mwende ke* ***Germany****, yu nikusitye* ***Germany****, syindu syakwa syi* ***Germany****, nikusya nginya* ***Germany****, Niendete by foot nyie, Wanzanze mbike* ***Germany*** - Nina mpenzi wangu aliye huko **Ujerumani**, Ruth Mwende yuko **Ujerumani**, sasa ninaenda **Ujerumani**, mali yangu iko **Ujerumani**, nitaenda hadi **Ujerumani**, Ninaenda kwa miguu mimi, Wanzanze nifike **Ujerumani UB 7 UK 130**

Neno hili limerudiwarudiwa ili kusisitiza dhamira ya mwimbaji ambapo analenga kuonyesha mapenzi yake kwa msichana anayemwimbia kwa kupanga safari ya ng'ambo ili aweze kumtembelea. Urudiaji wa neno hili unaleta msisitizo wa hisia za dharura inayohitajika na mwimbaji kumtembelea mpenzi wake. Urudiaji wa aina hii ulibainika katika nyimbo za injili za jamii ya Wakamba kama anavyoeleza (Muathe, 2012). Muathe aligundua kuwa waimbaji wa nyimbo za injili za jamii ya Wakamba kama vile Stella Mengele na Wilberforce Musyoka, wamerudia maneno na sentensi tofauti tofauti ili kusisitiza umuhimu wa dini katika jamii.

Kama wanavyodokeza Crystal na Davy (1969), vipengele vya kifonolojia kama urudiaji huathiri toni na hisia katika wimbo ambapo, baadhi ya maneno huweza kuonyesha utulivu huku mengine yakileta hisia za woga na dharura katika usemi.

Katika Muziki **WM KIMB III UK 128** maneno "*Ninakola* - Sitaki" na "*Wasa* - Rafiki" yamerudiwa. Kwa mfano katika sentensi hizi;

> *We* ***wasa*** *kitindo kyaku ninakola* **-** Wewe **rafiki** yangu urafiki wako sitaki
>
> *Ninakola we* ***wasa*** *tutaane vathei* - Sitaki wewe **rafiki** usinidai chochote **UB 1 MSH 1, 4 UK 128**

Urudiaji wa maneno haya unalenga kutoa msisitizo wa hisia za masikitiko ya mwimbaji kutokubaliana na rafiki yake na kutaka kuuvunja urafiki wao. Urudiaji huu unaonyesha ukali wa maamuzi ya mwimbaji na kuimarisha hisia za kukata tamaa na kutaka kujitenganisha na urafiki wa sampuli hiyo. Neno "*wasa* (rafiki)" limerudiwa kuonyesha hasira za mwimbaji na kuchoshwa na uhusiano wa rafiki yake.

Vilevile katika muziki huu **WM KIMB III UK 128**, kuna urudiaji wa kimuktadha ambao unajitokeza kwani wazo kuu la wimbo huu ni kukataa urafiki usio na faida. Kwa mfano, kuna urudiaji wa matendo ya kuchukiza yanayotendwa na rafiki ya mwimbaji huyu. Haya yanabainika katika sentensi zifuatazo:

> *Unguniaa simu kila wikendi yavika* - Huwa unanipigia simu kila wikendi ikifika
>
> ***Uimbia numaale wina mauseo mazuri* - Unaniambia nitoke eti uko na mazuri**
>
> *Mitoto mwa ya university ngethe mbyu* - Wasichana wa chuo kikuu vipusa warembo
>
> ***Na navika ndikwithia na maveti makuu* - Ila nikifika nakupata na kina mama wakongwe**
>
> *Nisuvia iveti syaku ndeiwa ngalama* - Huwa nawafadhili wanawake wako bila kuhisi gharama
>
> *Leu mbuki mbaka too no mbilu yakwa* - Chakula, pombe hadi malazi ni gharama yangu **UB 2, 3 UK 128,139**

Urudiaji wa matendo kama *"*huwa unaniambia nitoke eti uko na mazuri, kisha nikifika nakupata na akina mama wakongwe*",* unasisitiza ulaghai na udaganyifu katika urafiki baina ya mwimbaji na rafiki yake. Matendo haya yanarudiwa ili kueleza hali ya kutokuwa na uaminifu katika urafiki huu. Pia katika muziki huu **WM KIMB III UK 128,** mwimbaji anatumia sentensi kama:

> *Twataanisya uilika tulavu Mukuru, uyaambiaya uzambasya uivoya kimee* - Tukiachana unaingia vilabu vya Mukuru, unaanza kunidhalilisha ukiomba pombe. **UB 4 MSH I UK 129**

Huu ni mfano mwingine wa urudiaji wa kitendo cha kukasirisha kwani mwimbaji anasema rafiki yake anamdhalilisha katika vilabu vya Mukuru kwamba anahusiana na akina mama wakongwe. Kitendo hiki kinasisitiza uchungu alionao mwimbaji kutokana na kutumiwa vibaya na rafiki yake.

Urudiaji ni kipengele muhimu kinachotumika kuleta maana na kuongeza nguvu za kihisia katika tungo (Leech, 1969). Urudiaji umetumika katika muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba kuonyesha msukumo wa kihisia wa waimbaji, kuongeza maana ya kimuktadha na kuimarisha uwasilishaji wa ujumbe pamoja na kuleta ujumi.

4.2.2.2 Uradidi

Leech (1969) anafafanua uradidi kama kipengele cha mtindo kinachohusisha urudiaji wa sauti za konsonanti katika maneno au silabi zinazokaribiana. Uradidi unapatikana katika muziki wa benga **SY KIMB 1 UK 125** kama ifuatavyo;

> *Kitumi ndye**ndet**e kele**le**, nivulanitye Matenzawa*- Kwa maana sipendi kelele, nikiwa mlevi Matenzawa
>
> *Stimu sya vangi ki**nd**ingi, na mi**l**aa isi**l**aa kimwe*- Stimu za bangi pombe na miraa zinafanana
>
> *Iyisene na miambi**le**, sye**nd**ete vandu vatulisu* -Hazijui kupiga mdomo, hupenda mahali tulivu **UB 2, MSH 1,2 &3 UK 125**

Katika ubeti huu sauti za konsonanti/l/, /t/ na /nd/ zimerudiwa. Urudiaji wa aina hii unaongeza mdundo wa muziki huu na kuufanya uwe wa kuvutia zaidi. Vilevile katika wimbo huu **(SY),** uradidi unajitokeza katika ubeti ufuatao;

> ***Ni** kwithiwa **ni** Mu**ra**sta, na **ni**ishia kim**ra**sta* - Kwa maana mimi ni mrasta, na huwa naishi kama mrasta
>
> ***Ni**kyongaa ta mura**st**a, ngakusya vangi ta mu**ra**sta* - Huwa natafuna miraa kama mrasta, na kuvuta bangi kama murasta
>
> *Sikala yakwa **ni** **ro**sta, inyusawa **ni** mu**ra**sta* - Sigara yangu ni rosta, huwa inavutwa na m**ra**sta **KIMB I UB 7 UK 126**

Katika ubeti huu kuna uradidi wa sauti katika silabi (ni) na (sta), sauti hizi zimerudiwa kwa lengo la kusisitiza ujumbe wa mwimbaji. Mwimbaji anasifia uraibu wake wa kuvuta sigara aina ya 'rosta'. Uradidi wa aina hii unamsaidia mwimbaji kujenga

mtindo wa kipekee wa uimbaji wake na kuufanya muziki uwe wa kuvutia na rahisi kukumbukwa.

Pia, katika muziki **MK KIMB II UK 127**, uradidi unajitokeza ifuatavyo:

> ***M****unene wa****m****biiye tu****k****a****m****beni* - Mkubwa uliniambia tupige kampeni
>
> *Ni****k****enda ki****v****ila* ***k****yuke* ***k****witu* - Ndiposa kiti kije kwetu
>
> ***M****unene wa****m****biiye we u****k****anzuvia* - Mkubwa uliniambia wewe utanitunza
>
> *Oila* ***k****i****v****ila* ***k****iu****k****a* ***k****witu* - Pindi tu kiti kitakapokuja kwetu **UB 1 UK 127**

Katika ubeti huu, kuna uradidi wa sauti za konsonanti /k/, /v/ na /m/. Uradidi wa aina hii unakuza mdundo na mtindo wa kisanaa huku ukiongeza umakini na kutilia mkazo ujumbe unaopitishwa katika wimbo huu. Uradidi huu unasisitiza umuhimu wa "kiti" kama kifaa cha madaraka au nafasi ya utawala. Mwimbaji ameutumia kusisitiza haja ya viongozi kuzingatia umakinifu wanapochukua madaraka ili kuwasaidia wananchi waliowachagua. Wasanii hutumia mkakati wa uradidi ili kuongeza uzito na ufanisi wa hisia kwa hadhira lengwa (Leech, 1969).

4.2.2.3 Urari wa Sauti

Kwa mujibu wa nadharia ya umtindo, urari ni sifa ya kimtindo inayohusisha matumizi ya sauti zinazofanana hasa mwishoni mwa maneno au mishororo katika ushairi au wimbo. Urari huchangia katika kuongeza mdundo wa muziki na kuimarisha ujumi. Leech (1969) anauona urari kama kipengele muhimu cha mpangilio wa sauti katika ushairi au aina nyingine za kifasihi. Urudiaji wa sauti za konsonanti au vokali huweza kusababisha athari za kihisia au kimawazo za kazi za sanaa (Verdonk, 2002). Katika muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba urari unajitokeza ifuatavyo;

Katika muziki **MK KIMB II UK 127** ubeti ufuatao una vipengele vya urari;

> *Munene wambiiye tukambeini* - Mkubwa uliniambia tupige kampeni
>
> *Nikenda kivila kyuke kwi****tu*** - Ndiposa kiti kije kwetu

*Munene wambiiye we ukanzuvi**a*** - Mkubwa uliniambia wewe utanitunza

*Oila kivila kiuka kwi**tu*** - Pindi tu kiti kitakapokuja kwetu

*Kivila niwoosie na nyie ndwanzuv**ia*** - Kiti ulichukua na mimi haunitunzi

Kivila ni twosie na we mwa niwaie - Kiti tulichukua na wewe ukapotea

Ninguseng'a na ngikulya ii munene we kowolilwe - Ninashangaa na kuuliza mkubwa kwani ulisahau? **UB 1 UK 127**

Katika ubeti huu vina vya mwisho katika mshororo wa pili na wa nne vinafanana ambapo vinaishia kwa silabi (tu). Vilevile vina vya mwisho katika mshororo wa tatu na wa tano vinaishia kwa sauti ya vokali /a/. Urari unaojitokeza katika mishororo hii umetumika kuongeza mdundo wa mziki huu kwa lengo la kuufanya uwe wa kupendeza na kuvutia wasikilizaji. Urari hutumika katika muziki kuimarisha ujumi, kusisitiza toni ya wimbo na kuwezesha kukumbukwa kwa mishororo ya wimbo kwa urahisi.

Pia urari unajitokeza katika wimbo **SY KIMB I UK 125** ubeti ufuatao:

*Ni kwithiwa ni Mura**sta**, na niishia kimra**sta*** - Kwa maana mimi ni mrasta, na huwa naishi kama mrasta,

*Nikyongaa ta mura**sta**, ngakusya vangi ta mu**ra**sta* - Huwa natafuna miraa kama mrasta, na kuvuta bangi kama mrasta**,**

*Sikala yakwa ni **ro**sta, inyusawa ni mu**ra**sta* - Sigara yangu ni rosta, huwa inavutwa na mr**a**sta **UB 7 UK 126**

Katika ubeti huu vina vya kati na vya mwisho vinafanana kwa kuishia kwa silabi /sta/. Katika muziki huu mwimbaji anasisitiza maudhui ya utumiaji wa mihadarati kwa kutumia sauti zinazotokana na aina ya sigara anayoirejelea kama "rosta." Urari wa aina hii umetumika ili kuongeza wizani katika wimbo huu na kuvutia hadhira lengwa.

Vile vile katika muziki **AM KIMB VII UK 135** tazama ubeti ufuatao;

> *Niilye nyumba kwaka utu**ku**, muomo wakunangwa ni Mutu**ku**-* Nikiwa nimekaa kwangu usiku, mlango ukabishwa na Mutuku.
> *Chairlady uvoo wa matu**ku**, okite uchunguza akatavye Ndu**ku**-* "Chairlady habari za masiku", akiwa amekuja kuchunguza akamwambie Nduku. **UB 4 UK 135**

Katika ubeti huu, urari wa sauti unaonekana pale ambapo maneno mwishoni mwa mistari yanaishia kwa sauti zinazofanana (ku), hivyo kuongeza mvuto wa kishairi na muziki. Urari unaojitokeza katika muziki huu **(AM)** unadhihirisha urari wa mwisho wa mshororo unatumika ili kusaidia hadhira kuzingatia ubeti kwa urahisi. Urari wa aina hii unachangia kuongeza mvuto wa kishairi na kukuza uhusiano wa kihisia kati ya msanii na hadhira.

Kwa mujibu wa Leech (1969) urari hutumika kusababisha athari ya kudumu katika ubongo wa msikilizaji na kusababisha wimbo kukumbukwa kwa urahisi. Hujenga maumbo yanayosisitiza dhana, maudhui na maneno maalum pamoja na kudumisha hisia katika kazi za fasihi. Maoni haya yanaungwa mkono na Chilala (2018) anaposema kuwa urari katika mashairi au nyimbo husaidia kuzifanya kukumbukwa kwa urahisi na kuwapa waisikilizaji fursa ya kuimba pamoja na mtunzi. Kukumbukwa huku kunachangia umaarufu wa wimbo na ushiriki wa wasikilizaji.

4.2.2.4 Takriri

Kwa mujibu wa Leech (1969) takriri huhusisha ukariri wa maneno, dhana au mistari ndani ya matini kwa lengo la kusisitiza, kuimarisha maana au ujumi katika kazi ya sanaa. Takriri imejitokeza katika muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba kama ifuatavyo:

Katika muziki **WM KIMB III UK 128** katika beti hizi;

> *We **wasa** ii kitindo kyaku **ninakola*** - Wewe rafiki yangu urafiki wako sitaki
>
> *Kitumi nyie ndikwenda utindana na mbili* - Kwa sababu mimi sitaki kuishi na kupe

> *Unyonyae tupesa twakwa uteiwa nthoni* - Unatumia pesa zangu bila kuona aibu
>
> ***Ninakola*** *we* ***wasa*** *tutaane vathei* - Sitaki huo urafiki usinidai chochote **UB 1 UK 128**
>
> *Ninakola uwasa uu wina ngalama* - Sitaki tena urafiki huu una gharama. **UB 3 MSH 4 UK 129**
>
> *Kitindo kiu* ***ninakola*** *we* ***wasa*** *manya ou* - Urafiki huo sitaki tena, wewe rafiki fahamu hivyo **UB 5 MSH I UK 129**
>
> ***Uwasa*** *uu wa unyoonyaa ndienda Kisinga* - Urafiki huo wa kuninyonya sitaki Kisinga. **UB 5 MSH 4 UK 129**

Katika beti hizi kuna ukariri wa maneno "wasa - rafiki na *ninakola* - sitaki." Maneno haya yamekaririwa ili kuleta hisia za kukanusha na kudhihirisha hasira za mwimbaji dhidi ya urafiki usiokuwa na manufaa. Yametumika kuonyesha kutokuwa na furaha na kutokubaliana na urafiki huo.

Pia, mkakati wa takriri umetumika katika muziki **GF KIMB IV UK 129** ubeti ufuatao:

> *Nio ngethe yakwa yi* ***Germany****, Ruth Mwende ke* ***Germany****, yu nikusitye* ***Germany****, syindu syakwa syi* ***Germany****, Nikusya Nginya* ***Germany****, Niendete by Foot nyie, Wanzanze mbike* ***Germany*** - Niko na mpenzi wangu aliye huko Ujerumani, Ruth Mwende yuko Ujerumani, sasa naenda Ujerumani, mali yangu iko Ujerumani, nitaenda hadi Ujerumani, Ninaenda kwa miguu mimi, Wanzanze nifike Ujerumani **UB 7 UK 130**

Neno '*Germany'* (Ujerumani) linakaririwa katika mishororo ya ubeti mzima. Mwimbaji analikariri ili kusisitiza mapenzi aliyonayo kwa mpenziwe aliye nchi ya ng'ambo. Takriri huchangia upatanisho wa kileksia ndani ya maneno katika nyimbo na kuimarisha maudhui. Uchunguzi kuhusu aina mbalimbali za muziki, ikiwa ni pamoja na *hiplife*, unaonyesha kuwa vipengele vinavyorudiwa husaidia kuimarisha

lengo la mada ya wimbo na kuimarisha uwiano wake kwa jumla (Nkansah, 2021). Kupitia utumiaji wa takriri, wanamuziki huongeza kina cha hisia, uwezo wa kukumbukwa na sauti za kitamaduni katika nyimbo zao. Mbinu hii ya kimtindo inaboresha sio tu uzoefu wa usikilizaji lakini pia inachangia mafanikio ya kupitisha ujumbe muhimu kwa hadhira lengwa.

4.2.3 Kiwango cha Umbo

Kiwango cha mofolojia kinahusu jinsi maneno au leksimu zinavyoundwa. Leksimu huhusisha uteuzi wa msamiati katika kazi za fasihi. Kiwango hiki cha kimtindo kinajihusisha na maneno, istilahi na dhana za lugha fulani. Maumbo ya maneno pamoja na uteuzi wa msamiati katika muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba umebainishwa katika kiwango hiki.

Kulingana na Ooko (2008), wawasilianaji kimakusudi hufanya uchaguzi wa kileksia ili kuwasilisha kwa ufanisi ujumbe wanaokusudia kupitisha. Maana anayonuia mnenaji huwa imebanwa katika vipengele vya kileksia vinavyounda usemi maalum. Muktadha, mada na jamii husika huathiri uchaguzi wa maneno anayoyatumia msanii. Uchaguzi wa msamiati una uhusiano wa karibu na mada au muktadha wa mawasiliano na ni muhimu katika uwasilishaji wa maudhui, kwani huweza kumwelekeza msikilizaji kuelewa vyema ujumbe (Omolo, 2014). Kwa hivyo kulingana na watalaamu hawa uchaguzi wa maneno unaofanywa na waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba si wa kiutunzi tu, bali ni wa kimakusudi. Hii ni kwa sababu wasanii wanalenga kuwasiliana na hadhira yao. Maneno yanayochaguliwa katika muziki huu wa Benga yanadokeza maudhui yaliyoshughulikiwa pamoja na kuonyesha mtindo unaotumika kupitisha maudhui hayo.

4.2.3.1 Uhamishaji Msimbo

Mitray na Musken (1995) wanafasiri kuhamisha msimbo kama njia mbadala inayotumiwa na watu wenye umilisi wa lugha mbili katika mazungumzo. Mikakati ya kuhamisha msimbo hutokea pale ambapo maneno ya lugha nyingine huingizwa na kutumika katika kazi ya fasihi inayotumia lugha tofauti. Kwa mujibu wa Leech (1969) uchaguzi wa lugha wanaofanya wasanii hauhusishi tu ujumbe bali unahusu muktadha ambamo mazungumzo hufanyika.

Hali hii imejitokeza katika nyimbo za muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba ambapo waimbaji wametumia maneno ya Kiswahili na Kiingereza katika muziki wa

lugha ya Kikamba. Kwa mfano katika muziki **SY KIMB I UK 125** tazama sentensi zifuatazo:

> *Ningwiwa muyo kameneja, musasuko mwingi na* ***raha*** - Ninafurahi mimi kameneja, utamu mwingi na raha **UB1 MSH 1 UK 125**
>
> *Stimu sya Vangi Kindingi na* ***miraa*** *isilaa kimvye* - Stimu za bangi na pombe zinafanana **UB 2 MSH 2 UK 125**
>
> ***Kusema kweli*** *Matenzawa..*- Kusema kweli Matenzawa **UB 5, MSH 1 UK 126**

Maneno *'raha', 'miraa'* na '*kusema kweli'* ni maneno ya lugha ya Kiswahili ambayo yameingizwa katika muziki wa lugha ya Kikamba.

Mfano mwingine ni katika Muziki **WM KMB III UK 128** sentensi hizi;

> *Ungunia* ***simu*** *Kila wikendi yavika* - Huwa unanipigia simu kila wikendi ikifika **UB 2 MSH 1 UK 128**
>
> ***Mitoto*** *mwa ya* ***University*** *ngethe mbyu* - Wasichana wa chuo kikuu vipusa warembo **UB 2 MSH 3 UK 128**

Maneno *simu* na *mitoto* ni maneno ya lugha ya Kiswahili ilhali neno *university* ni la Kiingereza. Maneno haya yameingizwa katika muziki wa lugha ya Kikamba ili kuongeza ladha na kuvutia hadhira kusikiliza muziki huu.

Mifano mingine ni katika muziki **GF KIMB 1V UK 129**;

> *Niendaa* ***Airport*** *mbangite ulisa ndeke* - Huwa ninaenda uwanja wa ndege nikiwa na mpango wa kuabiri ndege **UB 3 MSH 1 UK 130**
>
> *Ngewa vai* ***sare*** *ya ndeke no mbaka ngaiva* - Lakini ninaambiwa hakuna sare lazima nilipie nauli ya ndege **UB 3 MSH 2 UK 130**
>
> *Nikusya nginya* ***Germany*** - Ninaenda hadi Ujerumani **UB 7 MSH 2 UK 130**

> *Niendete* ***by foot*** *nyie* - Ninaenda kwa miguu mimi **UB 7 MSH 4 UK 130**

Maneno *airport, Germany* na *by foot* ni maneno ya lugha ya Kiingereza ambayo yameingizwa katika muziki wa Kikamba. Neno *sare* ni neno la lugha ya Kiswahili linalomaanisha bila malipo yoyote. Mwimbaji ameyatumia kuweka dhahiri hisia zake za kimapenzi kwa mpenzi wake. Aina ya uhamishaji msimbo unaojitokeza katika mifano hii ni uhamishaji wa msimbo wa ndani ya sentensi, kwa kuwa waimbaji wamechanganya lugha mbili ndani ya sentensi moja ili kuunda athari ya kimtindo, kuimarisha mdundo wa muziki na kuvutia hadhira.

Pia waimbaji wametumia aina nyingine ya uhamishaji msimbo, ambapo mzungumzaji hubadilisha lugha kati ya sentensi tofauti, yaani sentensi moja inaweza kuwa katika lugha moja na sentensi inayofuata katika lugha nyingine. Kwa mfano katika muziki **AM KIMB VII UK 135**

> Mabaya mnanitakia Betty, *makamusyokea mara ikumi*, Mabaya mnayonitakia, Betty, yatawarudia mara kumi
>
> *Avakwa nzungawa ni Ngai Mumbi, wona ndivindya vena kitumi,* Mimi huwa nalindwa na Mungu Mwenyezi, ukiona nikinyamaza kuna sababu **UB 2 UK 135**
>
> *Yu nina dawa yenu mathethi, kwa muthenya dosi ni mala eli,* Sasa nina dawa yenu maadui, kwa siku dozi ni mara mbili.
>
> Na maisha yangu ni kama *movie, ithia ready kwina season two* - Na maisha yangu ni kama filamu, muwe tayari kuna sehemu ya pili **UB5 UK 135**

Katika beti hizi (**UB 2 na UB 5**) uhamishaji msimbo katika sentensi tofauti unadhihirika wazi katika muziki huu. Kwa mfano, katika mshororo wa "mabaya mnanitakia Betty, *makamusyokea mara ikumi* - mabaya mnayonitakia, Betty, yatawarudia mara kumi", lugha inayotumika inabadilika kati ya sentensi hizi kwa kutumia Kikamba na Kiswahili. Mchanganyiko unaonekana zaidi katika sentensi zinazofuata katika ubeti wa tano: "na maisha yangu ni kama movie, ithia ready kwina

season two – na maisha yangu ni kama filamu, muwe tayari kuna sehemu ya pili". Katika kila mfano, mabadiliko ya lugha yanatokea katika mipaka ya sentensi, jambo linaloashiria wazi kuwa msanii anatumia aina ya uhamishaji msimbo katika sentensi tofauti bali katika sentensi moja tofauti na mifano iliyopo hapo juu. Mbinu hii inamwezesha kuashiria tofauti za hisia, kuunda mvuto wa kishairi na kushughulikia hadhira mbalimbali kwa urahisi.

Kama anavyoeleza Myers-Scotton (1993), waimbaji huhamisha misimbo ili kuongeza maana ya ujumbe wanaolenga kupitisha kwa hadhira zao. Maoni haya yanaungwa mkono na Wambua (2001) anapoeleza kuwa, waimbaji wa muziki huhamisha misimbo kwa lengo la kujenga uhalisia wa maudhui, kusababisha hisia za kitamaduni, kuvutia hadhira na kuonyesha ubingwa wa ufanisi wa lugha. Matumizi ya mbinu ya kuhamisha msimbo huongeza uzito wa kishairi, jambo linalochangia athari za kimuundo na za kisanaa katika mazungumzo.

4.2.3.2 Msamiati wa Kukopa

Kulingana na Yule (1996) kukopa ni kuchukua maneno kutoka katika lugha nyingine na kuyaingiza katika lugha inayotumika. Ni uhamishaji wa leksia kutoka lugha moja hadi nyingine (Bynon, 1977). Katika nadharia ya umtindo, ukopaji unatambulika kama mkakati unaotumika katika lugha ili kuirutubisha na kuwezesha upitishaji wa ujumbe. Mkakati wa ukopaji ni mchakato ambao lugha moja huchukua maneno, dhana na matamshi ya lugha nyingine. Katika mtindo, ukopaji huchangia katika toni, sajili na mtindo mzima wa kazi ya sanaa (Leech, 1969). Waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba wamekopa msamiati kama inavyobainika katika muziki **SY KIMB I UK 125** mishororo ifuatayo;

> *Ningwiwa muyo* ***Kameneja*** - Ninahisi furaha Kameneja **UB I MSH I UK 125**
>
> *Ila ni* ***stimu*** *syakwa nyie* - Wakati nina stimu zangu mimi **UB I MSH 2 UK 125**
>
> *Stimu sya* ***vangi*** *kinding'i* - Stimu za bangi na pombe **UB 2 MSH 2 UK 125**
>
> *Ona kethwa ni* **chokola** -Hata kama ni chokora **UB 6 MSH 3 UK 125**

Ni kwitha ni ***murasta*** - Kwa kuwa mimi ni mrasta **UB 7 MSH 1 UK 126**

Sikala yakwa ni ***rosta*** - Sigara yangu ni rosta - **UB 7 MSH 3 UK 126**

Na ndi ***kilasi*** *Matenzawa, vai mundu tutatindanywa* - Na sina cheo Matenzawa, hakuna mtu ambaye hatuwezi kuishi naye - **UB 6 MSH 2 UK 126**

Katika mishororo hii, maneno yamekopwa kutoka kwa lugha ya Kiingereza na Kiswahili. Neno *kameneja* limekopwa kutoka kwa neno la Kiingereza 'manager', neno *stimu* limetokana na neno la Kiingereza 'steam' ilhali neno *kilasi* limetokana na la Kiingereza 'class'. Pia maneno *murasta* na *rosta* yanatokana na maneno ya Kiingereza *raster* na *roster*. Neno *vangi* limetokana na neno la Kiswahili *bangi* nalo neno *chokol*a linatoakana na neno la Kiswahili *chokora*. Kulingana na Myers-Scotton (1993), maneno huweza kukopwa ili kuonyesha ustadi wa lugha nyingine au kujitambulisha na kikundi cha watu fulani katika jamii. Mwimbaji katika wimbo huu **(SY)** amekopa maneno ili kujitambulisha na kundi la vijana wanaotumia mihadarati kwani anasifia uraibu wake wa kutumia dawa za kulevya. Mwimbaji anafanya hivyo kwa kutumia msamiati wa mtaani kama vile kujibandika jina *"Kamaneja"* na misamiati mingine inayotumika katika maeneo ya kutumia dawa za kulevya.

Katika muziki **WK KIMB V UK 131** maneno yafuatayo yamekopwa na kuingizwa katika lugha ya Kikamba.

Kumbavu - limetokana na neno la Kiswahili ***mpumbavu*** **UB 1 MSH 1 UK 131**

Sekondali - limetokana na neno la Kiingereza ***secondary*** **UB 2 MSH 3 UK 131**

Lipoti - kutokana na neno la Kiswahili **ripoti UB 3 MSH 1 UK 132**

Kama anavyodokeza Muathe (2016), ndiposa waimbaji waweze kupitisha jumbe zao kwa hadhira ni rahisi kukopa msamiati kuliko kuubuni upya. Hivyo waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba wametumia mkakati wa ukopaji ili kuweka

wazi jumbe zao kwa hadhira. Ukopaji wa maneno katika muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba umechangiwa na sababu kama vile baadhi ya hadhira ya muziki wa Benga wa jamii ya wakamba wamesoma na wana uelewa wa lugha nyingine (Wambua 2001).

4.2.3.3 Matumizi ya Visawe

Visawe ni maneno yenye maana sawa ama yanayokaribiana sana kimaana. Waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba wametumia visawe kwa mfano;

Katika muziki **SY KIMB I UK 125** mwimbaji ametumia msamiati ufuatao;

> *Ningwiwa **muyo** Kameneja, musasuko mwingi na **raha***
> - Ninahisi furaha Kameneja, utamu mwingi na raha.
> **UB 1 MSH 1 UK 125**

Maneno *muyo* na *raha* ni visawe vya neno raha au utamu lakini yametumika kwa pamoja katika wimbo huu. Mwimbaji anatumia maneno haya ili kuongeza mdundo na wizani katika muziki huu. Kwa kufanya hivyo mwimbaji analenga kuvutia wasikilizaji na kuufanya muziki huu uwe rahisi kukumbukwa. Urudiaji wa maneno yenye maana sawa unachangia kuweka athari ya kukumbukwa kwenye ubongo wa msikilizaji.

Katika wimbo **GF KIMB IV UK 129**,

> *Niuka na maau Germany Ruth **sweetie*** - Nitakuja kwa miguu Ruth **"sweetie,"**
>
> *No mbaka ngwone ngoo yakwa itulie* - Ni lazima nikuone roho yangu itulie. **UB 5 UK 130**
>
> *Ndisya kumiisya mbaka wiuika we **mbevi*** - Siwezi kuvumilia hadi utakapokuja **mpenzi,**
>
> *Kita umbeteela Germany niuka na mau* - Nisubiri Ujerumani nitakuja kwa miguu. **UB 6 UK 130**

Katika beti hizi maneno ***mbevi*** na ***sweetie*** katika ubeti wa tano mshororo wa kwanza, yametumika. Neno *mbevi* limetoholewa kutoka kwa neno la Kiingereza *babe* na vivyo hivyo neno *sweetie* limetokana na neno *sweet*, yote yameingizwa katika lugha ya Kikamba kwa kuzingatia mabadiliko ya kifonolojia na kimaana. Katika muziki huu

yametumika kama visawe ili kuonyesha mapenzi kwa lengo la kuimarisha mvuto wa kihisia kwa hadhira. Wambua (2001) akirejelea nyimbo za Kakai Kilonzo anadokeza kuwa, visawe hutumika kuondoa ukinaifu katika muziki. Wambua aligundua kuwa Kakai alitumia visawe katika baadhi ya nyimbo zake ili kuvutia hadhira yake. Kwa hivyo wasanii hutumia visawe ili kuwawezesha kufikisha athari lengwa kwa hadhira yao kadri inavyowezekena.

4.2.3.4 Msamiati wa Kubuni

Wasanii huweza kuunda msamiati wao wenyewe kupitia uchaguzi mbalimbali wa kimtindo. Leech (1969) anadokeza kuwa, uundaji wa msamiati una mchango mkubwa katika kuunda maana, hisia na toni katika matini. Nadharia ya umtindo inasisitiza kwamba msamiati hauhusu maana ya maneno ya mtu binafsi pekee bali jinsi maneno hayo yanavyofanya kazi pamoja ili kuunda muundo wa masimulizi au maudhui. Waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba wamebuni misamiati katika hali tofauti tofauti ili kufanikisha jumbe zao kwa hadhira lengwa.

Katika muziki **WK KIMB V UK 131** mwimbaji anatumia neno "***Wakatimba***" kama mada ya wimbo huu na kurudiwa mwishoni mwa kila ubeti. Hili ni jina la kubuni ambalo mwimbaji amempa mhusika kutokana na tabia zake. Kwa lugha ya kawaida neno hili lina maana ya 'makalio' katika lugha ya Kikamba. Neno hili hutumika katika jamii ya Wakamba kumkejeli mtu asiyekuwa na tabia za kupendeza. Kwa mfano, mhusika anayerejelewa katika wimbo huu ana tabia zisizopendeza kama vile kuzaa na kutupa mtoto kwenye mtaro kisha kuingilia anasa katika vilabu vya Mlolongo. Haya yanapatikana katika ubeti ufuatao.

> *Unaimutwae Pipeline ni nzamba ya mwako* - Ulikuwa umeolewa Pipeline na jamaa wa mjengo
>
> *Mukasyaa kana na itina ukekya mutauni* - Ukajifungua mtoto kisha ukamtupa kwenye mtaro
>
> *Ukatwika ndeki kali ilavu sya Mulolongo* - Ukawa msherati mkali katika vilabu vya Mlolongo
>
> *Niona wi ndia* ***Wakatimba*** *wi mana, na ndinakuuma Wakatimba kumbavu-* Naona ukiwa mjinga

Wakatimba wewe ni bure, na sijakutusi Wakatimba mpumbavu **UB 3 MSH 3, 4 ,5,6 UK 132**

Vilevile katika muziki **MK KIMB III UK 127;** mwimbaji amebuni jina la lakabu ambalo amempa kiongozi wa kisiasa anayemrejelea. Neno "*munene* –mkubwa" limetumika katika wimbo huu kurejelea kiongozi ambaye alichaguliwa na jamii ya mwimbaji. Neno hili limebuniwa ili kuleta taswira ya manufaa yanayotokana na uongozi (ukubwa). Kama anavyotaja mwimbaji manufaa hayo ni kama vile, kufaidika kwa jamii yake. Kwa mfano katika ubeti huu;

Navoyaa ngai mwa autethye - Nilimwomba mungu aghalau akusaidie

Muvaka nyie ngolwa ni kwivoyea - Hadi nikasahau kujiombea

Ngivoya unene uke kwitu - Nikiomba ukubwa uje kwetu

Munene *we nongi ututethye* - **Mkubwa** aghalau wewe utusaidie

Unene ni wosie nanyie ndyaa vaidika - Ukubwa umeuchukua na mimi sijafaidika

Unene ni twosie nanotukuthinaa - Ukubwa tuliuchukua lakini bado tunateseka

Ninguseng'a na ngikulya ii - Ninashangaa na kuuliza

Munene we kowolilwe - Mkubwa wewe kwani ulisahau **UB 2 UK 127**

Mwimbaji anasema kuwa alikuwa akiomba ukubwa uje katika jamii yake ndiposa mkubwa aghalau amsaidie yeye na jamii yake.

Pia, katika muziki **SY KIMB I UK 125** katika mshororo huu;

Nikyongete nyie Kativui, Mutulu nithiawa na raha - Nikiwa nimetafuna miraa, Mutulu mimi huwa na raha **UB 3 MSH 1 UK 125**

Neno "*nikyongete* -nikitafuna*"* limebuniwa ili kurahisisha uelewekaji wa ujumbe anaopitisha mwimbaji kwa njia ya kuvutia. Neno hili limetokana na kitendo cha kutumia dawa za kulevya za aina ya *miraa* ambazo hutumika kwa kutafunwa. Kama anavyoeleza Finnegan (1970) anaeleza kuwa wasanii hubuni msamiati mpya ili kuongeza maana, kuwasilisha hisia na kushirikisha hadhira kwa undani zaidi. Uundaji wa maneno kama haya unarahisisha uelewekaji wa ujumbe na kuongeza mvuto wa kisanaa kwa kutumia lugha ya jamii husika kwa njia ya ubunifu. Hivyo basi, matumizi ya neno "*nikyongete* - nikitafuna" yanaonyesha ubunifu wa msanii katika kubuni maneno ambayo yanaendana na muktadha wa kijamii na utamaduni.

4.2.4 Kiwango cha Kisintaksia

Kwa mujibu wa Leech (1969), kiwango hiki kinahusisha muundo wa sentensi pamoja na uchaguzi wa misamiati inayosaidia kuunda mtindo mzima wa kazi ya sanaa. Katika kiwango hiki, waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba wametumia aina mbalimbali za sentensi kama vile sentensi fupi fupi, sentensi ndefu, sentensi kiushi, sentensi huru na mkakati wa usambamba.

4.2.4.1 Sentensi Ndefu

Sentensi ndefu ni ile inayobeba hoja zaidi ya moja na hurejelewa kama sentensi ambatani au changamano. Kulingana na Wambua (2001), sentensi ndefu hutumiwa kupitisha mawazo yenye uzito kama vile huzuni, uvivu au mapenzi. Vilevile, Leech (1969) anadokeza kuwa sentensi ndefu huhusishwa na mtindo rasmi, wa kina au wa kimaelezo. Kwa hivyo, matumizi ya sentensi ndefu huongeza toni, mdundo na msisitizo katika maandishi au mazungumzo. Sentensi ndefu zimejitokeza katika muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba kama ifuatavyo:

Katika muziki **RN KIMB VI UK 132** sentensi zifuatazo;

> *Ngimina niasya Mbivilia yo yiasya* - Nikimaliza nasema kwamba Bibilia inasema,
>
> *Mundu wa kanzu ili akulile ula uteimwe* - Mtu aliye na kanzu mbili amwazime asiye na lolote,
>
> *Sammy Kasee tuikatate kukoma* - Sammy Kasee tusijaribu kulala

Twetele kunewa tondu moko tuinamo - Tukisubiri kupewa kwasababu mikono tunayo

Ndwike masavu, ika masavu, eka uvitya masavu - Fanya hesabu, fanya hesabu wacha kukosea hesabu

Woona wesa uvitya masavu ukatheelawa kitimba ni syana wakua ukomete valanda wa nyumba, nundu waiye mbesa ta ngaange - Utakapokosea hesabu utapigwa mateke kiunoni na watoto ukizeeka ukiwa umelala ferada mwa nyumba, kwa sababu ulikula pesa kama ambazo zimekaangwa **UB 4 UK 134**

Katika ubeti huu mwimbaji anarefusha sentensi ya mwisho. Anahadithia masahibu yanayotokana na ukosefu wa kudhibiti pesa. Mwimbaji anatumia mtindo wa kueleza kwa lengo la kuguza hisia za msikilizaji ili aweze kuelewa ujumbe unaopitishwa. Kwa mujibu wa Wambua (2001), waimbaji hutumia sentensi ndefu ili kupitisha maudhui yenye hisia nzito. Jambo hili husaidia kueleza kwa kina ujumbe unaopitishwa.

Vilevile, sentensi ndefu zinajitokeza katika muziki **SY KIMB I, UK 125** wake Ben Mbatha katika ubeti ufuatao:

Nikyongete nyie Kativui, Mutuli nithiawa na raha - Nikiwa ninatafuna miraa mimi Kativui, Mutulu mimi huwa na raha

Ninenaa na andu nesa nyie, makonaa ta ni wa kanisa - Huwa naongea na watu kwa ustaarabu mimi, hadi wanadhani mimi ni mtu wa kanisa

Matesi ni mundu vathei, Matenzawa ngesa utema - Huwa hawajui mimi ni mtu bure, Matenzawa nikitema miraa **UB 3 UK 125**

Katika ubeti huu mwimbaji ametumia sentensi changamano. Sentensi hizi zimejengwa kwa kutumia vipashio vingi vya kisarufi vilivyopangwa kwa namna isiyo ya moja kwa moja. Kwa mfano, katika sentensi hii *"Nikiwa ninatafuna miraa mimi Kativui, Mutulu mimi huwa na raha."* Kuna kiambishi cha wakati ‘nikiwa”

kinachofuatana na kitenzi kingine “ninatafuna.” Pia kuna mtindo wa kujirudia kwa nomino na kiwakilishi cha nafsi: “mimi Kativui, Mutulu mimi.” Jambo linalosababisha mchanganyiko wa viwakilishi. Mpangilio huu unaweka vishazi ndani ya vishazi, jambo linalohitaji uelewa wa kina ili kuelewa hoja kuu ya msemaji. Sentensi hizi ndefu zimetumika kueleza zaidi madhara ya uraibu wa dawa za kulevya anazotumia mwimbaji. Leech (1969) anadokeza kuwa sentensi ndefu huwapa wasanii nafasi ya kueleza kwa kina na kufafanua hoja mbalimbali. Leech anasema kwamba sentensi ndefu huleta hisia za kimawazo au utata na kutoa nafasi ya kuchunguza mawazo kwa kina. Aidha, anasisitiza kuwa sentensi ndefu husababisha hali ya taharuki inayoivutia hadhira kuendelea kusikiliza au kusoma kazi ya sanaa. Kwa mfano, katika ubeti uliopo hapo juu kwenye muziki (**SY),** sentensi ya kwanza ya wimbo huo haijakamilika kimaana bila kuongezewa sehemu ya pili ya sentensi hiyo. Mwimbaji anaposema; “nikiwa ninakula miraa mimi Kativui...” bila kuongeza chochote msikilizaji atabaki na hamu ya kutaka kujua nini kitakachotokea baadaye, baada ya “kula miraa.”

4.2.4.2 Sentensi Fupi

Kwa mujibu wa Cutts (2013), sentensi fupi ni zile ambazo hubeba hoja moja na hupitisha ujumbe moja kwa moja bila kutatanisha. Cutts, anadokeza kuwa sentensi hizi mara nyingi huundwa kwa neno moja au maneno yasiyozidi saba. Sentensi fupi huwasilisha wazo au hisia moja kwa uwazi na kwa athari ya moja kwa moja. Hutumika kusisitiza, kuharakisha mtiririko wa mawasiliano, kutoa athari za kihisia au za kishairi. Kinyume chake, sentensi ndefu huunganisha mawazo au virai mbalimbali, hivyo kutoa nafasi ya maelezo ya kina, taarifa za msingi au maelezo yenye tafakari zaidi.

Sentensi fupi katika muziki wa Benga zimetumika kama kipokeo au kiitikio ili kusisitiza ujumbe katika wimbo. Kwa mfano katika muziki **MK KIMB II UK 127**;

> *Ninguseng’a na ngikulya ii, munene we kowolilwe* ***(wiper)*** -Ninashangaa na kuuliza mkubwa kwani ulisahau? ***(wiper)*** **UB 1 MSH 7 UK 127**

Katika muziki mwimbaji ametumia sentensi ndefu kisha akatumia sentensi ya neno moja “wiper” ambalo limetamkwa mwishoni mwa kila ubeti wa muziki huu. Sentensi hii imetumika ili kusisitiza dhamira na kuonyesha wazi kiongozi anayerejelewa.

Mfano mwingine ni katika muziki **SY KIMB I UK 125** ubeti ufuatao;

> *Nikwithiwa ni murasta, na niishia ta murasta* - Kwa maana mimi ni mrasta, na huwa naishi kama mrasta.
>
> *Nikyongaa ta murasta, ngakusya vangi ta murasta* - Huwa natafuna miraa kama mrasta, na kuvuta bangi kama mrasta
>
> *Sikala yakwa ni rosta, inyusawa ni murasta* - Sigara yangu ni rosta, huwa inavutwa na mrasta. **UB 7 UK 126**

Mwimbaji ametumia sentensi fupi ambazo zimetenganishwa kwa vipumuo katika kila mshororo wa ubeti huu. Sentensi hizi zinaweka hoja ya msanii kuhusu uraibu wa dawa za kulevya wazi na zinaongeza wizani wa muziki huu. Vilevile katika muziki **RN KIMB VI UK 132** sentensi zifuatazo,

> *Raha Ndukauna, kuma tene ndukauna* - Raha haitawahi saidia, kutoka zamani raha haisaidii,
>
> *Ndwike masavu, ika masavu, eka uvitya masavu* - Fanya hesabu, fanya hesabu, wacha kukosea hesabu. **UB 1 MSH 1, 11 UK 133**

Mwimbaji anapoimba mishororo hii anatua na kuunda sentensi fupi zinazobeba hoja moja. Kwa mfano, sentensi "*Raha Ndukauna* - Raha haitawahi saidia," ni sentensi sahili inayobeba hoja moja kuhusu dhana ya raha. Sentensi hii ni fupi ikilinganishwa na sentensi anayotumia mwishoni mwa ubeti huu;

> *Ivundisye kusuvia mbesa syaku mwanake na uiyeka uyaa oou ta ngaange ti mboneki* - Jifunze kutunza pesa zako kijana, na uache kuzikula hivyo ni kama zimekarangwa, si rahisi kupatikana **UB 1 MSH 12 UK 133**

Mwimbaji ametumia sentensi fupi ili kusisitiza onyo kuhusiana na ubadhirifu wa fedha na kuelimisha jamii umuhimu wa kutunza pesa.

Sentensi fupi hutumika ili kuwezesha ujumbe kueleweka kwa urahisi bila kutatanisha. Pia, sentensi fupi huweza kutumiwa na wasanii ili kujenga taswira za matukio au

kueleza mazingira ambamo tukio limefanyika (Wambua, 2001). Sentensi fupi huwa rahisi kukumbuka na huweka ujumbe wazi pamoja na kuongeza mdundo wa muziki (Leech, 1969).

4.2.4.3 Sentensi Tongole

Kulingana na Wambua (2001) sentensi tongole ni zile ambazo zimetamkwa katikati mwa wimbo au muziki badala ya kuimbwa kwa mdundo wa wimbo au muziki husika. Baadhi ya waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba wametumia sentensi tongole katika muziki wao ambapo sentensi zingine zimetamkwa badala ya kuimbwa. Hali hii inatokea katika Wimbo **GF KIMB IV UK 129** kama ifuatavyo;

> *Nakwa ndina imbesya, na nowo i Kenya yoomie, nithi na maau nyie* - Nami sina pesa, na vile Kenya hii imekauka, nitaenda kwa miguu **UB 4 MSH 3 UK 130**
>
> *Onethwa ngavika mwaka uuya ungi, nithi na maau* - Hata kama nitafika mwaka ujao, nitaenda kwa miguu **UB 7 MSH 5 UK 130**

Sentensi hizi zimetumika ili kuongeza ujumbe ambao haupo katika beti za wimbo huu. Kwa kutumia sentensi hizi, mwimbaji anaendelea kueleza matatizo yanayomkumba, ambayo yamesababisha ashindwe kupata nauli ili aweze kumtembelea mpenzi wake aliye Ujerumani. Vilevile sentensi hizi zinaeleza zaidi mapenzi ya dhati aliyo nayo mwimbaji kwa mpenziwe anapoonyesha jitihada anazofanya ili aweze kumtembelea. Anaposema *"niuka na mauu* - nitaenda kwa miguu,*"* hali hii inaonyesha namna anavyojitolea kwa vyovyote vile ili kumtembelea mpenzi wake licha ya ukosefu wa nauli.

Vilevile katika wimbo **MK KIMB II UK 127** sentensi ya neno moja *'wiper'* imetamkwa mwishoni mwa kila mshororo wa mwisho wa beti za muziki huu.

> *Ninguseng'a na ngikulya ii munene we kowolilwe (wiper)* -Ninashangaa na kuuliza mkubwa kwani ulisahau? (*wiper*) **UB 1 MSH 7, UB 2 MSH 7 na UB 3 MSH 7 UK 127 - 128**

Neno hili limetamkwa mwishoni mwa kibwagizo cha muziki huu ili kuweka wazi kiongozi mahususi ambaye anarejelewa na mwimbaji.

Muziki **RN KIMB VI UK 132** mwimbaji ametumia sentensi tongole zifuatazo;

> *Ivundisye kusuvia mbesa syaku mwanake na uiyeka uyaa oou ta ngaange, ti mboneki* - Jifunze kutunza pesa zako kijana, na uache kuzitumia hivyo kama ambazo zimekaangwa, si rahisi kupatikana. **UB 1 MSH 11 UK 133**
>
> *Nyie Bosco Mulwa inamaainyie wia wa kivalua, mundu umbia neteele muthya wa mwei uikaavika twitha twaemaniwe* - Mimi, Bosco Mulwa, nilizoea kazi za vibarua; mtu ajaribu kuniambia nisubiri hadi mwisho wa mwezi, ukifika tutakuwa tayari tumekosana. **UB 2 MSH 10 UK 133**
>
> *Mundu uandikitwe mwai na ungi kivalua, andu asu onthe ni athukumi na methaa mayenda chapaa* - Mtu aliyeajiriwa kwa mwisho wa mwezi na mwingine wa kibarua, wote ni wafanyikazi na huwa wanadai chapaa. **UB 3 MSH 9 UK 134**
>
> *Woona wesa uvitya masavu ukatheelawa kitimba ni syana wakua ukomete valanda wa nyumba, nundu waiye mbesa ta ngaange* - Utakapokosea hesabu utapigwa mateke kiunoni na watoto ukizeeka ukiwa umelala feranda mwa nyumba, kwa sababu ulikula pesa kama ambazo zimekaangwa. **UB 4 MSH 6 UK 134**

Sentensi hizi zimetamkwa mwishoni mwa kila ubeti wa muziki huu. Mwimbaji amezitumia ili kusisitiza maudhui anayopitisha kama vile utunzaji wa fedha, kutoa onyo ya ubadhirifu wa fedha, ushirikiano wa kijamii katika kuinua uchumi na ukosefu wa kazi.

Kwa mujibu wa Leech (1969), wasanii huweza kutumia sentensi tongole ili kuwasilisha hisia za moja kwa moja na kuimarisha uhusiano wa kibinafsi na wasikilizaji. Wanapozitumia, sentensi hizi hufanya wimbo usikike kama mazungumzo ya ana kwa ana, hivyo kuwezesha wanamuziki kuhusisha wasikilizaji

kwa karibu zaidi. Mkakati huu husaidia waimbaji kuwasilisha maneno kana kwamba wanazungumza na wasikilizaji au wahusika moja kwa moja. Mbinu hii huongeza athari za kihisia na kukuza uhusiano wa karibu kati ya mwimbaji na hadhira lengwa.

4.2.4.4 Sentensi za Maswali

Sentensi za maswali zinazotumika katika muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba ni za kibalagha. Maswali ya kibalagha ni mtindo wa lugha unaotumia maswali yasiyohitaji majibu ya moja kwa moja, bali hutumika kusisitiza ujumbe unaowasilishwa. Balagha ni ustadi wa kutumia lugha kwa namna ya kuvutia, kushawishi au kuburudisha. Hivyo basi, maswali ya balagha katika muziki hulenga kusisimua na kuchochea hisia za hadhira pamoja na kuwavutia zaidi kusikiliza kazi za wasanii (Wambua, 2001). Waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba wametumia sentensi za balagha ili kufikia malengo tofauti tofauti kama ifuatavyo:

Katika muziki **MK KIMB II UK 127** wake Ken Maria, mshororo ufuatao ni wa kibalagha;

> *Ninguseng'a na ngikulya ii, Munene ko wolilwe?* - Ninashangaa na kuuliza, Mkubwa kwani ulisahau? **UB 1 MSH 7 UK 127**

Sentensi hii imetumika kama kibwagizo mwishoni mwa kila ubeti wa muziki huu. Mwimbaji anauliza swali ili kuteka hisia za anayelengwa ambaye ni 'kiongozi'' ndiposa aweze kukumbuka na kushughulikia matatizo yake. Swali hili limetumika kusisitiza ujumbe, kwa kuonyesha kutoridhika kwa mwimbaji kutokana na usaliti aliofanyiwa na "kiongozi" anayemrejelea.

Sentensi za maswali vilevile zinajitokeza katika muziki **WK KIMB VI UK 131**;

> *Wakatimba ni kyau? kana ni kukosa masomo?* - Wakatimba ni nini? ama ni kukosa masomo? **UB 2 MSH 1 UK 131**

Mwimbaji anauliza swali kwa sababu anashangazwa na tabia za mhusika "Wakatimba." Anajaribu kuwaonya watu wengine katika jamii ambao wanaweza kuwa na tabia kama za mhusika anayerejelewa. Kwa kuuliza swali hili mwimbaji analenga kuvutia hisia za hadhira lengwa kwa kuwafanya wafikirie zaidi na kutafakari ujumbe wa muziki huu.

Wasanii wa muziki mara nyingi hutumia maswali ya balagha kama mbinu ya kisanaa ili kuchochea fikra, kuhusisha wasikilizaji kihisia na kusisitiza dhamira bila kutarajia majibu ya moja kwa moja. Mbinu hii huongeza nguvu ya ushawishi na kuhimiza tafakari ya kina katika tungo kwa kuwaalika wasikilizaji kutafakari ujumbe badala ya kupewa maelezo ya moja kwa moja (Moore, 2012). Katika muziki wa kisasa, matumizi ya maswali ya balagha huweza kuunda athari ya mazungumzo ya ndani, yakimvutia msikilizaji kushiriki kiakili na kihisia, hivyo kuongeza uhusiano na uelewa wa ujumbe wa wimbo (Brackett, 2000).

4.2.4.5 Usambamba

Kwa mujibu wa Jakobson (1960) na Leech (1969), usambamba ni ruwaza zinazojitokeza mahali ambapo kuna vokali au konsonanti zinazofuatana kwa mfululizo maalum. Ni mbinu ya kisarufi inayohusisha kurudia muundo wa kisarufi katika sehemu mbalimbali za kifasihi, kama vile mishororo, vifungu au sentensi, ili kuleta uwiano na msisitizo. Katika nyimbo, usambamba hutumika kuimarisha muktadha wa kihisia, kujenga mdundo na kuwasilisha mawazo kwa njia inayoweza kukumbukwa kwa urahisi. Tazama mfano huu katika muziki **MK KIMB II UK 127**;

> ***Munene wambiiye*** *tukambeini* - Mkubwa uliniambia tupige kampeni
>
> *Nikenda* ***kivila kyuke kwitu*** - Ndiposa kiti kije kwetu
>
> ***Munene wambiiye*** *we ukanzuvia* - Mkubwa uliniambia wewe utanitunza
>
> *Oila* ***kivila kiuka kwitu*** - Pindi tu kiti kikikuja kwetu
>
> ***Kivila niwoosie*** *na nyie ndwanzuvia* - Kiti ulichukua na mimi haunitunzi
>
> ***Kivila ni twosie*** *na we mwa niwaie* - Kiti tulichukua na wewe ukapotea **UB 1 UK 127**

Ubeti huu unaonyesha matumizi ya kimakusudi ya usambamba wa kisintaksia na kisemantiki kama mbinu ya sanaa ili kuimarisha uwasilishaji wa dhamira. Usambamba wa kisintaksia unajitokeza katika muundo wa kisarufi unaojirudia katika kila mshororo, ambapo vifungu vya maneno vinaanza na kiima kikifuatwa na kitenzi

na kiambatisho, kwa mfano, “*Munene wambiiye tukambeini* - Mkubwa uliniambia tupige kampeni,” “*Munene wambiiye we ukanzuvia* - Mkubwa uliniambia wewe utanitunza.” Marudio haya ya muundo yanajenga mpangilio wa kishairi hivyo kuimarisha mtiririko wa wazo na kusisitiza ujumbe. Pia kuna usambamba wa maana au wa mawazo ambao umetumika kuzidisha maana kwa kulinganisha au kufafanua mawazo yanayokinzana, kama vile ahadi dhidi ya usaliti. Hili linajitokeza mwimbaji anaposema; “*we ukanzuvia* - wewe utanitunza*”* dhidi ya “*nyie nduunzuvia* - mimi haunitunzi.” Pia usambamba wa kimaana unaonekana kwa namna kila mshororo unavyowasilisha mawazo yanayohusiana na yanayotiririka kwa mfululizo kuhusu matokeo ya kupokea madaraka ya kisiasa “*kivila*- kiti.” Mwimbaji anasimulia mfululizo wa matukio yanayoonyesha hali ya kuvunjika moyo wakati ambapo kiti cha uongozi kinawafikia "Pindi tu kiti kikikuja kwetu," kwani kiongozi anashindwa kutimiza ahadi "Kiti ulichukua na mimi haunitunzi" na hatimaye kutoweka kabisa "Kiti tulichukua na wewe ukapotea.” Usambamba huu unaonyesha ongezeko la hali ya kukata tamaa. Vilevile usambamba wa anafora unadhihirika kupitia kurudiwa kwa neno *"kivila* - Kiti*"* mwanzoni mwa mishororo ya ubeti huu kwa mfululizo maalum. Jambo hili linasaidia kuimarisha mshikamano wa kimaudhui na mtindo wa muziki huu. Marudio haya hayasisitizi tu uzito wa kiti cha uongozi kama ishara, bali pia yanaunda muundo wa kishairi unaoakisi msisitizo wa kihisia wa mzungumzaji. Aina hizi za usambamba zinatumika kuangazia dhamira kuu ya kukata tamaa kisiasa, ambapo mzungumzaji anatathmini ahadi zilizotolewa wakati wa kampeni ambazo baadaye hazikutimizwa baada ya kiongozi kupata madaraka. Hivyo basi, usambamba huu hauleti tu urari wa kishairi bali pia unaimarisha nguvu ya mawasiliano ya ujumbe wa kijamii na kisiasa katika muziki.

Maoni haya yanahusiana na utafiti uliofanywa na Campbell (1983) kuhusu nyimbo za Kiswahili, alionyesha jinsi usambamba unavyotumika katika nyimbo za watoto na za watu wazima, hasa katika muktadha wa ngoma. Ilibainika kuwa nyimbo za Kiswahili hutumia mbinu za kisarufi kama vile kurudia maneno, vifungu na mistari ili kuleta mdundo na kuimarisha ujumbe wa kijamii na kitamaduni.

Usambamba pia unajitokeza katika muziki **SY KIMB I, UK 125** katika sentensi zifuatazo;

*Ni kwithiwa ni **Murasta**, na niishia **kimrasta*** - Kwa maana mimi ni mrasta, na huwa naishi kama mrasta

*Nikyongaa ta **murasta**, ngakusya vangi ta **murasta*** - Huwa natafuna miraa kama mrasta, na kuvuta bangi kama mrasta

*Sikala yakwa ni **rosta**, inyusawa na **murasta*** - Sigara yangu ni rosta, huwa inavutwa na mrasta **UB 7 UK 126**

Ubeti huu unahusisha usambamba wa kisintaksia, wa kimaana na wa anafora, ambao umetumika kwa pamoja ili kuimarisha uwasilishaji wa dhamira ya utambulisho wa *rastafari* (mrasta). Usambamba wa kisintaksia unaonekana kupitia marudio na muundo wa sentensi za mshororo wa kwanza na wa pili, ambapo kila mshororo unafuata mtindo sawa wa kisarufi unaojumuisha kiima, kitenzi na kiambatisho. Vipengele hivi vinachangiwa na matumizi ya kiunganishi "na." Kwa mfano, katika mishororo *"Ni kwithiwa ni Murasta, na niishia kimrasta*- kwa maana mimi ni mrasta, na huwa naishi kama mrasta*"* na *"Nikyongaa ta murasta, ngakusya vangi ta murasta* - Huwa natafuna miraa kama mrasta, na kuvuta bangi kama mrasta*."* Marudio haya ya muundo yanaleta urari wa kishairi na mshikamano wa kisanaa. Usambamba wa kimaana unaimarishwa kupitia mwendelezo wa mawazo yanayohusiana na dhamira kuu ya mtindo wa maisha ya murasta. Vilevile, usambamba wa anafora unadhihirika kupitia kurudiwa kwa neno "mrasta/rosta", ambalo linajitokeza kwa msisitizo mwishoni mwa mishororo ya ubeti huu. Jambo hili linaangazia uhusiano na fahari ya mwimbaji ya kujitambulisha na kundi la *Rastafari*. Kwa pamoja, aina hizi za usambamba zinasaidia kuthibitisha utambulisho, kuimarisha urari wa muziki na kuwasilisha ujumbe kwa namna ya kishairi na ya kipekee. Usambamba ni mkakati wa kimtindo unaotumika kuongeza ujumi katika kazi ya sanaa na kusisitiza ujumbe (Leech,1969). Kwa hivyo usambamba katika ubeti huu unatumika kuongeza mdundo na wizani katika muziki huu ili kuimarisha ujumi na kuvutia hadhira lengwa.

4.2.4.6 Ukiushi wa Kisintaksia

Nyandiwa (2015) akimrejelea Cluysenaar (1976:31) anadokeza kuwa ukiushi ni kuondoka katika maana inayotarajiwa katika viwango tofauti vya lugha kama vile leksia, fonolojia, mofolojia, semantiki na sarufi. Viwango hivyo mbalimbali vinaweza kuwa katika sarufi na fonolojia au katika viwango vya sentensi na virai. Ukiushi

huashiria ukuaji wa utanzu wa fasihi unaohusika (Mohammed, 1986). Ukiushi wa kisintaksia hutokana na kukiuka kanuni za kutunga sentensi au uundaji wa maneno. Leech (1969) anaeleza kuwa ukiushi wa kisintaksia unahusisha ukiukaji wa muundo wa kawaida wa matumizi ya lugha kama vile matumizi ya sentensi zenye dosari. Ukiushi huimarisha mawasiliano ya kisanaa katika kazi za fasihi kwa kuleta ubunifu, kusisitiza maana na kuongeza kina cha dhamira. Kama anavyoeleza Leech (1969), ukiushi huwezesha matumizi ya lugha ya kimtindo hivyo kumruhusu mwandishi kuvunja kaida za kisarufi ili kuunda mpangilio wa kishairi. Jambo hili husaidia wasanii kuakisi hali ya kisaikolojia ya hadhira lengwa na kuwahusisha katika fasiri za kina za kazi za fasihi. Ukiushi huboresha kwa kiasi kikubwa maudhui na muundo wa kazi ya fasihi.

Waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba wametumia sentensi zisizozingatia sarufi kama zifuatazo;

Katika muziki **WK KIMB V UK 131** sentensi ifuatayo;

> *Wakatimba nyie kweli* ***nguseng'a*** *ni tabia syaku* - Wakatimba mimi kweli nashangaa kwa sababu ya tabia zako **UB 1 MSH 1 UK 131**

Katika sentensi hii, neno '*nguseng'a'* (nashangaa) limedondolewa fonimu ya nafsi 'ni-' na hivyo kufupishwa kutoka muundo wa kawaida '*ninguseng'a'* (Ninashangaa*)*. Ukiushi huu wa kisintaksia unasababishwa na matumizi ya mkakati wa inkisari. Unaathiri muundo wa sentensi kwa kuvunja kanuni za lugha sanifu, kwani kiambajengo cha nafsi ya kwanza hakipo wazi. Badala yake, maana ya nafsi inabebwa na muktadha wa kisemantiki. Mbinu hii inachochea msisitizo wa hisia za mshangao na kutoridhishwa, na wakati huo huo kuongeza uhalisia wa mazungumzo ya kila siku na mvuto wa kisanaa katika muziki huu.

Mfano mwingine ni katika wimbo **GF KIMB IV, 129** ambapo kuna sentensi ifuatayo;

> ***Ngilasya niilye****, ngethia ndiota na Mwende –.* Huwa nimeekaa, najipata nikiota na Mwende
>
> *Ngethe yi muingo, Germany ngewa kuiya* - Msichana aliye nchi ya ng'ambo Ujerumani kweli nahisi kulia **UB 1 UK 129**

Sentensi '*ngilasya niilye* - huwa nimeekaa' haijakamilika mwimbaji anatua anapoimba sehemu ya sentensi hiyo kuashiria kipumuo jambo linalofanya sentensi hiyo kuwa kishazi kitegemezi kinachohitaji kukamilishwa. Mwimbaji anakatiza kauli hiyo kupumua au kutua katika uimbaji, kabla ya kuendelea na *"ngethia ndiota na Mwende* - najipata nikiota na Mwende." Ukiushi huu wa sintaksia unaonyesha matumizi ya sentensi isiyo kamili kama mbinu ya kisanaa ya kuonyesha mtiririko wa fikra, kusisitiza hisia au kuwasilisha hali ya kisaikolojia ya mzungumzaji. Kwa kutumia kishazi kitegemezi, mwimbaji anajenga hali ya kutarajia au kutegemea mwendelezo wa mawazo, ambayo yanajibiwa au kuendelezwa katika sehemu inayofuata. Aidha, kipumuo kinachotumika hapa kina nafasi muhimu katika uwasilishaji wa kisanii kwa kusisitiza hali ya kutafakari au hali ya mchanganyiko wa fikra kuhusu Mwende. Hali hii inaifanya sentensi hii ionekane kuwa ya kihisia na ya kibinafsi, ikionyesha msisimko au mshikamano wa hisia za ndani za mwimbaji kwa mpenzi wake. Hivyo basi, ukiushi huu wa kisintaksia unatoa nafasi ya kisanaa ya kuwasilisha fikra kwa njia ya kipekee, inayotofautiana na miundo ya kawaida ya kisarufi ili kuleta athari ya kihisia kwa hadhira.

Wasanii hutumia mkakati wa ukiushi ili kuongeza mdundo wa muziki na kuteka hisia za hadhira yao (Leech,1969). Gafur na wenzake (2021) wanadokeza kuwa, ukiushi wa kisintaksia huwaruhusu wanamuziki kufupisha hisia kwa maneno machache. Ilibainika kuwa mwimbaji Ed Sheeran mara kwa mara alitumia vitenzi visaidizi katika nyimbo zake ili kuongeza mdundo wa wimbo. Mbinu hii inawezesha uwasilishaji wa moja kwa moja wa hisia na kuleta mtiririko wa muziki.

4.2.5 Kiwango cha Semantiki

Kiwango hiki kinahusu namna matumizi ya lugha yanavyoathiri maana. Ni kiwango kinachohusu matumizi ya lugha ya kitamathali na namna lugha hiyo inavyopitisha maana inayokusudiwa. Mikakati inayochunguzwa chini ya kiwango hiki ni kama vile ukinzani, kinaya, oksimoroni, vitendawili, kejeli na tautolojia (Indangasi, 1998)

4.2.5.1 Tautolojia

Tautolojia ni mbinu ya kimtindo inayohusisha kurudia wazo au dhana kwa kutumia maneno tofauti, lakini yanayowasilisha maana moja kimsingi. Mkakati huu hutumika mara nyingi katika kazi za sanaa kukuza sifa za wahusika au kuendeleza maudhui.

Mkakati huu unatumika katika muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba kukuza maana kama ifuatavyo:

Katika muziki **SY KIMB I UK 125** tautolojia imetumika katika mishororo ifuatayo;

> *Ningwiwa muyo Kameneja, musasuko mwingi na raha* - Ninafurahi mimi Kameneja, utamu mwingi na raha **UB 1 MSH 1 UK 125**

Katika mshororo huu usemi "utamu na raha" kimsingi unawasilisha hali sawa ya kuridhika au kutosheka, inayochangia wazo la furaha. Tautolojia hii ina umuhimu wa kisemantiki na kisanaa kwa kuwa inasisitiza hali ya kuridhika na kutosheka inayotokana na furaha ya mhusika. Kwa kutumia maneno mawili yanayowasilisha maana sawa msanii anaimarisha wazo la furaha kwa kulipa uzito wa kiishara na kihisia.

Vilevile katika muziki **SY KIMB I UK 125** ubeti ufuatao;

> *Ni kwithiwa ni Murasta, na niishia kimrasta.* - Kwa maana mimi ni mrasta, na huwa ninaishi kama mrasta
>
> *Nikyongaa ta murasta, ngakusya vangi ta murasta* - Huwa natafuna miraa kama mrasta, na kuvuta bangi kama mrasta **UB 7 MSH 1, 2 UK 126**

Mshororo wa kwanza ni wa kitautolojia kwa sababu kusema "Mimi ni mrasta" na "ninaishi kama mrasta" kimsingi ni kauli zinazosisitiza utambulisho wa mwimbaji bila kuongeza habari mpya. Kauli hizi zinaeleza sifa za mwimbaji kama mtu aliye na uraibu wa dawa za kulevya. Mshororo wa pili "huwa natafuna miraa kama mrasta, na kuvuta bangi kama mrasta", vishazi vyote viwili vinasisitiza wazo la kuwa "mrasta" kupitia vitendo vya kutafuna miraa na kuvuta bangi. Mishororo hii inasisitiza mtindo wa maisha ya mwimbaji bila kutoa tofauti zaidi.

Vilevile tautolojia imetumika katika muziki **WM KIMB III UK 128** katika ubeti huu:

> *We wasa ii kitindo kyaku ninakola* -Wewe rafiki yangu urafiki wako sitaki
>
> *Kitumi nyie ndikwenda utindana na mbili* - Kwa sababu mimi sitaki kuishi na kupe

Unyonyae tupesa twakwa uteiwa nthoni - Unatumia pesa zangu bila kuona aibu

Ninakola we wasa tutaane vathei - Sitaki huo urafiki usinidai chochote **UB 1 UK 128**

Katika ubeti huu kauli "wewe rafiki yangu urafiki wako sitaki, unyonye pesa zangu bila kuona aibu na sitaki huo rafiki usinidai chochote," ni za kitautolojia. Hii ni kwa sababu zinaonyesha hisia za kutowajibika kwa rafiki ya mwimbaji bila kuongeza habari zozote. Vipengele vya tautolojia katika ubeti huu vinatumika kuimarisha mada za usaliti, unyonyaji na mzigo wa kihisia ndani ya urafiki. Kwa kurudia misemo hii, mwimbaji anaonyesha kiwango cha juu cha kufadhaika kutokana na usaliti au unyonyaji na kutoridhika na uhusiano huo, akisisitiza uamuzi wake wa kukata kabisa mahusiano hayo. Sentensi hizi za kitautolojia zimetumika ili kutilia nguvu ujumbe wa wimbo huu. Urudiaji huu unaongeza athari za kihisia na kujenga mdundo kwa lengo la kuvutia wasikilizaji. Pia unatumika kuufanya ujumbe kukumbukwa kwa urahisi. Matumizi ya tautolojia huongeza kina cha hisia katika lugha (Fadlilah na wenzake 2021).

4.2.5.2 Ukinzani

Ukinzani huhusisha matumizi ya vipengele vinavyopingana kimaana katika kazi ya sanaa ili kuchochea hisia za hadhira lengwa. Ukinzani huweza kuchukua aina tofauti kama vile wahusika wenye sifa zinazopingana, maudhui yanayopingana na uchaguzi wa vipengele vya lugha vinavyopingana. Waimbaji wa muziki wa Benga wametumia mkakati wa ukinzani kama ifuatavyo:

Katika muziki **MK KIMB II UK 127**;

Munene wambiiye tukambeini - Mkubwa uliniambia tupige kampeni

Nikenda kivila kyuke kwitu - Ndiposa kiti kije kwetu

Munene wambiiye we ukanzuvia - Mkubwa uliniambia wewe utanitunza

Oila kivila kiuka kwitu - Pindi tu kiti kikikuja kwetu

Kivila niwoosie na nyie ndwanzuvia - Kiti ulichukua na mimi haunitunzi

Kivila ni twosie na we mwa niwaie - Kiti tulichukua na wewe ukapotea **UB 1 UK 127**

Katika ubeti huu mwimbaji anapitisha maana kinzani ya matarajio dhidi ya ukweli anaposema "*waambiiye tukampeini, waambiye ukanzuvia* - uliniambia nipige kampeni; uliniambia utanitunza." Hapa, mzungumzaji anatoa matarajio makubwa kulingana na zile ahadi zilizotolewa, tofauti na hali ya kukata tamaa inayofuata wakati ahadi hizo zinavunjwa. Kauli "*kivila ni twoosie na nyie nduunzuvia, kivila nitwoosie na we mwa niwaaie* - kiti ulichukua na mimi haunitunzi na kiti tulichukua na wewe ulipotea" zinaonyesha kuhama kutoka hali ya kutunzwa hadi hali ya kupuuzwa. Kauli hizi zinaonyesha ukinzani wa uaminifu ambao mwimbaji alikuwa nao kwa "mkubwa" ambaye baadaye anausaliti uaminifu huo kwa kutomjali mwimbaji. Ukinzani huu unaimarisha maudhui ya usaliti wa kisiasa katika muziki huu.

Vilevile katika muziki **MK KIMB II UK 127** ubeti ufuatao:

Navoyaa ngai mwa autethyie - Nilimwomba mungu aghalau akusaidie

Muvaka nyie ngolwa ni kwivoyea - Hadi nikasahau kujiombea

Ngivoya unene uke kwitu - Nikiomba ukubwa uje kwetu

Munene we ututethye - Mkubwa angalau wewe utusaidie

Unene niwosie na nyie ndyaa vaidika - Ukubwa uliupata ila mimi sikufaidika

Unene ni twosie nanotukuthinaa - Ukubwa tuliupata na bado tunateseka **UB 2 UK 127**

Katika ubeti huu, mwimbaji anaonyesha ukinzani wa kihisia kati ya matumaini ya jamii kwa pamoja na maumivu ya mtu binafsi. Anaposema "nikiomba ukubwa uje kwetu na ukubwa uliupata ila mimi sikufaidika", anaibua hali ambapo mafanikio

yaliyotamaniwa kwa jamii nzima yamepatikana, lakini yeye binafsi hakunufaika. Hii inaibua ukinzani kati ya ndoto ya mafanikio ya kijamii na hali halisi ya kutengwa au kupuuzwa kwa mtu binafsi. Ukinzani huu unazidi kujitokeza katika kauli "nilimwomba Mungu angalau akusaidie, hadi nikasahu kujiombea", ambapo mwimbaji anaeleza jinsi alivyomwombea mtu mwingine kwa dhati kiasi cha kujisahau mwenyewe. Mwimbaji anaamini katika mafanikio ya kiongozi, lakini mafanikio hayo hayaonyeshi huruma wala faida kwake binafsi, jambo linaloonyesha hisia za kukata tamaa. Kwa jumla, ukinzani huu unasitiri ndani yake ujumbe wa matumaini yanayokinzana na hali ya kusahaulika, hivyo kuimarisha maudhui ya usaliti wa matarajio ya kisiasa. Mbinu hii inaongeza nguvu hisia za mwimbaji na kuchochea usikilizaji na hisia za huruma kutoka kwa hadhira.

Ukinzani vilevile unajitokeza katika muziki **WK KIMB V UK 131** kama ifuatavyo;

> *Wakatimba nyie kweli nguseng'a ni tabia syaku* - Wakatimba mimi kweli ninashangaa kwa tabia zako
>
> *Ona kutwika wi mwanake wi akili ndogo* - Hata ingawa wewe ni mrembo una akili ndogo
>
> *Muvaile waku ni ukengana wi mundu wa vata* - Mavazi yako yanaweza kudanganya kwamba wewe ni mtu wa maana
>
> *Indi malondu maku we ve amwe me kithekani* - Lakini bado wapo kondoo wako walio kichakani
>
> *Niona wi ndia Wakatimba wi mana* - Naona ukiwa mjinga Wakatimba wewe ni bure
>
> *Na ndinakuuma Wakatimba kumbavu* - Na sijakutusi Wakatimba mpumbavu **UB 1 UK 131**

Katika ubeti huu mshororo wa pili mwimbaji anasema "ingawa wewe ni mrembo, una akili ndogo." Mshororo huu unaonyesha ukinzani wa urembo wa kimwili na ukosefu wa akili. Mzungumzaji anakubaliana na urembo wa mhusika huyo ilhali anakosoa uwezo wake wa kiakili, akionyesha mgongano kati ya sura ya nje na uwezo wa kiakili. Pia ukinzani wa maana unajitokeza katika mshororo wa sita mwimbaji anaposema

"*na ndinakuuma Wakatimba kumbavu* - na sijakutusi Wakatimba mpumbavu." Ingawa mwimbaji anamtusi mhusika moja kwa moja kwa kumwita "mpumbavu" anasema hajamtusi. Pia katika wimbo huu **(WK)** mwimbaji anauliza;

> "*Wakatimba ni kyau? kana ni kukosa masomo?* - Wakatimba ni nini? ama ni ukosefu wa masomo?" **UB 2 MSH 1 UK 131**

Hapa mwimbaji anahoji iwapo matendo ya mhusika yanatokana na ujinga au ukosefu wa elimu. Tofauti hii inaangazia mitazamo ya jamii inayounganisha elimu na busara na uamuzi bora, ikizua maswali kuhusu uwajibikaji na mambo yanayoathiri uchaguzi. Wanamuziki kimkakati hutumia maana tofauti katika nyimbo zao kama kipengele cha kimtindo ili kuongeza uzito wa maudhui, kuibua majibu ya kihisia, na kuboresha kushiriki kwa wasikilizaji. Wasanii wa muziki hutumia mkakati wa ukinzani kuongeza kina cha hisia na kupitisha ujumbe (Fadlilah na wenzake 2021).

4.2.5.3 Kinaya

Kinaya ni kinyume cha matarajio. Kwa mujibu wa Leech (1969) kinaya huhusisha tofauti kati ya kile kinachosemwa na kinachomaanishwa, au kinachotarajiwa na kile kinachotokea. Tofauti hii kwa kawaida hutegemea uelewa wa pamoja au muktadha kati ya mzungumzaji na hadhira.Waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba wametumia kinaya katika miziki yao kama ifuatavyo;

Katika muziki **MK KIMB II UK 127** wake Ken Maria kinaya kimetumika katika ubeti ufuatao:

> *Navoyaa ngai mwa autethye* - Nilimwomba mungu akusaidie
>
> *Muvaka nyie ngolwa ni kwivoyea* - Hadi nikasahau kujiombea
>
> *Ngivoya unene uke kwitu* - Nikiomba ukubwa uje kwetu
>
> *Munene we nongi ututethye* - Mkubwa wewe aghalau utusaidie
>
> *Unene ni wosie nanyie ndyaa vaidika* -Ukubwa uliupata na mimi sijafaidika

Unene ni twosie nanotukuthinaa - Ukubwa tuliuchukua lakini tunateseka

Ninguseng'a na ngikulya ii - Ninashangaa na kuuliza

Munene we kowolilwe - Mkubwa wewe kwani ulisahau **UB 2 UK 127**

Katika ubeti huu ni kinaya kuwa mwimbaji alikuwa anamwombea kiongozi hadi akasahau kujiombea lakini baada ya kuchukua uongozi, kiongozi akamsahau. Anasema kuwa ukubwa walichukua lakini yeye na jamii yake bado wanateseka. jambo hili ni kinaya kwani inatarajiwa mwimbaji na jamii yake wafaidike baada ya kiongozi kupata mamlaka.

Pia katika wimbo **GF KIMB IV UK 129** wake Ken Maria mwimbaji ametumia kinaya katika ubeti huu;

Niuka na maau Germany Ruth sweetie - Nitakuja kwa miguu hadi Ujerumani Ruth "sweetie"

No mbaka ngwone ngoo yakwa itulie - Lazima nikuone roho yangu itulie **UB 5 UK 130**

Ndisya kumiisya mbaka wiuika we mbevi - Siwezi kuvumilia hadi uje wewe mpenzi

Kita umbeteela Germany niuka na mau – Nisubiri Ujerumani nitakuja kwa miguu **UB 6 UK 130**

Mwimbaji ametumia kinaya katika ubeti huu kwa kusema kwamba *"Nitakuja kwa miguu Ujerumani Ruth sweetie"*, akimaanisha kuwa yuko tayari kumfuata mpenzi wake hadi Ujerumani kwa njia ya kutembea kwa miguu. Hili ni jambo lisilowezekana kwa hali ya kawaida, kwani kutoka Kenya hadi Ujerumani ni safari ndefu inayohitaji usafiri wa kisasa kama ndege au meli. Kinaya kimetumika kuonyesha uzito wa hisia au dhamira ya mwimbaji. Anasisitiza uzito wa mapenzi yake na kuonyesha yuko tayari kufanya jambo lolote, hata lisilowezekana, ilimradi tu afike kwa mpenzi wake.

Vilevile, katika muziki **WK KIMB V UK 131** katika ubeti huu;

Wakatimba nyie kweli nguseng'a ni tabia syaku - Wakatimba mimi kweli nashangazwa na tabia zako

Ona kutwika wi mwanake wi akili ndogo - Hata ingawa wewe ni mrembo akili yako ni ndogo **UB 1 MSH 1, 2 UK 131**

Wakatimba ni kyau? kana ni kukosa masomo - Wakatimba ni nini ama ni kukosa masomo

Na nengi yila twakomanie wambiiye wio sawa- Lakini tulipokutana ulinihakikishia kwamba ungali sawa

Kyethivo nikwo wasomee sekondali nene - Shule ya Kyethivo, ndipo uliposomea sekondari kubwa **UB 2, MSH 1,2, 3 UK 131**

Katika ubeti huu mwimbaji ametumia kinaya anapomzungumzia mhusika 'Wakatimba'. Anasema kwamba Wakatimba ni mrembo na amesoma hadi sekondari kubwa ya Kyethivo, lakini tabia zake hazilingani na kiwango chake cha elimu wala haiba yake. Kwa mfano, mwimbaji anashangazwa na jinsi akili ya Wakatimba inavyofanya kazi, anaposema: *"Ona kutwika wi mwanake wi akili ndogo* - hata ingawa wewe ni mrembo akili yako ni ndogo," kumaanisha kuwa, licha ya uzuri wake, ana akili ndogo. Zaidi ya hayo, licha ya kusoma hadi sekondari, Wakatimba anajihusisha na matendo yasiyoendana na mtu mwenye elimu, kama vile kujifungua mtoto na kumtupa kwenye mtaro **(UB 3 MSH 3)**, kitendo ambacho huenda kikahusishwa na ujinga au ukosefu wa maadili. Jambo hili linasababisha kinaya baina ya matarajio ya kijamii kwa mtu aliyesoma na urembo wake, na matendo halisi ya mhusika. Kwa mujibu wa Leech (1969), kinaya hutumika kuongeza mvuto wa kifani, kusisitiza hisia na kuwasilisha ujumbe kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Katika muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba, waimbaji hutumia kinaya kama mbinu ya kimakusudi kuongeza uzito wa maana, kuchochea fikra na kuwasiliana kwa undani zaidi na wasikilizaji wao (Zahria na Wibowo, 2024).

4.2.5.4 Paradoksia

Kulingana na Leech (1969) paradoksia ni kauli au pendekezo ambalo, licha ya kuonekana kinzani au lenye utata, hufichua ukweli wa ndani au uliofichika.

Paradoksia hupinga mitazamo ya kawaida ya kufikiri. Huangazia migongano ya maisha au uzoefu wa mwanadamu ambao hauwezi kusuluhishwa kwa urahisi kupitia mawazo ya kawaida. Mkakati wa paradoksia umetumika katika muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba kama ifuatavyo:

Katika muziki **SY KIMB I UK 125;**

> *Ningwiwa muyo Kameneja, musasuko mwingi na raha., Ngasyoka ngavewa mulamu, ila ni stimu swakwa nyie, Nikyongete na ngavya ngwai, Nithuanite na andu me mikwa* - Ninafurahi mimi Kameneja, utamu mwingi na raha, ninarudi kuhisi mvuto, wakati niko na stimu zangu mimi, nikitafuna miraa na kuvuta bangi, sina hamu ya watu wenye kisirani. **UB I UK 125**

Katika ubeti huu mwimbaji anahusisha matumizi ya mihadarati na hali ya furaha na ustawi wa kihisia anaposema; "Ninafurahi mimi Kameneja, utamu mwingi na raha... Nikila miraa na kuvuta bangi, sina hamu ya watu wenye kisirani." Paradoksia inaibuka kutokana na ukweli kwamba licha ya mihadarati kutoa raha ya muda mfupi, inajulikana kuwa na madhara ya kiafya, kihisia na kijamii. Kwa hivyo, kauli kwamba mtu anaweza kupata furaha ya kweli au utulivu kupitia matumizi ya dawa za kulevya ni ya kiparadoksia na inapingana na ukweli unaokubalika kwa kawaida kuhusu athari za mihadarati. Paradoksia hii inaibua mvutano kati ya ustawi wa kweli na kuridhika kwa muda kwa njia za hatari. Inadhihirisha hali ya kutegemea vichocheo vya nje ili kupata furaha au kukwepa maumivu ya kijamii, jambo linaloonyesha mgogoro wa ndani wa mhusika. Inatumika kuibua tafakari ya kina kuhusu mapambano ya kisaikolojia yanayowakumba watu wanaojaribu kukwepa upweke au shinikizo la kijamii kupitia njia zisizo za kawaida. Kwa kutumia paradoksia, mwimbaji anafanikisha kuwasilisha hali halisi ya maisha kwa namna inayochochea tafakari za kina kuhusu furaha, utegemezi na kujitenga kijamii.

Katika muziki **GF KIMB IV UK 129** paradoksia inajitokeza ikatika ubeti huu;

> *Ngilasya niilye, ngethia ndiota na Mwende* - Huwa nimekaa, najipata nikiota na Mwende

Ngethe yi muingo Germany kweli ngewa kuiya - Msichana aliye ng'ambo Ujerumani kweli nahisi kulia **UB 1 UK 129**

Wiku muingo ngumisia muno we Mwende - Ukiwa huko ng'ambo nakukosa sana rohoni wewe Mwende

Ngakwatwa ni mutwe wauka na ku ngwone - Ninapatwa na wazo la kuja huko nikuone **UB 2 UK 130**

Katika beti hizi, mwimbaji anaeleza kwa hisia za kina hamu yake ya kumtembelea mpenzi wake Mwende aliye Ujerumani. Paradoksia inaibuka kupitia kuchanganya hali mbili zinazokinzana: ukaribu wa kihisia na umbali wa kijiografia. Mwimbaji anahisi uwepo wa Mwende kwa kina, anaota naye na anajawa na hisia za ukaribu, lakini kwa uhalisia wako mbali sana kwani mpenzi wake yuko ng'ambo, Ujerumani. Hii ni paradoksia kwa sababu mtu hawezi kimantiki kuwa karibu na mtu aliye mbali sana kimwili, lakini kihisia anaonekana kuwa karibu zaidi kuliko hali halisi inavyoruhusu. Paradoksia hii inaangazia mgongano kati ya matamanio ya kiroho au kihisia na vikwazo vya kimazingira, ikionyesha namna mapenzi yanavyoweza kushinda mipaka ya kijiografia. Kwa mujibu wa Suebpeng na wenzake (2020), paradoksia ni mbinu ya kimtindo inayoboresha kina cha ujumbe na mguso wa kihisia wa tungo. Kwa kuunganisha hali zinazopingana, upendo wa karibu dhidi ya umbali wa kimwili, mwimbaji anasisimua hisia za wasikilizaji na kuwahamasisha kutafakari juu ya maana halisi ya uhusiano wa mbali. Kwa hivyo, paradoksia hapa si tu njia ya kifani, bali ni chombo cha kueleza mapambano ya ndani ya mhusika na ugumu wa mapenzi ya mbali.

4.2.5.5 Tamathali za Usemi

Kulingana na Mulokozi (1989) tamathali za usemi ni kauli au tungo fupi za kisanaa zenye kubeba mafunzo au maana ya kijamii. Wanamuziki wa Benga wa jamii ya Wakamba wametumia tamathali za usemi kama inavyodhihirika kupitia mifano mbalimbali kutoka kwa nyimbo zao. Tamathali zilizotambuliwa katika sehemu hii zimefafanuliwa kwa kuzingatia muktadha ambao zimetumika ndani ya muziki wa Benga. Zifuatazo ni tamathali za usemi zinazojitokeza katika muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba;

Matumizi ya chuku: kulingana na Mbatia (2001) chuku ni matumizi ya lugha yenye kutilia chumvi kwa lengo la kukuza au kusisitiza jambo kupita kiasi. Wamitila (2008) anaeleza kwamba chuku hufanya sifa za kitu au mhusika kuonekana kupita kiasi na hivyo kumvutia msomaji au msikilizaji kwa uzito wa maelezo yanayotolewa. Hali hii huifanya chuku kuwa mbinu yenye mvuto wa kisanaa kwa kuwa huamsha hisia na kuongeza urembo wa kifasihi. Waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba wametumia mkakati huu. kwa mfano, katika muziki **WK KIMB V, UK 131** matumizi ya chuku ni dhahiri na yana lengo la kutoa maoni ya kijamii na kimaadili kuhusu tabia za mhusika anayekosolewa. Mwimbaji anatumia chuku kumkosoa mhusika kwa tabia zake zisizokubalika katika jamii anaposema;

> *Wakatimba nyie kweli nguseng'a ni tabia syaku* - Wakatimba mimi kweli nashangaa kwa tabia zako
>
> *Ona kutwika wi mwanake wi akili ndogo* - Hata ingawa wewe ni mrembo akili yako ni ndogo
>
> *Na ndinakuuma Wakatimba Kumbavu* -Na sijakutusi Wakatimba mpumbavu **UB 1, MSH 1,2 & 6 UK 131**

Hapa, neno "mpumbavu" linatumika kumtaja mhusika kwa dhihaka, likionyesha kutokubaliana na tabia zake. Aidha, mwandishi anaposema: "Hata ingawa wewe ni mrembo una akili ndogo,"anatumia chuku kumkosoa mhusika kwa kulinganisha uzuri wake na upungufu wa akili. Utafiti uliofanywa na Thiong'o na wenzake (2022) , ulibainisha kwamba wasanii hutumia vipengele vya kisanaa kama vile chuku kuwasilisha ujumbe wa kijamii na kimaadili kwa njia inyovutia na kuhamasisha wasikilizaji kutafakari kuhusu hali fulani katika jamii.

Matumizi ya tafsida: kwa mujibu wa Njogu na Chimera (1999), tafsida ni matumizi ya lugha safi na yenye staha ili kuepuka kutumia maneno yanayochukiza, machafu au ya kudhalilisha. Ni mbinu ya kutumia lugha isiyo ya moja kwa moja kutaja mambo ambayo ni mwiko, ya aibu au yenye kufedhehesha katika jamii. Waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba wametumia tafsida ili kupitisha ujumbe wao na kukwepa kuvunja miiko ya jamii hii.

Kwa mfano, tafsida imetumika katika muziki **WM KIMB III, UK 128** kama vile;

> *Na ndwi thoni nakuivia nginya* ***leu wa utuku*** - Hata hauna aibu nilikuwa nakulipia hadi **chakula cha usiku**. **UB 3 MSH 3 UK 129**

Mwimbaji ametumia maneno *"leu wa utuku*- chakula cha usiku*"* kumaanaisha kitendo cha ndoa ambacho ni mwiko kutajwa moja kwa moja kulingana na utamaduni wa jamii ya Wakamba. Maneno haya katika hali ya kawaida yana maana ya kushiriki kitendo cha ndoa. Vilevile katika wimbo huu mwimbaji ametumia tafsida anaposema maneno haya;

> *Uyasasya* ***nikuwaa maveti*** makuu - Unasema huwa **nabeba kinamama** wakongwe **UB 4, MSH 3 UK 129**

Mwimbaji ametumia maneno haya kumwonya rafiki yake anayemuharibia jina kwa kusema huwa anashiriki mapenzi na wanawake wakongwe waliomzidi umri. Katika jamii ya Wakamba mila haziruhusu watu wenye umri mdogo kufanya mapenzi na watu waliowazidi umri. Hivyo basi, mwimbaji anakwepa kulitaja jambo hilo moja kwa moja ili kuepuka fedheha na aibu. Msemo "*nikuwaa* - nabeba", una maana ya kushiriki au kuhusiana kimapenzi na wanawake wakongwe. Matokeo haya yanaungwa mkono na Muema (2019) anaposema kuwa waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba hutumia tafsida ili kukwepa lawama, kuepuka kupitisha jumbe tatanishi, kukwepa aibu na kuburudisha. Matokeo ya utafiti huu yanakubaliana na utafiti uliofanywa na Muema, kwani inadhihirika kuwa waimbaji katika miziki iliyochanganuliwa hapo juu wametumia tafsida kukwepa aibu na kuweka wazi jumbe zao. Kwa mujibu wa Leech (1969) tafsida hutumika kama chombo cha kimkakati ili kuepuka kuwaudhi wasikilizaji, kudumisha hisia za kijamii, kuunda athari ya kisanii au ya kifasihi, kuendeleza toni ya wimbo na kutii haki za mawasiliano ya umma. Maneno ya kitafsida huwasaidia wanamuziki kuwasilisha ujumbe wenye nguvu huku wakidhibiti athari za lugha ya jamii husika.

Matumizi ya sitiari: ni mbinu ya ulinganisho wa moja kwa moja bila kutumia vilinganishi. Ni mbinu ya kifasihi inayotumika kutoa ulinganifu au kulinganisha kati ya vitu viwili vilivyo tofauti kwa kutumia maneno ya picha, ili kuleta ufanisi katika kueleza wazo au hisia (Leech, 1969). Sitiari hutumika kuonyesha uhusiano wa kihisia au wa kimantiki kati ya vitu au hali tofauti. Sitiari huambatana na mitindo inayolenga kumvutia msikilizaji na kumsaidia kuelewa ujumbe wa kifasihi kwa undani zaidi.

Katika muziki **WM KIMB III 128** wake Alex Kasau sitiari inadhihirika ifuatavyo;

Kwanza, mada ya muziki huu "*Wasa **Mbili***- Rafiki **Kupe**" ni sitiari ambapo mwimbaji anamfananisha rafiki yake na kupe (*Wasa mbili*- Rafiki Kupe). Kupe ni mdudu anayevyonza damu kutoka kwa wanyama. Mwimbaji anamfananisha rafiki yake na kupe kwani anajifanya rafiki yake ili aweze kutumia pesa zake. Kwa mfano mwimbaji anasema katika sentensi hii;

> *"Ukanyonyaa tupesa twaka uteiwa nthoni* - Unatumia pesa zangu bila kuona aibu*."* **UB 1 MSH 3 UK 128**

Hapa mwimbaji analalamika jinsi rafiki yake amekuwa akifaidika kifedha kutoka kwake, ndiposa akamwita kupe.

Katika muziki **SY KIMB I UK 125** sitiari imetumika:

> *Imwe ndia na itathambaa, yienya **kiko muthekethi*** - Wengine wajinga na wasiozingatia usafi, **wachafu kama tarimbo UB 8 MSH 2 UK 126**

Katika kauli hii, mwimbaji anamfananisha mwanamuziki mwingine na 'tarimbo'. Tarimbo ni chuma kinachotumika kuchimbia mchangani. Kwa kawaida chuma hicho huwa kichafu kutokana na udongo. Kwa hivyo mwimbaji anatumia neno "*methekethi*-tarimbo" kueleza namna mwanamuziki huyo amekosa kuzingatia usafi wa mwili. Kutokana na wimbo huu mwimbaji anahimiza wanajamii kuwa ni vyema kuzingatia usafi wa mwili. Sitiari hutumika kuongeza ujumi na kuivutia hadhira. Vilevile hutumika kupitisha hisia zenye uzito.

Matumizi ya tashihisi: hii ni mbinu ya kitamathali ya kuvipa vitu visivyo uhai sifa za kibinadamu. Tashihisi imetumika katika muziki **MK KIMB II UK 127** ubeti ufuatao:

> *Munene wambiiye tukambeini* - Mkubwa uliniambia tupige kampeni
>
> *Nikenda **kivila kyuke kwitu*** - Ndiposa **kiti kije kwetu**
>
> *Munene wambiiye we ukanzuvia* - Mkubwa uliniambia utaniangalia

Oila ***kivila kiuka kwitu*** - Pindi tu **kiti kitakapokuja kwetu. UB 1 UK 127**

Katika muziki huu mwimbaji anakipa kiti sifa za kuwa na uhai anaposeama "kiti kije kwetu." Hii ina maana uongozi uje kwa jamii ya mwimbaji.

Pia, katika muziki **SY KIMB I UK 125** tashihisi inajitokeza ifuatavyo;

Stimu sya vangi kindingi, na milaa isilaa kimye - Stimu **za bangi, pombe na miraa zinafanana**

Iyisene na miambile, ***syendete vandu vatulisu*** - Hazijui kupiga mdomo, **hupenda mahali tulivu UB 2 MSH 2, 3 UK 125**

Katika muziki huu mwimbaji ameupa ulevi hisia za kibinadamu anaposema stimu za bangi, miraa na pombe hazijui kupiga mdomo, hupenda mahali tulivu. Tashihisi hii imetumika kusisitiza hisia zinazotokana na matumizi ya dawa za kulevya. Waimbaji hutumia tashihisi ili kuongeza ladha katika muziki wao na kuivutia hadhira. Leech (1969) anadokeza kuwa wasanii huweza kutumia tashihisi ili kuchochea hisia za hadhira lengwa, kuongeza maana na kuimarisha ustadi wao wa utunzi.

4.3 Ujumi Katika Muziki wa Benga wa Jamii ya Wakamba

Kwa mujibu wa Ponera (2014), ujumi ni neno lililotafsiriwa kutoka kwa neno la Kiingereza "aesthetics." Neno hili lilitumika kwa mara ya kwanza na Alexander Gottlieb Baumgarten mwaka wa 1735. Ujumi ni tawi la falsafa ambalo hushughulikia ubaya, uzuri, ladha, uhasi, ubora au urembo. Katika muktadha wa muziki, ujumi husaidia kuelewa namna vipengele vya sauti, mitindo ya uimbaji na mpangilio wa tungo vinavyochangia urembo na maana ya muziki. Kant (2000) anaeleza kuwa ujumi ni taaluma inayochunguza maamuzi ya ladha, ambayo huwa ya mtu binafsi lakini yanaweza kueleweka au kukubalika na watu wote. Alidokeza kwamba tunapohukumu kitu kuwa kizuri, tunakifurahia bila kutegemea faida yoyote binafsi, tunapendezwa na uzuri wake tu, si kwa sababu kina manufaa au kinaendana na maadili.

Dewey (1934) alisisitiza umuhimu wa uzoefu katika sanaa, akidai kuwa sanaa inapaswa kufahamika kama sehemu ya uzoefu wa binadamu (sanaa kama uzoefu). Aliuona ujumi kama taaluma inayotokana na mwingiliano kati ya kazi ya sanaa na mlengwa. Beardsley (1981) alipendekeza kuwa uzoefu wa kiujumi una sifa ya umoja,

nguvu za hisia na uzito wa kimaudhui, vinavyomwezesha msikilizaji au mtazamaji kutafakari kwa kina kazi ya sanaa. Thiong'o (1986) alisisitiza kuwa ujumi wa Kiafrika ni wa kiutendaji na wa kijamii unaotegemea sanaa simulizi na huambatana na maana za kimaadili, kiroho na kisiasa.

Leech (1969) anasema kuwa mawasiliano ya kiujumi ni mchakato ambao kazi ya sanaa huwasilisha maana ya kina zaidi kuliko ile ya mawasiliano ya kawaida. Mchakato huu wa kiujumi mara nyingi husababisha hisia na uelewekaji wa kazi ya sanaa kwa njia inayozidi mbinu za mawasiliano ya kawaida. Kwa mujibu wa Leech, ujumi sio tu kuhusu umbo au uzuri; unahusisha mwingiliano wa kina kati ya msanii, kazi ya sanaa na hadhira. Leech aliamini kuwa ujumi una uwezo wa kipekee wa kuwasilisha mawazo na hisia tata, ambazo huenda zisiweze kuelezeka kwa lugha ya kawaida. Nadharia ya umtindo inasisitiza mwingiliano kati ya msanii na hadhira, ikieleza kwamba thamani ya sanaa au ujumi imo katika uwezo wake wa kuwasilisha maana na kuamsha hisia za hadhira.

Kutokana na uchanganuzi uliofanywa katika lengo la kwanza ilibainika kwamba waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba wametumia mikakati mbalimbali ya kimtindo katika miziki yao. Sababu kuu inayofanya waimbaji hawa kutumia mikakati hiyo ni kuivutia hadhira kwa kuhahakisha mikakati hiyo imetumika kwa namna ya kiujumi. Waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba wameimarisha ujumi katika miziki yao kama ifuatavyo:

4.3.1 Ujumi wa Kihalisia

Ujumi wa kihalisia hurejelea mbinu za kisanaa zinazolenga kuonyesha maisha kama yalivyo, kwa kuzingatia uzoefu wa kila siku pamoja na hali halisi za kijamii na kibinadamu, bila kupotosha ukweli wala kutilia chumvi. Katika muktadha wa muziki, ujumi wa kihalisia hutumika kuonyesha hisia za kweli, kuangazia changamoto za maisha halisi na kuunda uhusiano wa karibu baina ya mwimbaji na wasikilizaji kwa kuakisi hali zao halisi. Kwa mujibu wa Eagleton (1990), uhalisia katika sanaa hulenga kuzalisha upya hali halisi ya uzoefu wa kawaida na kuufanya uwe na ukweli unaotambulika. Jambo hili huongeza uwezo wa kazi kueleweka kirahisi na kugusa hisia za hadhira. Ujumi wa kihalisia unajitokeza katika muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba kama ifuatavyo;

Katika muziki **SY KIMB I UK 125** katika ubeti ufuatao;

*Ni kwithiwa ni mura**sta**, na niishia kimra**sta*** - Kwa maana mimi ni mrasta, na huwa ninaishi kama mrasta

*Nikyongaa ta mura**sta**, ngakusya vangi ta mura**sta*** - Huwa natafuna miraa kama mrasta, na kuvuta bangi kama mrasta

*Sikala yakwa ni ro*sta, *inyusawa ni mura*sta - Sigara yangu ni rosta, huwa inavutwa na mrasta **UB 7 UK 126**

Katika ubeti huu ujumi wa kihalisia unaonekana wazi kupitia mtindo wa urari anaotumia mwimbaji. Kwanza, mwimbaji anaeleza maisha ya mtu wa kundi la "rasta" kwa kutumia lugha rahisi, ya moja kwa moja na inayojikita kwenye shughuli halisi kama vile kuishi, kutafuna miraa, kuvuta bangi na sigara. Hizi ni tabia na mitindo ya maisha inayotambulika na baadhi ya watu katika jamii, hivyo zinaakisi maisha ya kila siku bila mapambo wala kuficha uhalisia wa hali hizo. Kwa mujibu wa kanuni za ujumi wa uhalisia, kazi ya sanaa inapaswa kuonyesha hali halisi za jamii, wahusika wa ukweli na mazingira yanayofanana na yale ambayo wasikilizaji hukumbana nayo (Eagleton, 2008). Ubeti huu unatimiza hilo kwa kuonyesha wazi mtindo wa maisha ya mtu wa kundi la kijamii "rasta," na hivyo kuwawezesha wasikilizaji kuhusisha ujumbe huo na maisha halisi yanayowazunguka. Zaidi ya hayo, matumizi ya urari kama vile, urudiaji wa muundo wa kisarufi: "ni murasta… kimrasta… ta murasta... ni rosta… ni murasta," unatoa muundo wa ruwaza zinazoiga mzunguko wa maisha ya kila siku. Hili linaendana na maelezo ya Leech (1969) kwamba urari huweza kutumika kuonyesha mwendelezo wa maisha na kuongeza uhalisia kupitia mtiririko wa kisauti.

Pia ujumi wa kihalisia unajitokeza katika muziki **SM KIMB VIII UK 136** kama ifutavyo:

Kwakwa syo mbesa ti kindu, indi akaunti ni mbinge- Kwangu pesa si kitu, lakini akaunti zimefungwa

No nguutumia kindu kasweetie naku mbumiisye - Nitakutumia kitu kidogo mpenzi nivumilie **UB 4 MSH 1,2 UK 137**

Kauli hizi zinabainisha changamoto halisi za kifedha ambazo watu wa mjini hukumbana nazo. Msanii anatumia hali ya akaunti zilizofungwa kuonyesha matatizo ya kiuchumi kwa namna ya uhalisia unaoeleweka kwa hadhira.

> *Nikwoona TikTok nyie kana ngeeewa muleelo, na yuyu niende tuvange wikendi imwe tukomane-Huwa nakuona TikTok mtoto, naishiwa nguvu, na sasa nataka tupange wikendi moja tuonane*
>
> *Maneno haya sio mageni mjini, nikwatya nimukuelewa kina ngwasya, maneno haya sio mageni mjini tauni kuyingwa ndia andu yu nakyanuku-* Maneno haya sio mageni mjini, nina uhakika mnaelewa ninachokisema, maneno haya sio mageni mjini, mjini hakuna mjinga watu sasa wamechanuka.**UB 5 UK 137**

Katika ubeti huu (**UB 5**) mwimbaji anatumia mifumo halisi ya mahusiano ya kisasa, ikiwemo mitandao ya kijamii 'TikTok', kuonyesha mapenzi ya mjini. Huu ni ujumi wa kihalisia unaojikita katika maisha ya kila siku ya vijana wanaishi mjini. urudiaji wa kibwagizo *"maneno haya sio mageni mjini… mjini hakuna mjinga, watu sasa wamechanuka"* unajenga taswira ya jamii ambayo imeelimika na haiwezi kudanganywa. Hii ni kauli ya hekima ya kijamii inayotokana na hali halisi ya maisha ya mjini, ambapo watu wamepata ujuzi kutokana na uzoefu wa maisha.

Vilevile, muziki **WM KIMB III UK 128** neno "*mbili-* kupe" limetumika kistiari kufanananisha rafiki ya mwimbaji na tabia zake za kumtegemea mwimbaji. Neno hili linasababisha ujumi wa urafiki na kutia bidii pamoja na kujiepusha na uvivu. Kwa mfano katika ubeti huu;

> *We wasa ii kitindo kyaku ninakola* - Wewe rafiki urafiki wako sitaki
>
> *Kitumi nyie ndikwenda* ***utindanya na mbili*** - Kwa sababu sitaki **kuishi na kupe**
>
> *Unyonyae tupesa twakwa uteiwa nthoni* - Unatumia pesa zangu bila aibu **UB 1 MSH 1,2, 3 UK 128**

Ujumi wa uwajibikaji, kutia bidii na kuhasi uvivu unawakilishwa katika ubeti huu. Mwimbaji anaelekeza lawama kwa rafiki anayenyonya rasilimali zake bila kuchangia, akimtaja kuwa ni "kupe." Hili linajenga ujumi wa kihalisia kwa kutumia lugha ya moja kwa moja na taswira za maisha halisi ya utegemezi wa kijamii, hali inayojitokeza

miongoni mwa vijana wasiojituma kikazi. Aidha, ujumbe huu unaakisi ujumi wa kihalisia kupitia sauti ya upinzani dhidi ya uvivu na kuhimiza uwajibikaji na kujitegemea. Matokeo sawia yalibainika katika utafiti uliofanywa na Mutisya na Muhoro (2022) ulioonyesha kuwa nyimbo za michezo za watoto wa jamii ya Wakamba huhusisha maadili ya ujumi wa kihalisia kama vile, uwajibikaji, ufahamu wa mazingira, uhimizaji wa kutia bidii na kuhasi uvivu, urafiki na utamaduni. Matokeo haya yanaonyehsa kuwa nyimbo katika jamii ya Wakamba ni chombo muhimu cha kujenga ujumi na kupitisha maadili ya jamii.

Pia katika muziki **RN KIMB VI UK 132** ubeti huu;

> *Raha ndukauna kuma tene ndukauna* - Raha haitawahi saidia, kutoka zamani raha haisaidii
>
> *Tindikana nawo indi mwiso ukaiya* -Sukumana nayo lakini mwisho utalia
>
> *Maisha me muyo ta woona mbesa winasyo* - Maisha ni tamu, kwanza ukiwa na pesa
>
> *Indi nitheelaa ukakopa mbaka sya uya* - Lakini huwa zinaisha unakopa hadi za chakula
>
> *Starehe sya aka na kuteewa syi muyo* - Starehe za wanawake na kuuziwa zina ladha
>
> *Musaala waku wiminiwa baa ni aka*- Mshahara wako utamalizika kwenye klabu kwa wanawake
>
> *Na wathelelwa mayosa abiria ungi*- Na ukiishiwa wanachukua abiria mwingine,
>
> *Uilekelwa mbevo uithina ta kana ka ngya* - Unaachwa kwenye baridi na kuteseka kama mtoto wa maskini,
>
> *Ndwike masavu, ika masavu, eka uvitya masavu (uvundisye kusuvia mbesa syaku mwanake na uiyeka uyaa oou ta ngaange, ti mboneki*- Fanya hesabu, fanya hesabu, wacha kukosea hesabu (jifunze kudhibiti pesa

zako kijana na uachae kuzitumia hivyo kama ambazo zimekaangwa sio rahisi kuzipata) **UB 1 UK 133**

Ubeti huu unaakisi ujumi wa kihalisia kupitia uwasilishaji wa maisha halisi ya kijamii kwa kutumia lugha ya moja kwa moja, maudhui ya kila siku na hisia za kweli zinazotokana na hali za maisha. Katika ubeti huu, mwimbaji anazungumzia matatizo yanayotokana na maisha ya starehe kama vile matumizi mabaya ya pesa, anasa, ulevi, mahusiano ya kimapenzi ya muda mfupi na hali ya umaskini unaofuata. Lugha inayotumika ni ya kawaida, ikiwakilisha kwa uaminifu hali ambazo wasikilizaji wengi wanaweza kuzitambua au kuhusiana nazo. Matumizi ya kauli "*ukakop*a *mbaka sya uya*- unakopa hadi za chakula (MSH 4)" na "*uilekelwa mbevo uithina ta kana ka ngya*- unaachwa kwenye baridi na kuteseka kama mtoto wa maskini (MSH 8)" zinawasilisha uhalisia wa matatizo ya kiuchumi na kijamii yanayowakumba watu wa kawaida.

Vilevile, kibwagizo cha kejeli "fanya hesabu, fanya hesabu, wacha kukosea hesabu" kinawasilisha ujumbe wa tahadhari kwa njia ya kuchekesha lakini yenye uzito, hivyo kuchanganya uhalisia na mbinu za kisanaa. Ingawa kibwagizo hicho kinaweza kuonekana kama mchezo wa lugha kwa mtazamo wa ujumi wa kisasa, bado kinaendeleza dhamira ya ujumi wa kihalisia kwa kusisitiza umuhimu wa matumizi bora ya rasilimali, jambo ambalo ni sehemu ya maisha ya kila siku. Kwa mujibu wa Leech (1969) na Menninghaus na wenzake (2022), mikakati ya kimtindo huimarisha maana ya ujumbe huku ikitoa mvuto wa kisanaa unaobeba hisia za muktadha halisi wa kijamii. Hivyo basi, ubeti huu ni mfano bora wa matumizi ya ujumi wa kihalisia katika muziki wa Kiafrika wa kisasa kwa kuonyesha changamoto za kijamii kupitia lugha ya wazi na taswira halisi za maisha.

4.3.2 Ujumi wa Kigothiki

Kwa mujibu wa Byron & Townshend (2014) neno gothiki linarejelea mtindo au aina ya kazi ya sanaa inayohusisha vipengele vya giza, mafumbo, hofu na mambo ya ajabu yasiyo ya kawaida. Istilahi hii hutumika katika fasihi na sanaa kuonyesha mazingira ya kutisha, hisia kali kupita kiasi na maudhui ya ajabu kama vile mizimu na kifo. Vipengele vya kigothiki mara nyingi hutumika kuchunguza matamanio yaliyofichwa, wasiwasi wa kijamii, au mmomonyoko wa maadili, hivyo kuviwezesha kuwa nyenzo zenye nguvu katika kuwasilisha maana ya kimafumbo na kina cha kisaikolojia katika

fasihi (Byron na Townshend, 2014). Katika utafiti huu ujumi wa kigothiki umeimarishwa ifuatavyo;

Kwa mfano, kibwagizo cha beti za muziki **RN KIMB VI UK 132**;

> *Ndwike masavu, ika masavu, eka uvitya masavu* - Fanya hesabu, fanya hesabu, wacha kukosea hesabu. **UK 133**

Kurudiwa kwa onyo hili kunawasilisha hisia nzito za kijamii. Jamii inaonywa dhidi ya ubadhirifu wa pesa na kuzingatia matumizi mwafaka. Mtindo huu unaibua ujumi wa kigothiki kwa kuunda mazingira ya hofu, tahadhari na hali ya hatari inayotokana na uharibifu wa maadili na kuporomoka kwa utu wa binadamu ndani ya maisha ya kila siku ya kukosa fedha au kushindwa kiuchumi. Kwa mujibu wa Bradley (2018), ujumi wa kigothiki hujitokeza pale ambapo hali ya kawaida ya maisha huonyeshwa ikidorora kuelekea maangamizi ya kiakili au kijamii, jambo linaloonekana wazi katika kibwagizo hiki. Onyo hili halihusu tu udhibiti wa fedha, bali pia linaashiria hatari ya mtu kupoteza mwelekeo wa kimaadili na kijamii. Kwa hivyo, inajenga muktadha wa kihisia unaoendana na mvutano kati ya udhibiti wa mantiki na kuporomoka kwa hali ya kawaida, mojawapo ya viini vya ujumi wa kigothiki kwa mujibu wa (Spooner, 2007).

Vilevile katika muziki **SM KIMB VIII UK 136** ubeti ufuatao:

> *Ve syindu ngwatie kwona Anita ngavewa kyeva*- Kuna mambo ninayoyaona , Anita kweli nahisi huruma,
>
> *Nayuyu mbangie niwete, ula ukumena amene yu*- Na sasa nimeamua kuyasema, atakaye nichukia anichukie
>
> *Maneno haya sio mageni mjini, nikwatya nimukuelewa kila ngwasya, maneno haya sio mageni mjini tauni kuyingwa ndia andu yu nakyanuku*.-Maneno haya sio mageni mjini, nina uhakika mnaelewa ninachokisema, maneno haya sio mageni mjini, mjini hakuna mjinga watu sasa wamechanuka.**UB 1 UK 136**

Ubeti huu unaonyesha wasiwasi na msukumo wa kihisia. Kauli “kuna mambo ninayoyaona, Anita kweli nahisi huruma, na sasa nimeamua kuyasema, atakaye

nichukia na anichukie" inaomnyesha hisia kali za kusikitisha zinzzomsukuma mwimbaji. Wasiwasi wa mambo kutendewa visivyo na msongo wa ndani ni dhihirisho la kigothiki, ambapo nafsi hujipata ikikabiliwa na mapambano ya ndani, hofu ya upweke na hukumu ya jamii.

Uradidi wa kibagizo cha beti za muziki huu **(SM)** "*maneno haya sio mageni mjini...*" umetumika kama kiashiria cha mafumbo ya kijamii. Marudio haya yanabeba uzito wa kifasihi wa kigothiki: yanafanya muziki uwe na sauti ya kinabii inayotoa onyo kuhusu hali ya jamii, kwa namna ya fumbo linalotisha.

Pia katika muziki huu **SM KIMB VII UK 136:**

> *Nienda twose kalumu kasweetie naku tutundume, no tukome utuku muima mbevi ndakwitya-* Nataka tuchukue chumba, mpenzi tuzungumze, tunaweza kulala usiku mzima **UB 5 MSH 1,2 UK 137**
>
> *Nikwoona TikTok nyie kana ngakwatwa ni muleleo-* huwa nakuona TikTok mtoto naishiwa nguvu
>
> *Na yuyu niende tuvange wikendi imwe tukomane* – Na sasa nataka tupange wikendi moja tupatane **UB 6 MSH 1,2 UK 137**

Kauli kama *"Nataka tuchukue chumba, mpenzi tuzungumze, tunaweza kulala usiku mzima"* au *"Huwa nakuona TikTok mtoto, naishiwa nguvu"* zinaibua matamanio ya mwili na mapenzi yaliyofichwa. Katika mtazamo wa kigothiki, matamanio haya yanaweza kuonekana kama nguvu za giza zinazoweza kupelekea mmomonyoko wa maadili au hofu ya jamii kuhusu mabadiliko ya mienendo ya vijana.

Ujumi wa kigothiki pia unajitokeza katika muziki **WK KIMB V UK 131**. Katika ubeti huu;

> *Wakatimba nyie kweli nguseng'a ni tabia syaku* - Wakatimba mimi kweli nashangaa kwa tabia zako
>
> *Ona kutwika wi mwanake wi akili ndogo* - Hata ingawa wewe ni mrembo una akili ndogo

Muvaile waku ni ukengana wi mundu wa vata - Mavazi yako yanaweza kudanganya kuwa wewe ni mtu wa maana

Indi malondu maku we ve amwe me kithekani - Lakini bado wapo kondoo wako walio kichakani

Niona wi ndia Wakatimba wi mana - Naona ukiwa mjinga Wakatimba wewe ni bure

Na ndinakuuma Wakatimba kumbavu - Na sijakutusi Wakatimba mpumbavu **UB 1 UK 131**

Urudiaji wa maneno kama "*kumbavu* – mpumbavu" pamoja na kauli za kudhalilisha kama "*niona wi ndia* - naona ukiwa mjinga" zinaonyesha namna lugha inavyotumika kama chombo cha kutoa hukumu kali na kuibua muktadha wa maumivu ya kihisia. Maneno haya, ingawa si ya kitafsida, yana mvuto wa kimakabiliano kwa kuwa yanatoka nje ya mawasiliano ya kawaida na yanahusisha mashambulizi ya moja kwa moja dhidi ya utu wa mhusika. Kwa mujibu wa Bradley (2018), vipengele vya kigothiki hujengwa kupitia hisia za uwoga na hali ya kuvunjika kwa maadili, ambavyo vyote vinaonekana bayana katika ubeti huu. Lugha isiyo ya kitafsida inayotumika hapa haitumiki tu kwa lengo la kukemea, bali pia inawasilisha hali ya kihisia iliyochafuka ambayo inaweza kuibua huzuni au mshtuko kwa upande wa msikilizaji. Kwa njia hii, ujumi wa kigothiki huchangia kuongeza mvuto wa kazi ya sanaa kwa kuimarisha kina cha kisaikolojia na dhamira ya kuhoji maadili na tabia za kijamii. Kwa hivyo, aina hii ya ujumi huibua tafakari za kina kuhusu hali ya maisha ya binadamu na jamii inayomzunguka.

4.3.3 Ujumi wa Kimapenzi

Ujumi wa kimapenzi ni mtindo wa kisanaa unaolenga kuonyesha hisia za ndani za mtu, uzoefu wa kibinafsi, ubunifu wa fikra na uzuri wa mazingira ya asili au mambo ya kushangaza yenye mvuto. Mtindo huu hujitokeza kama njia ya kupinga sanaa za zamani zilizozingatia mantiki na kanuni zisizobadilika (Berlin, 1999). Katika muziki, ujumi huu huonekana wazi kupitia mbinu za kisanaa kama vile kutumia maneno yenye hisia kali, kueleza mapenzi au uchungu wa moyo, kutumia taswira za uzuri wa kiasili na kurudia maneno ili kusisitiza hisia. Ujumi wa kimapenzi huweza

kujidhihirisha kupitia miundo mirefu ya sentensi iliyojaa hisia, ikionyesha ubinafsi wa hali ya juu na maonyesho ya kina ya uzuri (Abrams, 1999; Fitzgerald, 2010). Hili linajitokeza katika muziki **RN KIMB VI UK 132** ambapo mwimbaji anatumia sentensi tongole ifuatayo;

> *Woona wesa uvitya masavu ukatheelawa kitimba ni syana wakua ukomete valanda wa nyumba, nundu waiye mbesa ta ngaange* - Utakapokosea hesabu utapigwa mateke kiunoni na watoto ukizeeka ukiwa umelala ferada mwa nyumba, kwa sababu ulikula pesa kama ambazo zimekaangwa **UB 4 MSH 6 UK 134**

Katika sentensi hii ujumi wa kimapenzi unaibuka kwa njia yenye nguvu kupitia matumizi ya sentensi ndefu iliyojaa hisia, ambayo ni kiashiria muhimu cha mtindo huu wa ujumi kama inavyobainishwa na (Abrams, 1999; Fitzgerald 2010). Kupitia sentensi kama:

> "Utakapokosea hesabu utapigwa mateke kiunoni na watoto ukizeeka ukiwa umelala ferada wa nyumba, kwa sababu ulikula pesa kama ambazo zimekaangwa..." **MSH 6**

Katika dondoo hili, mwimbaji anajenga picha ya adhabu na fedheha anayoweza kupata mtu anayekosea katika maisha yake. Kauli *"utapigwa mateke kiunoni na watoto ukizeeka ukiwa umelala ferada mwa nyumba"* inaunda taswira ya udhalilishaji na mateso ya kimwili na kisaikolojia, huku *"ulikula pesa kama ambazo zimekaangwa"* ikionyesha maisha ya anasa na upotovu. Picha hii inazua hisia za maumivu ya ndani, majuto makali na huzuni, hali inayomfanya mhusika ajitazame upya kwa mtazamo wa kujilaumu. Hali hii ndiyo inaunda kiini cha ujumi wa kimapenzi kwa kuonyesha mgongano wa hisia kati ya furaha ya anasa za awali na uchungu wa majuto baadaye. Sentensi hii inamwongoza msikilizaji kupitia hisia za majuto, huzuni na uhalisia wa maisha. Inaeleza jinsi mtu anavyoweza kuangamia kijamii na kifamilia kwa sababu ya matumizi mabaya ya fedha. Zaidi ya hayo, matumizi ya taswira ya "kupigwa mateke na watoto ukiwa umelala kwenye ferada mwa nyumba," yanamfanya msikilizaji atafakari hali ya mtu aliyetelekezwa, ambayo ina ladha ya uzuri wa huzuni. Pia kuna hisia za kupoteza utu, za mtu anayeanguka

kutoka hali ya heshima hadi unyonge wa mwisho, jambo linaloibua hisia za huruma. Kwa hivyo, kupitia ujenzi wa sentensi ndefu yenye hisia nzito na picha inayochochea fikra za kina juu ya maisha na maadili, mwimbaji anadhihirisha wazi ujumi wa kimapenzi.

Katika muziki **GF KIMB IV UK 129** mwimbaji ametumia picha za vitu halisi kumleta msikiliziji katika ulimwengu wake wa kihisia. Kwa mfano taswira za umbali na safari zinajitokeza katika sentessi hizi;

> *Nieendaa airport mbangite nyie ulisa ndeke* - Huwa ninaenda katika uwanja wa ndege nikiwa na mpango wa kuabiri ndege **UB 3 MSH 1 UK 130**
>
> *Ngesilya ivitha nilise meli Mombasa kuu* - Nafikiria kujificha niabiri meli huko Mombasa **UB 4 MSH 1 UK 130**

Sentensi hizi zinajenga taswira ya safari ya mwimbaji na vikwazo anazokabiliana nazo anapojitayarisha kumtembelea mpenzi wake. Vilevile safari ya mwimbaji kwenda Ujerumani inaonyesha taswira ya umbali wa kihisia uliopo baina yake na mpenzi wake. Mishororo hii inaonyesha ujumi wa kimapenzi kwa kuonyesha hisia za ndani za mwimbaji zinazomsukuma kufanya juhudi za kumtembelea mpenziwe.

4.3.4 Ujumi wa Kitamaduni

Ujumi wa kitamaduni huhusu mikakati ya kisanaa inayoakisi na kuwasilisha maadili, utambulisho na tajriba za jamii fulani. Eagleton (1990) na Thiong'o (1986) wanasisitiza kuwa ujumi wa kitamaduni umefungamana kwa kina na itikadi pamoja na utambulisho wajamii. Katika muziki, ujumi wa kitamaduni huimarishwa kupitia matumizi ya lugha za asili, ala za kitamaduni, mitindo ya uigizaji na uimbaji pamoja na maudhui yanayoshabihiana na maadili ya kijamii na hali halisi ya maisha (Finnegan, 1970; Turino, 2000). Waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba wameimarisha ujumi huu kama ifuatavyo;

Katika muziki **SY KIMB I UK 125** tazama sentensi zifuatazo;

> *Ndinenenaa na andu mwanake, ndakyongete ni mutavye* - Huwa sizungumzi na watu mimi, kama sijatafuna miraa **UB 4 MSH 1 UK 125**

> *Matesi ni mundu vathei, Matenzawa ngesa utema* - Huwa hawajui mimi ni bure, Matenzawa nisipotafuna miraa **UB 3 MSH 3 UK 125**

Ujumi wa kitamaduni unaojitokeza katika muziki huu unaeleweka kupitia matumizi ya lugha na maudhui yanayoakisi maisha halisi ya jamii ya mwimbaji. Sentensi hizi, zimetumia mkakati wa ukiushi ambao unavunja kanuni za kisarufi za lugha ya Kikamba, hasa kwa kuingiza neno la Kiswahili "miraa." Hili linaibua ujumi wa kitamaduni kwa sababu linaakisi matumizi ya lugha inayotokana na mwingiliano wa maisha ya kisasa na utamaduni asilia.

Mwimbaji ametumia neno *miraa* kama dhana inayotambulika kijamii ili kuonyesha tabia inayofungamana na utamaduni wa jamii yake. Miraa hapa sio mmea wa kawaida, bali ni kiwakilishi cha tabia, mienendo na mitazamo inayotambuliwa na jamii ya mwimbaji. Kwa hivyo, sentensi hizi zinadhihirisha namna mwimbaji anavyojitambulisha kama mshiriki halisi wa jamii yake, kueleza hali zake za kiakili, kijamii na kitamaduni kupitia matumizi ya neno "miraa" kama kitambulisho cha maisha yake ya kila siku. Kwa njia hii, muziki huu hauwasilishi tu ujumbe wa kibinafsi, bali unatoa nafasi ya msikilizaji kutambua na kuhusiana na mazingira ya kitamaduni ya mwimbaji. Ujumi huu unatoa taswira ya kijamii inayohusisha matumizi ya lugha mseto na tabia ya kijamii kama vile kutafuna miraa.

Katika muziki **RN KIMB VII UK 132** ujumi wa kitamaduni umeimarishwa kupitia matumizi ya mikakati ifuatayo;

> *Ivundisye kusuvia mbesa syaku mwanake na uiyeka uya oou ta ngaange*- Jifunze kutunza pesa zako kijana, na uache kuzitumia hivyo kama ambazo zimekaangwa **UB 1 MSH 12 UK 133**
>
> *Na wathelelwa mayosa abiria ungi, Uilekelwa mbevo uithina ta kana ka ngya* - Na ukiishiwa wanachukua abiria mwingine, Unaachwa kwenye baridi na kuteseka kama mtoto wa maskini **UB 1 MSH 7, 8 UK 133**

Ujumi wa kitamaduni katika muziki huu umeimarishwa kupitia matumizi ya misemo isiyo ya kawaida, ya kejeli na yenye taswira ili kuvutia hisia na fikra za msikilizaji.

Kauli kama, *"Ivundisye kusuvia mbesa syaku mwanake na uiyeka uyaa oou ta ngaange* **UB 1 MSH 12***"* na *"Uilekelwa mbevo uithina ta kana ka ngya* **UB 1 MSH 7, 8***"* ni mifano ya matumizi ya sitiari na lugha ya taswira inayochanganya uhalisia wa maisha ya kijamii na uzito wa kitamaduni. Misemo hii inavunja matumizi ya lugha ya moja kwa moja kwa kutumia lugha ya picha na kejeli ambayo inahusishwa na maisha ya kawaida ya jamii ya Wakamba. Kwa mfano, tashbihi ya "kutumia pesa kama ambazo zimekaangwa" inawasilisha dhana ya ubadhirifu kwa njia ya kuchekesha lakini yenye ujumbe mzito ilhali "kuachwa kwa baridi kama mtoto wa maskini" inasisitiza hatari ya kutokuwa na mipango au uangalifu wa kifedha. Mikakati hii imetumika kuimarisha ujumi wa kitamaduni kwa kuonyesha maisha halisi, tabia na changamoto zinazokumba vijana na wanajamii kwa ujumla. Kwa hivyo, ujumi huu unafanya muziki huu kuwa sio tu kwa ajili ya burudani, bali pia chombo cha mafunzo, maonyo ya kijamii na uhifadhi wa utamaduni wa jamii. Matokeo haya yanalingana na madai ya Barber (1987), kwamba lugha ya kisanii inayotumika katika muziki huchanganya burudani na mafundisho ya kijamii ili kuufanya muziki kuwa chombo madhubuti cha kufundisha, kuonya na kuendeleza utamaduni.

Muziki **RN KIMB VII UK 132** tazama mishororo ifuatayo;

> *Raha Ndukauna Kuma Tene Ndukauna, Tindikana nawo indi mwiso ukaiya* - Raha haitawahi saidia, kutoka zamani raha haisaidii, Sukumana nayo lakini mwisho utalia. **UB 1 MSH 1 UK 133**

Mishororo "raha haitawahi saidia, kutoka zamani raha haisaidii, sukumana nayo lakini mwisho utalia" unaakisi maadili ya jamii ya Wakamba kuhusu umuhimu wa kujizuia, kuwajibika na kutafakari athari za matendo ya muda mfupi. Hapa, ujumi huu wa kitamaduni umejengwa kupitia ukinzani kati ya raha ya muda mfupi na mateso ya baadaye. Hali hii inaibua falsafa ya maisha inayosisitiza busara, nidhamu na utunzaji wa rasilimali kwa mustakabali bora. Matokeo haya yanaonyesha namna muziki unavyotumika kama chombo cha kuendeleza na kueneza maadili ya kijamii, hasa yale yanayohimiza uwajibikaji. Kwa hivyo, muziki huu hauwasilishi tu ujumbe wa kihisia bali umebeba maadili ya kijadi yanayowiana na mitazamo ya jamii kuhusu maisha bora na yenye heshima. Matokeo haya yanakubaliana na hoja ya Thiong'o (1986) anayesisitiza kuwa kazi za kisanaa zinapaswa kufungamana na maisha ya jamii na

kuwa sehemu ya mchakato wa jamii kwa kuendeleza maadili na uelewa wa hali halisi. Aidha, Finnegan (1970) anaeleza kuwa wasnii katika fasihi simulizi, wakiwemo waimbaji na washairi wa jamii za Kiafrika, hutumia lugha ya kinathari na ushairi kuhamasisha tabia njema, nidhamu na kuonya dhidi ya matendo yanayoweza kuhatarisha maisha ya mtu au jamii.

Kwa hivyo, kama inavyobainishwa na watafiti hawa, muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba unatumika kama chombo cha mafunzo ya kijamii na utamaduni. Ujumi wa kitamaduni katika muziki huu unahimiza maadili kama vile uwajibikaji, heshima na maisha yenye mwelekeo wa kiutu.

4.3.5 Ujumi wa Kiishara

Ujumi wa kiishara katika muziki unahusisha matumizi ya lugha ya ishara na sitiari ili kuibua hisia badala ya kupitisha ujumbe kwa njia ya moja kwa moja au ya wazi. Mtindo huu humwezesha msikilizaji kupata maana kupitia taswira za kisanaa, toni ya sauti na tamathali za usemi kama zinavyotumika katika tungo. Kama wanavyoeleza Balakian (1967), Fisher (2015) na Hatten (2018), hali ya utata na kutoeleza jambo moja kwa moja, ni kiini cha ujumi huu. Jambo hili huwezesha msikilizaji kushiriki kihisia kwa undani zaidi. Kama anavyoeleza Finnegan (1970), matumizi ya lugha ya ishara katika kazi za fasihi ya Kiafrika kama vile sitiari na methali huwezesha kupitisha maana tata za kijamii. Katika muziki wa Benga ujumi wa kiishara umeimarishwa kupitia mitindo mbalimbali. Kwa mfano;

Katika muziki **RN KIMB VII UK 132** mwimbaji ametumia sentensi zifuatazo za kisitiari na tashbihi;

> "*Ivundisye kusuvia mbesa syaku mwanake na uiyeka uyaa oou ta ngaange, ti mboneki* - Jifunze kutunza pesa zako kijana, na uache kuzitumia hivyo kama ambazo zimekaangwa, si rahisi kupatikana" **UB 1 MSH 12 UK 133**
>
> "*Uilekelwa mbevo uithina ta kana ka ngya* - Unaachwa kwa baridi na kuteseka kama mtoto wa maskini" **UB 1 MSH 8 UK 133**

Katika mishororo hii, ujumi wa kiishara unajitokeza kupitia matumizi ya sitiari na tashbihi, ambazo zimetumika kuibua hisia na kuchochea tafakari za msikilizaji badala ya kueleza maana kwa njia ya moja kwa moja. Mshororo *"Ivundisye kusuvia mbesa syaku mwanake na uiyeka uyaa oou ta ngaange, ti mboneki*- Jifunze kutunza pesa zako kijana, na uache kuzitumia hivyo kama ambazo zimekaangwa, si rahisi kupatikana,*"* unalinganisha ubadhirifu wa pesa na kuzitumia kama chakula kilichokaangwa, tamathali inayojenga picha yenye nguvu kuhusu matumizi ya fedha yasiyo ya busara. Hii ni sitiari yenye uzito wa kihisia inayosababisha msikilizaji afikirie kwa kina kuhusu madhara ya kifedha. Vilevile, katika mshororo *"Uilekelwa mbevo uithina ta kana ka ngya"*, tashbihi ya kuteseka kama mtoto wa maskini inaibua huruma na huzuni, ikionyesha matokeo ya kuishi bila kuwajibika kifedha. Matokeo haya yanaakisi maoni ya Grensideng na wenzake (2023) wanaoeleza kuwa lugha ya kitamathali katika nyimbo huunda picha za kudumu katika akili za wasikilizaji na kuchochea mwitikio wa kihisia. Vilevile, Leech (1969) anasisitiza kuwa lugha ya ishara hutumika na waimbaji kuibua hisia, kuongeza mvuto wa kisanaa na kufikisha ujumbe kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Kiini cha ujumi wa kiishara ni kutumia lugha ya picha na ishara ili kufikisha maana fiche, kuamsha hisia na kuhimiza tafakari za kina. Kwa hivyo ujumi wa kiishara katika muziki huu unahimiza uwajibikaji wa matumizi ya rasilimali kwa njia inayovutia wasikilizaji.

Pia, katika muziki **WM KIMB III UK 128;**

> *Unyonyae tupesa twakwa uteiwa nthoni* – Unatumia pesa zangu bila aibu **UB 1 MSH 3 UK 128**
>
> *Uwasa uu wonyoonyaa ndienda kisinga* **-** Urafiki huu wa kuninyonya sitaki Kisinga **UB 4 MSH 4 UK 129**
>
> *Nisuvia iveti syaku ndeiwa ngalama...na ndwi thoni nakuivia nginya leu wa utuku- huwa* **-** Nawasaidia wanawake wako bila kuhisi gharama…. na hauna aibu nilikuwa nakulipia hadi chakula cha usiku **UB 3 MSH I,3 UK 129**
>
> *Twataanisya uilika tulavu Mukuru, Uyambiiya uzambasya uivoya kimee* – Tukiachana unaingia vilabu

vya Mukuru, unaanza kunidhalilisha ukiomba pombe

UB 4 MSH 1,2 UK 129

Katika muziki huu, ishara mbalimbali zimejengewa ndani ya lugha ya maumivu, kejeli na unyonyaji ili kufikisha ujumbe kuhusu urafiki wa kijamii unaolenga maslahi ya upande mmoja. Kauli kama: *"unyonyae tupesa twakwa uteiwa nthoni* - Unatumia pesa zangu bila aibu na *Uwasa uu wonyoonyaa ndienda kisinga* - Urafiki huu wa kuninyonya sitaki Kisinga," zinafichua dhana ya unyonyaji na usaliti lakini si kwa njia ya lawama ya moja kwa moja, bali kupitia mfumo wa picha na kinaya. Pia, kauli kama "*Nisuvia iveti syaku ndeiwa ngalama, na ndwi thoni nakuivia nginya leu wa utuku* - Nawasaidia wanawake wako bila kuhisi gharama, na hauna aibu nilikuwa nakulipia hadi chakula cha usiku" zinaonyesha ishara ya gharama kama picha ya mzigo wa kihisia na kifedha alionao mwimbaji. Hili linaashiria mgongano wa matarajio na uhalisia ambapo mwimbaji amechoshwa na mahusiano ya upande mmoja. Aidha, taswira ya mwimbaji kuwafadhili wanawake wa rafiki yake kwa kuwanunulia pombe na chakula, ni ishara ya unyonge na imetumika kisitiari kuonyesha jinsi mwimbiji anavyonyanyaswa bila shukrani. Kauli "Twataanisya *uilika tulavu Mukuru uyambiiya uzambasya uivoya kimee* - Tukiachana unaingia vilabu vya Mukuru unaanza kunidhalilisha ukiomba pombe," inaonyesha namna jina la mwimbaji linavyopakwa tope katika maeneo ya vileo. Jambo hili ni ishara ya fedheha na usaliti wa urafiki. Ujumi wa kiishara katika muziki huu umejengwa kupitia lugha ya picha, sitiari na urudiaji wa maudhui ili kuwasilisha ujumbe wa kuchoshwa na mahusiano ya kirafiki yasiyo na usawa. Msanii anawakilisha hisia za kuchoshwa, kuumizwa na kuamua kuvunja urafiki kwa njia inayoibua hisia za kutafakari na kuelewa undani wa mateso ya urafiki huo. Hivyo basi, muziki huu umetumia ujumi wa kiishara kuwasilisha uzoefu wa kibinafsi kwa njia inayovutia na kutoa nafasi ya ufasiri mpana wa kijamii.

4.3.6 Ujumi wa Kisiasa

Ujumi wa kisiasa hurejelea namna kazi za kisanaa hutumia mbinu za kitamathali kama vile, sitiari, tashbihi na taswira kuwasilisha mijadala ya kisiasa, maoni ya kijamii, au msimamo wa kisiasa, kwa njia ya kiubunifu inayovutia hadhira na kuibua tafakari. Kwa mujibu wa Rancière (2004), ujumi wa kisiasa ni njia ya kusawiri au kupinga mamlaka, ukandamizaji, au ahadi za uongo kupitia mbinu za kisanii. Muziki, kama anavyobainisha Street (2013), ni jukwaa la kipekee la kueleza maumivu, matarajio na

usaliti wa kisiasa kwa njia ya hisia na lugha ya sanaa. Ujumi huu umeimarishwa katika muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba kama ifuatavyo;

Katika muziki wa Benga, ujumi wa kisiasa umebainika kupitia matumizi ya maswali ya balagha, lugha ya hisia, sitiari na urudiaji, unaowasilisha hali ya kukatishwa tamaa na usaliti wa kisiasa. Kwa mfano katika mshororo huu;

> *Ninguseng'a na ngikulya ii munene we kowolilwe* - Ninashangaa na kuuliza, mkubwa kwani ulisahau? **MK KIMB II UK 127** (kibwagizo)

Mshororo huu unaorudiwa mwishoni mwa kila ubeti unadhihirisha masikitiko ya wananchi waliojitolea katika kampeni kwa matumaini ya kuboresha hali yao, lakini walipata kutelekezwa baada ya kiongozi kupata mamlaka.

Vilevile katika muziki huu **MK KIMB II UK 127**,

> *Kivila niwoosie na nyie ndwanzuvia* - Kiti ulichukua na mimi haunitunzi **UB 1 MSH 5 UK 127**
>
> *Navoyaa ngai mwa autetheye* - Nilimwomba mungu angalau akusaidie **UB 2 MSH 1 UK 127**
>
> *Unene ni twosie nanotukuthinaa* - Tuliuchukua lakini bado tuko na shida **UB 2 MSH 6 UK 127**
>
> *Ningutulya ndu na kwita uekeo* - Ninapiga magoti na kuomba msamaha **UB 3 MSH 1 UK 128**

Sentensi hizi zinatilia mkazo usaliti wa kisiasa, ambapo mwananchi ananyimwa matunda ya ushindi alioupigania. Ubeti wa pili unadokeza wazi hali ya imani na matumaini: "Nilimwomba naomba Mungu angalau akusaidie... lakini bado tuko na shida", kauli hii inaonyesha namna siasa zinavyotumika kama chombo cha matumaini ya mabadiliko, lakini baadaye matumaini haya yanageuka kuwa chimbuko la maumivu. Katika ubeti wa tatu, kwa kutumia lugha ya unyenyekevu kama *"napiga magoti na kuomba msamaha"*, unaibua picha ya mnyonge anayeomba rehema mbele ya kiongozi aliyemtelekeza, hali inayoonyesha mgawanyiko wa nguvu za kijamii kati ya viongozi na wananchi.

Ujumi wa kisiasa katika muziki huu umeimarishwa kupitia matumizi ya lugha ya maumivu na kejeli ili kuwasilisha mivutano ya mamlaka, hali ya kupuuzwa kwa wananchi na usaliti wa kisiasa. Muziki huu hauwasilishi tu hisia za msanii, bali ni sauti ya walio wengi na waliokatishwa tamaa. Matokeo haya yanaendana na hoja ya Street (2013) kuwa muziki una uwezo wa kipekee wa kuunganisha hisia za binafsi, hali za kisiasa na kuibua hoja nzito kwa njia ya kisanaa.

4.4 Athari Lengwa za Matumizi ya Mikakati ya Kimtindo

Kulingana na Leech (1969) mikakati mbalimbali ya kiisimu na vipengele vya kimtindo hutumika kuleta athari maalum kwa hadhira. Leech (1969) anafafanua athari lengwa kama matumizi ya kimakusudi ya lugha. Mikakati ya kimtindo wanayotumia waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba hulenga kuleta athari mbalimbali katika jamii. Hapa tunaangazia jinsi uchaguzi wa lugha unavyoweza kuathiri mawasiliano na kuunda athari maalum kwa wasikilizaji. Baadhi ya athari wanazolenga waimbaji wa muziki huu ni pamoja na:

4.4.1 Uwasilishaji wa Masuala ya Wanawake

Waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba wametumia vipengele vya kimtindo kumchora mwanamke kwa namna mbalimbali. Kwa mfano katika muziki **WK KIMB V UK 131,** neno 'Wakatimba' katika mada ya muziki huu; "*Wakatimba Kumbavu* - Wakatimba Mpumbavu" limetumika kimajazi. Ni neno lenye maana ya sehemu ya mwili, makalio katika jamii ya Wakamba. Mwimbaji amelitumia kumkejeli na kumdunisha mhusika. Neno hili hutumika katika jamii ya Wakamba kumaanisha mtu asiyekuwa na adabu. Hivyo neno hilo limetumika kumchora mwanamke kama mtu asiyekuwa na tabia za kupendeza katika jamii. Kwa mfano, mhusika katika wimbo huu ana tabia zisizopendeza kama vile, kujifungua na kutupa mtoto kwenye mtaro, kuolewa na kuacha ndoa yake na kuingililia tabia za usherati katika eneo la Mlolongo. Haya yanapatika katika ubeti ufuatao mishororo iliyokolezwa;

> *Hivi majusi inataviwe lipoti ng'asenga* - Hivi majuzi nilipewa ripoti nikashangaa
>
> ***Unaimutwae Pipeline ni nzamba ya mwako* - Ulikuwa umeolewa Pipeline na jamaa wa mjengo**

***Mukasyaa kana na itina ukekya mutauni* - Mkazaa mtoto na kisha ukamtupa kwenye mtaro**

Ukatwika ndeki kali ilavu sya mulolongo - Ukawa msherati mkali katika vilabu vya Mlolongo **UB 3 UK 132**

Pia katika ubeti huu mwanamke amechorwa kwa namna hasi kama asiyekuwa na utu. Kwa mfano mwimbaji katika mshororo wa tatu anasema kuwa mhusika alizaa mtoto kisha akamtupa kwenye mtaro. Kitendo cha kutupa mtoto kwenye mtaro kinaonyesha ukosefu wa utu na kutowajibika kwa mwanamke.

Vilevile mwanamke amechorwa kama chombo cha kumfurahisha mwanamume na ambaye umuhimu wake ni kuolewa na kumridhisha mwanamume. Kwa mfano, katika muziki huu **WK KIMB V UK 131**;

***Ila woonaa aka atwae tikwitha me ndia* -** Unapowaona **wanawake waliolewa sio kwamba ni wajinga**

Ni kwitha ***usu niwo wia wa aka duniani* -** Ni kwasababu **hiyo ndiyo kazi ya wanawake duniani**

Naku utiiye utwae usulule usu nu ukambavu **-** Nawe umeacha kuolewa uzurure huo ni umpumbavu

Na kusyaa kana na ukekya isu ni laana - Na kujifungua mtoto na kutupa hiyo ni laana. **UB 4 UK 132**

Sentensi hizi zinaonyesha mtazamo wa kijinsia unaoweka ndoa kama jukumu kuu na la lazima kwa mwanamke. Aidha, mwimbaji anawalaumu wanawake wasioolewa anaposema *"ila wonaa aka atwae ti kwithia me ndia* -unapowaona wanawake walioolewa sio kwamba ni wajinga*"* na "*ni kwithia usu niwo wia wa aka duniani* – Ni kwa sababu hiyo ndio kazi ya wanawake duniani." Ujumbe huu unaangazia masuala ya kijinsia kwa kuakisi matarajio ya kijamii kuhusu mwanamke kama "mke na mama." Mtazamo huu unaweza kuchukuliwa kuwa wa kibanifu na unaoweza kudhibiti uhuru wa wanawake kwa kuwakaba katika majukumu ya kifamilia tu, badala ya kutambua uwezo wao katika nyanja nyingine kama elimu, kazi au uongozi.

Mfano mwingine ni katika muziki **WM KIMB III UK 128** ubeti ufuatao;

Unguniaa simu kila wikendi yavika - Huwa unanipigia simu kila wikendi ikifika

Uimbia numaale wina mauseo - Unaniambia nitoke uko na mazuri

Mitoto mwa ya university ngethe mbyu - Vipusa wa chuo kikuu wasichana warembo

Na navika ndikwithia na maveti makuu - Ila nikifika nakupata na kina mama wakongwe **UB 2 UK 128**

Nisuvia iveti syaku ndeiwa ngalama - Huwa nawafadhili wanawake wako bila kuhisi gharama

Leu mbuki mbaka too no mbilu yakwa - Chakula, pombe hadi malazi ni gharama yangu

Na ndwi thoni nakuivia nginya leu wa utuku - Na hauna aibu nilikuwa nakulipia hadi chakula cha usiku **UB 3, MSH 1, 2, 3 UK 129**

Katika ubeti wa pili, mshororo wa pili, mwimbaji ametumia msemo "*wina mauseo* - Uko na mzuri" kurejelea wasichana warembo wa chuo kikuu ambao rafiki yake huwa ameahidi kumletea. Msemo huu umetumika kumchora mwanamke kama chombo cha kumfurahisha mwanamume kwani mwimbaji anatarajia rafiki yake amletee wasichana wazuri wa chuo kikuu watakaomfurahisha. Vilevile mwimbaji katika ubeti huu anatumia maneno ya kumdunisha na kudhalilisha mwanamke kama vile; "*maveti makuu*- akina mama wakongwe" na "*mitoto* – vipusa." Mwimbaji anawarejelea wanawake waliokomaa kiumri kama watu wakongwe na wasio na ladha yoyote anaposema "*maveti makuu*" na kuwarejelea wasichana wa chuo kikuu kama "*mitoto*." Mwimbaji huyu pia amemchora mwanamke kama mtu asiyekuwa na uwezo wa kumiliki mali ama asiye kuwa na chake bali anamtegemea mwanamume kwa kila jambo. Kwa mfano katika ubeti wa tatu anaposema *'Nisuvia iveti syaku ndeiwa ngalama* - Huwa nawafadhili wanawake wako bila kuhisi gharama, *Leu mbuki mbaka too no mbilu yakwa* - Chakula, pombe hadi malazi ni gharama yangu*"* **MSH 1&2**. Mwimbaji analalamika kuwa alikuwa anagharamia mahitaji yote ya wanawake wa rafiki yake bila kuhisi gharama. Hii ina maana kuwa mwanamke anafadhiliwa na

mwanamume kwa kila jambo. Matokeo haya yanalingana na utafiti uliofanywa na Zolkifli na Ghani (2024) ulioonyesha jinsi matumizi ya mikakati ya kimtindo kama vile, sitiari, urudiaji na taashira hutumika kuchora na kuhimiza wanawake. Wanadai kuwa mikakati ya kimtindo ni muhimu katika kuimarisha diskosi ya mawasiliano kuhusu mwanamke katika muziki maarufu.

4.4.2 Kuwasilisha Jumbe za Kisiasa

Maudhui ya kisiasa yametawala katika muziki **MK KIMB II UK 127.** Mwimbaji ametumia vipengele mbalimbali vya kimtindo kufanikisha maudhui haya. Swali la kibalagha "Mkubwa kwani ulisahau? - *Munene ko wolilwe?"* limetumika kama mada ya muziki huu na kurudiwa kama kibwagizo katika kila ubeti. Kwa mfano, katika mshororo huu:

> *Ninguseng'a na ngikulya ii munene we kowolilwe* - Ninashangaa na kuuliza, mkubwa kwani ulisahau? **UB I MSH 7 UK 127**

Sentensi hii ni kibwagizo cha beti za muziki huu na imerudiwarudiwa ili kusisitiza ujumbe ambao mwimbaji anapitisha kwa mwanasiasa anayelengwa. Mwimbaji anasisitiza kuwa mwanasiasa amemsahau baada ya kupata cheo kwa kuuliza swali hili la kibalagha. Pia, neno "*Munene"- Mkubwa* ni jina la lakabu ambalo mwimbaji amempa mwanasiasa anayemrejelea katika muziki wake. Mwimbaji analalamika kuwa mwanasiasa amemsahau baada ya kunyakua uongozi.

Maudhui ya kisiasa pia yanapatikana kupitia matumizi ya sentensi fupi katika **MK KIMB II UK 127** ubeti ufuatao;

> *Munene wambiiye tukambeini, Nikenda kivila kyuke kwit* - Mkubwa uliniambia tupige kampeni, ndiposa kiti kije kwetu
>
> *Munene wambiiye we ukanzuvia, Oila kivila kiuka kwitu* - Mkubwa uliniambia wewe utanitunza, pindi tu kiti kitakapokuja kwetu
>
> *Kivila niwoosie, na nyie ndwanzuvia* - Kiti ulichukua, na mimi haunitunzi

Kivila ni twosie, na we mwa niwaie - Kiti tulichukua, na wewe ukapotea

Ninguseng'a na ngikulya ii, munene we kowolilwe? (wiper), - Ninashangaa na kuuliza mkubwa kwani ulisahau? (*wiper*) **UB 1 UK 127**

Katika sentenzi hizi kuna urudiaji wa neno '*kivila*' (kiti) ambalo ni neno la kijazanda lenye maana ya uongozi. Neno hili limerudiwarudiwa kusistiza umuhimu wa uongozi katika jamii hii ya Wakamba. Ubeti huu unaonyesha usaliti wa kisiasa kwani mwimbaji anasema kuwa "mkubwa" alimwambia wapige kampeni ndiposa uongozi uje kwao kisha baada ya kupata uongozi amtunze. Lakini kinyume na matarajio yake mwanasiasa hajashughulikia matakwa yake, kwani anasema baada ya kuchukua kiti mkubwa alipotea. Kauli "kiti kije kwetu" limetumika kitashihisi kumaanisha haja ya uongozi kuja katika jamii ya mwimbaji. Pia mwimbaji katika ubeti huu anatumiasentensi tongole anapotamka neno *wiper* ambalo ni jina la chama cha mwanasiasa anayerejelewa. Kulingana na Street (2013), muziki wa kisiasa ni nyenzo ya kuhamasisha jamii kuhusu usaliti na unyanyasaji wa kisiasa. Jambo linalobainika katika muziki huu.

4.4.3 Suala la Dawa za Kulevya

Waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba wametumia mikakati ya kimtindo kuwasilisha suala la matumizi ya dawa za kulevya. Kwa mfano;

Muziki **SY KIMB I UK 125** unaangazia athari na uhalisia wa matumizi ya dawa hizi, ambapo umejikita katika kuonyesha madhara ya uraibu na namna dawa hizo zinavyoharibu maisha ya watumiaji. Mwimbaji anatumia mikakati mbalimbali ya kimtindo ili kurutubisha na kuwasilisha maudhui haya kwa namna yenye mvuto na uzito wa kijamii. Kwa mfano, mada ya wimbo huu "*Sikala Yakwa* -Sigara Yangu" ina matumizi ya leksimu *sigara* lenye maana aina ya dawa ya kulevya. Vilevile katika muziki huu ubeti ufuatao umesheheni msamiati wa mihadarati.

Ningwiwa muyo kameneja, musasuko mwingi na raha - Ninafurahi mimi kameneja, utamu mwingi na raha

Ngasyoka ngavewa mulamu, ila ni ***stimu*** *swakwa nyie* - Ninarudi kuhisi mvuto, wakati niko na stimu zangu mimi

Nikyongete na ngavya ngwai, Nithuanite na andu me mikwa –Nikitafuna **miraa** na kuvuta **bangi**, sina hamu ya watu wenye kisirani **UB I, MSH 1,2,3 UK 125**

Katika ubeti huu mwimbaji ametumia maneno *muyo, musasuko* na *raha* katika mshororo wa kwanza ambayo ni visawe vya neno furaha kuonyesha jinsi anavyoshabikia na kurafurahia uraibu wake wa dawa za kulevya. Hii inaonyesha mtazamo chanya wa kibinafsi juu ya dawa hizo, licha ya hatari zake kiafya na kijamii. Mwimbaji anataja aina za dawa za kulevya anazotumia kama vile bangi, miraa na sigara. Kauli '*ngavya ngwai*' katika mshororo wa tatu ni msemo wa lugha ya Kikamba wenye maana ya kuvuta bangi.

Vilevile katika ubeti ufuatao muziki **SY KIMB I UK 125;**

Kitumi ndyendete kelele, nivulanitye Matenzawa - Kwa maana sipendi kelele, nikiwa nimelewa Matenzawa

Stimu sya vangi kindingi, na milaa isilaa kimwe - Stimu za bangi, pombe na miraa zinafanana

Iyisene na miambile, syendete vandu vatulisu - Hazijui kupiga mdomo, zinapenda mahali tulivu **UB 2 UK 125**

Mwimbaji anaeleza mazingira ambayo ni mwafaka kwa matumizi ya dawa za kulevya anapotumia kauli kama vile; "*Stimu sya vangi, kindingi* - Vileo kama bangi, pombe na miraa zinafanana" na "*Iyisene na miambile syendete vandu vatuliu"* - Hazijui kupiga mdomo, zinapenda mahali tulivu." Mkakati wa kimtindo wa uradidi umetumika kusisitiza jinsi mazingira yanavyochangia katika matumizi ya dawa za kulevya. Matokeo haya yanathibitishwa na ripoti ya Chuo Kikuu cha California, Berkeley, ambayo ilibaini kuwa katika kipindi cha miaka ishirini, marejeleo ya matumizi ya dawa za kulevya katika muziki wa *Rap* yaliongezeka mara sita, huku ujumbe unaoshabikia matumizi hayo ukionekana kukubalika zaidi katika jamii. Jambo hili linaonyesha kuwa baadhi ya muziki huwasilisha dawa za kulevya kama

sehemu ya maisha ya kawaida au chanzo cha raha ya maisha badala ya kuziangazia kama hatari (Health Day News, 2008).

Muziki huu unaakisi mtazamo wa kifasihi unaojielekeza katika kutukuza au kushabikia matumizi ya dawa za kulevya. Ingawa unaweza kuonekana kama uhalisia wa kijamii, pia unaibua mjadala kuhusu nafasi ya wasanii katika kuhamasisha au kukosoa tabia hatarishi katika jamii. Badala ya kukemea uraibu, mwimbaji anaonekana kuusifia kama chanzo cha raha na kuridhika kwa mtu binafsi. Kwa hivyo, muziki huu unakuwa chombo cha kuonyesha mtazamo wa mtumiaji, lakini pia unaweza kutumika kama nyenzo ya kuchambua mitazamo ya kijamii kuhusu dawa za kulevya miongoni mwa vijana. Pia, hali kama hii ilidhihirishwa katika uchambuzi wa yaliyomo kwenye muziki wa kizazi kipya, ambapo ilibainika kuwa wasanii wengi huonyesha matumizi ya mihadarati kama sehemu ya mtindo wa maisha unaotamanika (Primack na wenzake, 2018).

Katika muziki **WM KIMB III UK 128,** mikakati ya kimtindo imetumika kukuza na kuendeleza maudhui ya matumizi ya dawa za kulevya kama ifuatavyo;

> *Leu* ***mbuki*** *mbaka too no mbilu yakwa* - Chakula, pombe hadi malazi ni gharama yangu **UB 3 MSH 2 UK 128**
>
> *Twataanisya uilika* ***tulavu*** *Mukuru* -Tukiachana unaingia vilabu vya Mukuru
>
> *Uyambiiya uzambasya uivoya kimee* - Unaanza kunidhalilisha ukiomba pombe **UB 4 MSH 1,2 UK 129**

Katika mishororo hii **(MSH 2 UB 3 na MSH 1, 2 UB 4**) mwimbaji anaeleza sababu za kutaka kuvunja urafiki wake na rafiki anayemnyanyasa. Katika ubeti wa tatu mshororo wa pili, inaoneka jinsi mwimbaji na rafiki yake walivyo na uraibu wa kulewa pombe. Vilevile neno *"tulavu* – Vilabu*"* limetohozwa katika ubeti wa nne, mshororo wa kwanza. Neno hili linarejelea vilabu ambapo ni maeneo ya vileo. Mwimbaji aneleza madhara ya dawa za kulevya anaposema *"uyambiiya uzambasya uivoya kimee-* unaanza kunidhalilisha ukiomba pombe. Neno "kunidhalilisha-*uzambasya,"* ni msemo wa lugha ya Kikamba yenye maana ya kumsengenya mtu au kumwaribia mtu jina. Mwimbaji anasema rafiki yake huwa anamsengénya katika

vilabu vya Mukuru akiomba pombe. Hii inatokana na uzoefu wa matumizi ya pombe unaopelekea rafiki yake kuenda kuomba pombe wakati mwimbaji hayupo kumsaidia. Katika muziki huu, mwimbaji anatumia mikakati mbalimbali ya kimtindo kuonyesha athari za matumizi ya dawa za kulevya katika maisha binadamu kijamii, kiuchumi na kihisia. Kwa hivyo, muziki huu unakuwa chombo cha kutafakari nafasi ya uraibu wa mihadarati miongoni mwa watu katika jamii, pamoja na changamoto za mahusiano zinazotokana na matumizi ya dawa za kulevya. Matokeo haya yanalingana na matokeo ya uchambuzi uliofanywa na Wright na wenzake (2018), ambao uligundua kuwa utambulisho na msimamo wa vijana katika tamaduni zinazohusiana na muziki, kama vile *Hip-Hop* unahusishwa na hatari zinaoongezeka kutokana na matumizi ya tumbaku na aina nyingine za dawa za kulevya.

Katika muziki **RN KIMB VI UK 132**, katika mishororo ifuatayo

> *Starehe sya aka na kuteewa syi muyo* - Starehe za wanawake na kuuziwa zina ladha,
>
> *Musaala waku wi miniwa baa ni aka* - Mshahara wako utamalizika kwenye klabu kwa wanawake
>
> *Na wathelelwa mayosa abiria ungi* - Na ukiishiwa wanachukua abiria mwingine **UB 1 MSH 5,6, 7 UK 132**

Mishororo hii inaonyesha madhara ya kiuchumi yanayotokana na na matumizi ya dawa za kulevya. Mwimbaji anatoa onyo kwamba kuenda katika maeno ya burudani almarufu klabu kutasababisha matumizi mabaya ya fedha. Kwa mujibu wa Johnson na Lee (2020) uraibu wa dawa za kulevya husababisha masaibu ya kifedha na kupelekea kuzorota kwa uchumi wa mtu binafsi na kuchangia deni. Msemo "*mayosa abiria ungu*- wanachukua abiria mwingine" inadhihirisha mwendelezo wa kutegemeana na uraibu wa kuendeleza madhara ya dawa za kulevya.

4.4.4 Kuwasilisha Hisia za Kibinafsi na Kijamii

Kulingana na Leech (1969) lugha ya kisanii hutumia miundo ya kimtindo kama vile fonolojia, uchaguzi wa maneno na sintaksia ili kuibuia hisia maalum kwa hadhira lengwa. Waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba wametumia mikakati ya kimtindo kuwasilisha hisia za kibinafsi na za kijamii. Kwa mfano;

Katika muziki **GF KIMB IV UK 129** mwimbaji anaonyesha hisia zake za kimapenzi kwa msichana anayempenda aliye nchi ya Ujerumani. Hili linabainika anaposema ataenda kwa miguu hadi Ujerumani kumtembelea mpenzi wake. Isitoshe anatumia maneno ya kimapenzi kama vile *sweetie, mbevi* kama ilivyo katika beti hizi;

> *Niuka na maau Germany Ruth sweetie* - Nitakuja kwa miguu Ujerumani Ruth 'sweetie'
>
> *No mbaka ngwone ngoo yakwa itulie* - Lazima nikuone roho yangu itulie. **UB 5 UK 130**
>
> *Ndisya kumiisya mbaka wiuika we mbevi* - Siwezi kuvumilia hadi uje mpenzi
>
> *Kita umbeteela German niuka na mau* - Nisubiri Ujerumani nitakuja kwa miguu. **UB 6 UK 130**

Maneno katika beti hizi *Mbev*i na *Sweetie* yametumika kurejelea mpenzi. Vilevile mwimbaji anawasilisha hisia za mapenzi yake anaposema lazima amwone mpenzi wake roho yake itulie kwani hawezi kuvumilia tena.

Vilevile, muziki unatumika kupitisha hisia za kibinafsi kama ilivyo katika **SY KIMB I UK 125** ubeti ufuatao:

> *Nigwwa muyo kameneja, musasuko mwingi na raha* - Ninafurahi mimi kameneja, utamu mwingi na raha
>
> *Ngasyoka ngavewa mulamu, ila ni stimu swakwa nyie* - Narudi kuhisi mvuto, wakati niko na stimu zangu mimi
>
> *Nikyongete na ngavya ngwai, Nithuanite na andu me mikwa* -Nikitafuna miraa na kuvuta bangi, sina hamu ya watu wenye kisirani **UB 1 UK 125**

Kutokana na ubeti huu (UB 1) ni dhahiri kuwa mwimbaji anapitisha hisia za furaha inayotokana na matumizi ya dawa za kulevya, ametumia maneno ya visawe kama vile *muyo, musasuko* na *raha* - Utamu mwingi na raha, ambayo yana maana ya furaha ili kusisistiza hisia zake za uraibu wa vileo.

Pia waimbaji wa muziki wa Benga hutumia mikakati ya kimtindo kwa lengo la kupitisha hisia za kijamii. Kwa mfano katika muziki **MK KIMB II UK 127**; Mwimbaji anasema kuwa alikuwa akiomba mungu amsaidie mwanasiasa ndiposa achukue uongozi aweze kusaidia jamii yake. Anasema kuwa hata baada ya kupata uongozi bado jamii yake ingali na shida anaposema;

> *Navoyaa ngai nginya ngolwa ni kwivoyea* - Nilimwomba Mungu hadi nikasahau kujiombea
>
> *Unene nitwoosie na no tukuthina* - Ukubwa tulichukua na bado tunashida **UB 2 MSH 1, 4 UK 127**

Kimsingi, nadharia ya umtindo inasisitiza kwamba uchaguzi wa mtindo hauhusu tu kujenga ujumi katika lugha bali pia ni muhimu katika kueleza na kuibua hisia kwa hadhira. Jinsi msanii anavyobadilisha miundo ya lugha husaidia kuwasilisha mihemko, toni na hisia ambazo huchochea fasiri za hadhira lengwa. DeNora (2000) anasisitiza kuwa muziki hufanya kazi kama teknolojia ya nafsi, inayowawezesha watu kudhibiti hisia, kumbukumbu na hali za kijamii kupitia usikilizaji na uigizaji wa muziki kwa namna ya kibinafsi. Uchanganuzi huu unathibitisha kuwa uchaguzi wa kimtindo katika muziki si wa kiholela, bali ni wa kimakusudi ili kuwasilisha maana za kina, za kihisia na kijamii.

4.4.5 Kuhamasisha kuhusu Maadili na Kuchochea Mabadiliko ya Kijamii

Vipengele vya lugha vinaweza kutumika kuhamasisha, kuathiri au kuchochea hisia na misimamo ya kijamii. Kulingana na Leech (1969), vipengele vya kimtindo vinaweza kutumika kuunda athari au hisia maaalum. Finnegan (2012) anadokeza kuwa fasihi simulizi na desturi za muziki wa Kiafrika mara nyingi hutumia vipengele vya kishairi na kimtindo kuwasilisha masuala ya kijamii. Ngara (1985) anadokeza kwamba, vipengele vya kimtindo katika fasihi na nyimbo hutumika kama vyombo vya ushawishi wa kiitikadi, kwa kuchanganya urembo wa kisanaa na ufundishaji wa maadili. Hivyo, kupitia matumizi ya mikakati ya kimtindo, wanamuziki wanaweza kuwahusisha wasikilizaji kwa ufanisi huku wakitoa mafunzo yenye nguvu kuhusu hali ya jamii. Waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba wametumia mikakati ya kimtindo kuelimisha au kuhamasisha jamii kama ifuatavyo;

Muziki **WK KIMB V UK 131** katika ubeti ufuatao; jamii inaonywa dhidi ya kitendo cha uavyaji mimba.

> *Naku utiiye utwae usulule usu nu ukambavu* - Na wewe umeacha kuolewa uzurure, huo ni umpumbavu
>
> *Na kusyaa* ***kana na ukekya isu ni laana*** **- Na kujifungua mtoto kisha kumtupa hiyo ni laana**
>
> *Niona wi ndia Wakatimba wi mana* - Ninaona ukiwa mjinga Wakatimba wewe ni bure
>
> *Na ndinakuuma Wakatimba kumbavu* - Na sijakutusi wakatimba mpumbavu **UB 4, MSH 3,4,5,6 UK 132**

Katika ubeti huu mwimbaji anamwonya mhusika kuwa kitendo cha kujifungua na kutupa mtoto kingemsababishia laana. Jamii inaelimishwa umuhimu wa kuwatunza watoto na kuzingatia haki zao. Mwimbaji anamwambia mhusika kuwa kujifungua na kutupa mtoto ni laana, jambo hili linawatahadharisha watu wengine katika jamii wanaoweza kufanya kama mhusika. Mwimbaji anamchora mhusika kama ishara ya kukengeuka kimaadili na kuangazia tabia yake kama onyo kwa wanajamii wengine ambao wanaweza kuwa na tabia kama hizo. Taswira ya matendo ya mhusika inaibua hisia kwa upande wa msikilizaji na kumfanya awe mwangalifu kuhusiana na madhara ya kijamii yanayotokana na matendo sawia. Hivyo jamii inahimizwa kutafakari uzito wa tabia kama hizo na hivyo kuufanya muziki huu uwe chombo cha kuelekeza jamii. Kwa mujibu wa Leech (1969) uchaguzi wa kiisimu kama vile maneno, sintaksia na fonolojia una uwezo wa kuathiri mitazamo ya kijamii kwa namna mbalimbali.

Katika muziki **MK KIMB II UK 127,** swali hili la balagha limerudiwa mwishoni mwa kila ubeti.

> "*Ninguseng'a na ngikulya ii munene ko woolilwe –* Ninashangaa na kuuliza, mkubwa kwani ulisahau?*"*

Swali hili linasisitiza kufadhaika kwa mwimbaji kutokana na usaliti aliofanyiwa na mwanasiasa aliyemchagua. Kwa kurudia neno *"mkubwa"*, mwimbaji analenga kusisitiza nafasi ya kiongozi ambaye yeye na jamii yake walimchagua kwa imani kubwa. Hata hivyo, msisitizo huo unaibua hali ya kukatishwa tamaa pale ambapo

kiongozi huyo anashindwa kuwasaidia kama walivyotarajia. Kwa kutumia sentensi hizi mwimbaji analenga kuhamasisha jamii iweze kutafakari kuhusu hali ya kisiasa na kijamii inayoathiri maisha yao ya kila siku. Mwimbaji analenga kuhamasisha jamii kuhusu tabia ya baadhi ya wanasiasa ambao huwapa matumaini wananchi wakati wa kampeni kwa ahadi zisizotekelezwa na kisha kuwasahau mara baada ya kupata mamlaka. Muziki huu unatumika kama jukwaa la kukosoa mifumo ya kisiasa yenye upungufu wa uwajibikaji, kwa kusisitiza hatari ya uongo wa kisiasa, udanganyifu wa viongozi na kuangazia athari zake kwa wananchi wa kawaida. Kwa kiwango kikubwa, mwimbaji anatilia mkazo haja ya jamii kuwa macho dhidi ya propaganda za kisiasa, hivyo kuchochea mabadiliko ya kifikra kuhusu uongozi bora na uwajibikaji wa viongozi walioko madarakani.

Katika muziki **RN KIMB VI UK 132,** mwimbaji analenga kuhamasisha jamii katika mishororo ifuatayo;

> *Raha ndukauna kuma tene ndukauna* – Raha haisaidii kutoka zamani raha haisaidii **UB 1 MSH 1 UK 133**
>
> *Starehe sya aka na kuteewa syi muyo* - Starehe za wanawake na kuuziwa zina ladha,
>
> *Musaala waku wi miniwa baa ni aka* - Mshahara wako utamalizika kwenye klabu kwa wanawake, **UB 1 MSH 5, 6 UK 133**
>
> *Ndwike masavu, ika masavu, eka uvitya masavu* - Fanya hesabu, fanya hesabu, wacha kukosea hesabu **UB 1 MSH 12 UK 133**
>
> *Ngimina niasya Mbivilia yo yiasya* - Nikimaliza nasema Bibilia inasema,
>
> *Mundu wa kanzu ili akulile ula uteimwe* - Mtu aliye na kanzu mbili amwazime asiyekuwa na lolote **UB 4 MSH 1,2 UK 134**

Matumizi ya kauli "*raha ndukau* - raha haisaidii" katika muziki huu inatumika kuelimisha kuhusu maadili muhimu ya maisha kama vile utunzaji wa fedha,

uwajibikaji wa mtu binafsi na maadili ya kijamii. Muziki huu unatahadharisha dhidi ya matumizi mabaya ya pesa, maisha ya starehe kupindukia na kupuuza malengo ya muda mrefu, huku ukisisitiza umuhimu wa kupanga bajeti, kufanya kazi kwa bidii, na ustawi wa kifamilia. Mishororo kama vile "*Ndwike masavu, ika masavu, eka uvitya masabu* - Fanya hesabu, fanya hesabu wacha kukosea hesabu" na "*Musaala waku wiminiwa baa ni aka* - Mshahara wako utamalizika kwenye klabu kwa wanawake" imetumika kama mafundisho ya kimaadili na ukosoaji wa kijamii, hasa kwa vijana wanaokabiliana na changamoto za kiuchumi.

Zaidi ya hayo, wimbo huu unasisitiza huruma na msaada wa kijamii, ukitumia marejeo ya kidini na kitamaduni kama vile "*Mundu wa kanzu ili akulile ula uteimwe* - Mtu aliye na kanzu mbili amwazime asiyekuwa na lolote," Kwa jumla, wimbo huu unachanganya maoni ya kijamii na mafundisho ya kimaadili, ukionyesha jinsi muziki unavyoweza kutumika kama njia ya elimu ya maisha na kuongeza uelewa wa jamii. Hii inalingana na nadharia ya Paulo Freire (1970) ya elimu kama zoezi la uhuru, inayosisitiza uelewa wa kina wa kijamii na ustawi wa pamoja. Ujumbe katika muziki huu unatumika kama somo la maadili kuhusu usawa wa kijamii na huruma kwa wengine.

Pia katika muziki **SY KIMB I UK 125**;

> *Iwa nthoni muno malama na uithi uthambe ndia ino* - Hisi aibu sana wewe Malama, na uende uoge mjinga wewe
>
> *Na uyieka uthi uikengana, wi wa mbadi ya Matenzawa* - Na uache kuenda ukidanganya, kwamba wewe ni mwanabedi wa Matenzawa
>
> *Na uvutiiye kiko Malama, muthukumi utathambaa* - Nilikupiga kalamu kwasababu ya uchafu, Malama mfanyikazi asiyeoga **UB 10 UK 127**

Katika ubeti huu mwimbaji anawaonya wanajamii dhidi ya kutozingatia usafi wa kimwili. Anadokeza madhara yanayoweza kutokana na tabia kama za mhusika "Malama" kama vile kupigwa kalamu. Utafiti uliofanywa na Danquah Dark na wenzake (2022) ulionyesha jinsi wasanii hutumia mikakati ya kimtindo kama vile

usambamba, tamathali za usemi na ukiushi kuonya dhidi ya masuala ya ufisadi na kuhimiza usawa wa kijamii. Maoni haya yanawiana na matokeo yetu ambapo imebainika kuwa waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba hulenga kuonya jamii kuhusiana na matumizi mabaya ya fedha na maadili yasiyofaa katika jamii.

4.4.6 Kuendeleza Utamaduni

Leech (1969) anasisitiza kuwa lugha haitumiki katika ombwe tupu bali hujikita kwa kina katika utamaduni ilikotoka na kuakisi imani, maadili na kanuni za jamii husika. Leech, anasema kwamba miundo ya kimtindo ya kazi ya sanaa huathiriwa na muktadha wa kitamaduni ambamo kazi hiyo imetolewa. Miundo hii inaweza kuathiri jinsi kazi hiyo inavyoeleweka na hadhira lengwa. Mikakati ya kimtindo imetumika kuendeleza tamaduni za jamii ya Wakamba kama ifuatavyo;

Muziki **SY KIMB I UK 125** sentensi ifuatayo;

> *Imwe ndia na itathambaa, yiania kiko* ***mutheketi*** - Wengine wajinga na wasiooga, ni wachafu kama **tarimbo UB 4 MSH 2 UK 125**

Katika sentensi hii mwimbaji anamfananisha mwanamuziki mwingine na tarimbo-*muthekethi*. Neno '*muthekethi*- tarimbo' ni kifaa kinachotumiwa katika jamii ya Wakamba kuchimba mashimo mchangani. Mashimo hayo hutumika kupanda mbegu za chakula au kutengeneza maghala ya kuweka chakula. Kutokana na matumizi ya neno hili "muthekethi" jamii inakumbushwa utamaduni wao ambao ni kupanda na kuhifadhi chakula. Isitoshe, mwimbaji anawakosoa wengine wanaoshindwa kudumisha viwango vya usafi na nidhamu ambavyo mzungumzaji anahusisha na utambulisho wa kitamaduni wa jamii hii ya wakamba.

Pia katika Muziki huu **SY KIMB I UK 126** ubeti wa sita:

> *Niilye ou na ndivinduka, ona ngavuwa nivo vau* - Niko hivyo na siwezi badilika, hata nikipigwa ni hivyo
>
> *Na ndi kilasi Matenzawa, vai mundu tutatindanywa* - Na sina cheo Matenzawa, hakuna mtu hatuwezi kuishi na yeye

> *Ona ethiwa ni chokola ngutavye, muradi twithye tuyiwana* - Hata ikiwa ni chokora nikwambie, ilmradi tuwe tunasikilizana **UB 6 UK 126**

Matumizi ya kejeli yanadhihirika katika mishororo kama vile: "hata ikiwa ni chokora nikwambie, ilimradi tuwe tunasikilizana," ambapo mzungumzaji anapandisha kwa kutumia kejeli wazo la "chokora" (mtu wa mtaani au ombaomba) hadi kwenye nafasi ya usawa. Jambo hili linadokeza swala la madaraja ya kijamii na tofauti za kitabaka katika jamii ya mwimbaji. Inaonyesha kwamba katika jamii hii ya Wakamba thamani ya mtu haitambulishwi kwa utajiri au usafi bali kwa uzoefu wa pamoja wa binadamu na kuelewana. Kutokana na ubeti huu jamii inakumbushwa kukwepa kuwatega watu kulingana na vyeo au matabaka ya kijamii.

Katika muziki **RN KIMB VI UK 131** mwimbaji anatumia mikakati mbalimbali ya kimtindo kukuza na kuendeleza utamaduni hasa kuhusu masuala ya kazi, pesa, familia na umoja. Matumizi ya misemo kama vile;

> *Ivundisye kusuvia mbesa syaku mwanake na uiyeka uyaa oou ta ngaange, ti mboneki* - Jifunze kutunza pesa zako kijana, na uache kuzitumia hivyo kama ambazo zimekaangwa, si rahisi kupatikana **UB 1 MSH 12 UK 131**
>
> *Na wathelelwa mayosa abiria ungi, uilekelwa mbevo uithina ta kana ka ngya*- Na ukiishiwa wanachukua abiria mwingine, unaachwa kwenye baridi na kuteseka kama mtoto wa maskini **UB 1 MSH 7,8 UK 131**
>
> *Ndwike masavu, ika masavu, eka uvitya masavu* - Fanya hesabu, fanya hesabu, wacha kukosea hesabu. (Kibwagizo) **UK 131**

Matumizi ya mishororo hii ya kitamathali inaonyesha matumizi ya lugha ya kawaida katika jamii hii na inatekeleza jukumu la mafunzo ya kimaadili. Kauli hizi zinadhihirisha maadili ya uwajibikaji wa mtu binafsi na jamii kwa jumla kwa kutilia maanani vizazi vijazo kama ilivyo desturi ya mafunzo za tamaduni za kiafrika (Thiong'o, 1986). Uradidi wa sentensi; "*Ndwike masavu, ika masavu, eka uvitya*

masavu - Fanya hesabu, fanya hesabu, wacha kukosea hesabu" umetumika kama mwongozo wa kiuchumi na mkakati wa kimtindo kukumbusha na kuhimiza jamii kuhusu uwajibikaji wa kifedha. Matumizi ya kibwagizo katika kazi za kifasihi, ikiwemo muziki wa Benga, huchukua nafasi muhimu ya kimaana na kimaumbo. Kwa mujibu wa Momanyi na Maitaria (2011), kibwagizo si tu mshororo unaorudiwa mwishoni mwa beti, bali ni kifaa cha kimtindo kinachosaidia kuimarisha umbo na muundo wa kazi ya kifasihi, kuongeza wizani pamoja na kusisitiza ujumbe mkuu wa msanii. Katika muziki huu **(RN),** kibwagizo kimetumika kama mbinu ya kusisitiza dhima kuu za kijamii zinazowasilishwa kwa kutoa onyo kwa wanajamii. hii inalingana na maoni ya Barber (1997), kwamba wanamuziki wa Kiafrika mara nyingi hupachika jumbe za maadili na kijamii ndani ya mifumo ya kimtindo ili kuwezesha mashairi au muziki kufanikisha kwa wakati mmoja burudani na elimu ya kitamaduni. Matumizi ya marejeleo ya Biblia katika muziki huu yanatia muziki huu kina cha kidini na kimaadili na kupatanisha maadili ya Kikristo na ukomunisti wa jadi wa Kiafrika. Haya ni katika muziki **RN KIMB VI UK 132** mishororo ifutayo;

> *Ngimina niasya Mbivilia yo yiasya, Mundu wa kanzu ili akulile ula uteimwe*- Nikimaliza nasema Bibilia inasema, Mtu aliye na kanzu mbili amwazime asiye na lolote **UB 4 MSH 1, 2 UK 134**

Marejeleo ya kidini, kwa kutumia vipengele vya kimtindo ndani ya lugha ya kila siku, yanatoa mfano wa jinsi mikakati ya kimtindo inavyotumiwa kusimba mitazamo mipana ya kitamaduni. Matokeo haya yanalingana na utafiti uliofanywa na Osubo & Kebaya (2023) uliobainisha kuwa, waimbaji kwa ustadi hutumia mikakati ya kimtindo kukuza na kuendeleza utamaduni na kuufanya wimbo kuwa nyenzo ya kitamaduni inayolenga kuunda kanuni za kimaadili na kuongoza tabia za watu binafsi katika jamii.

4.4.7 Kukuza Ushirikiano katika Jamii

Kwa mujibu wa Leech (1969) lugha ina jukumu la kijamii kuimarisha ushirikiano, umoja na utambulisho wa kijamii. Wanamuziki hutimiza jukumu hili kwa kutumia vipengele vya kimtindo kama vile kuchanganya ndimi, urudiaji, misemo na vitendawili vya kitamaduni. Kupitia ukiushi wasanii huhimiza utambulisho wa makundi ya jamii na kujenga hisia za umoja wa kitamaduni. Kwa mfano, matumizi

ya mara kwa mara ya lugha za kilahaja, methali, na marejeleo ya kauli zinazofahamika kijamii na kisiasa katika muziki hutumika kama mkakati wa kimtindo wa kuanzisha ukomunisti na fahamu za pamoja (Leech, 1969). Thiong'o (1986) anasisitiza umuhimu wa uchaguzi wa lugha katika kuendeleza umoja na utambulisho wa jamii. Kwa mujibu wa Barber (1997) wasanii maarufu wa muziki wa Kiafrika mara nyingi hutunga muziki unaoleta ushirikiano katika jamii kupitia tamaduni na masuala ya kijamii yanayohusiana.

Waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba wametumia mikakati ya kimtindo kwa lengo la kujenga ushirikiano katika jamii kama ifuatavyo:

Katika muziki **RN KIMB VI UK 132** ubeti ufuatao;

> *Kwithiwa na mbesa ndumanye isu ni vaati* - Kuwa na pesa, jua hiyo ni bahati,
>
> *Syaite muno andu aingi mainasyo,* - Zimepotea sana watu wengi hawana,
>
> *Nienda wisilye mbesa undu tukwataa,* - Nataka ufikirie pesa vile huwa tunapata,
>
> *Kuthukuma utuku andu ala angi metoo,* - Kufanya kazi usiku watu wale wengine wakiwa wamelala,
>
> *Wia ofisi onawo wio fatigue,* - Kazi ya ofisi pia inachosha,
>
> *Kwetelaa mbesa mpaka mwisho wa mwei,* - Kusubiri pesa hadi mwisho wa mwezi,
>
> *Kivalua Kenya kyaite muno wa mama,* - Kibarua Kenya kimepotea sana mtoto wa mama,
>
> *Wakomana nakyo tumbula vate ithau,* - Ukipata fanya bila mchezo,
>
> *Ndwike masavu, ika masavu, eka uvitya masavu (Nyie bosco mulwa inamaainyie wia wa kivalua, mundu umbia neteele muthya wa mwei uikaavika twitha*

twaemaniwe)- Fanya hesabu, fanya hesabu, wacha kukosea hesabu. (mimi Bosco Mulwa nilizoea kazi ya kibarua, mtu akijaribu kuniambia nisubiri hadi mwisho wa mwezi ukifika tutakuwa tumekosana) **UB 2 UK 133**

Katika ubeti huu (UB 2) mwimbaji kimakusudi anajenga sauti ya uzoefu wa pamoja na umoja wa mapambano ya kiuchumi anaposema, "*nienda wisilye mbesa undu tukwataa,* - Nataka ufikirie pesa vile huwa tunapata, *kuthukuma utuku andu ala angi metoo*- Kufanya kazi usiku watu wale wengine wakiwa wamelala." Mwimbaji kwa kutumia kauli hizi analenga kuimarisha ushirikiano wa kijamii na kukuza umoja kwa kurejelea watu wengine katika jamii. Muziki huu unatumia mikakati ya kimtindo kuhimiza ushirikiano kwa kurejelea makundi ya wafanyikazi katika jamii kwani mwimbaji anazungumzia watu wanaofanya kazi usiku huku wengine wakiwa wamelala na pia kazi za ofisini. Urudiaji wa sentensi, "*ndwike masavu, ika masavu, eka uvitya masavu* - Fanya hesabu, fanya hesabu, wacha kukosea hesabu," unahimiza ushirikiano wa uwajibikaji. Mwimbaji anatumia sentensi tongole iliyo katika mabano, yenye toni ya mawasiliano ya kawaida mwishoni mwa ubeti huu ili kuziba pengo lililopo baina yake na wasikilizaji kwa lengo la kuimarisha umoja. Kwa kuonyesha matumizi ya pesa sio tu kwa faida ya kibinafsi lakini kwa manufaa ya jumuiya ambazo zinapaswa kutumiwa kwa busara, na kwa kuhimiza tabia ya kuwajibika kwa ajili ya vizazi vijazo, msanii anakuza sio tu nidhamu ya mtu binafsi bali uwajibikaji wa jamii kwa pamoja. Onyo lililopachikwa kwenye wimbo huu halielekezwi kwa msikilizaji aliyejitenga bali kwa jumuiya ya wafanyakazi, hivyo basi kujenga ushirikiano kama athari ya kimaadili na ya kimtindo.

Katika muziki **MK KIMB II UK 127** beti zifuatazo;

Munene wambiiye tukambeini, Mkubwa uliniambia tupige kampeni

Nikenda kivila kyuke kwitu, Ndiposa kiti kije kwetu

Munene wambiiye we ukanzuvia, Mkubwa uliniambia wewe utanitunza

Oila kivila kiuka kwitu, Pindi tu kiti kitakapokuja kwetu

Kivila niwoosie na nyie ndwanzuvia, Kiti ulichukua na mimi haunitunzi

Kivila ni twosie na we mwa niwaie, Kiti tulichukua na wewe ukapotea

Ninguseng'a na ngikulya ii munene we kowolilwe, Ninashangaa na kuuliza mkubwa kwani ulisahau? **UB 1 UK 127**

Katika ubeti huu mwimbaji anatumia vipengele vya kimtindo kuibua hisia za ushirikiano na usaliti wa jamii kwa pamoja. Matumizi ya viwakilishi vya wingi vya nafsi ya kwanza katika mishororo hii; *munene wambiiye **tu**kambeini* - Mkubwa uliniambia **tu**pige kampeni, *nikenda kivila kyuke **kwitu*** - Ndiposa kiti kije **kwetu,** *oila kivila kiuka **kwitu*** -Pindi tu kiti kitakapokuja kwetu na *Kivila ni **twosie** na we mwa niwaie* - Kiti **tul**ichukua na wewe ukapotea, vinajenga hisia za mapamabano ya kisiasa na matumaini ya jamii kwa pamoja. Uchaguzi wa lugha zinazotumika katika ubeti huu zinajenga hisia za kundi nzima la jamii bali sio mtu binafsi.

Vilevile katika muziki huu, **MK KIMB II UK 127** tazama ubeti ufuatao;

Navoyaa ngai mwa autethyie - Nilimwomba Mungu angalau akusaidie

Muvaka nyie ngolwa ni kwivoyea - Hadi nikasahau kujiombea

Ngivoya unene uke kwitu - Nikiomba ukubwa uje kwetu

Munene we nongi ututethye - Mkubwa wewe angalau utusaidie

Unene niwosie na nyie ndyaa vaidika - Ukubwa umeshauchukua na mimi sijafaidika

Unene ni twosie nanotukuthinaa - Ukubwa tuliuchukua na bado tuko na shida

> *Ninguseng'a na ngikulya ii munene we kowolilwe (wiper)* Ninashangaa na kuliza mkubwa kwani ulisahau? (wiper) **UB 2 UK 127**

Matumizi ya kinaya katika mishororo hii "*Navoyaa ngai mwa autethye*- Nilikuwa naomba Mungu angalau akusaidie, *Muvaka nyie ngolwa ni kwivoyea*- Hadi nikasahau kujiombea" inaonyesha kujinyima kwa mwimbaji binafsi kwa lengo la faida ya jamii kwa pamoja. Urudiaji wa kauli kama vile; "Unene ni twosie- Ukubwa tulichukua, *na tuyaafaidika*- na hatukufaidika" kunasababisha usambamba wa kibalagha. Jambo ambalo Leech (1969) analiona kama mkakati wa kimtindo unaokuza jukumu la kueleza na ushawishi wa lugha. Kauli hizi zinavutia umakini wa tofauti baina ya ahadi za jamii kwa pamoja na ukweli wa kujitenga pindi mamlaka yanapopatikana. Kwa kumrejela Mungu, mwimbaji analenga kuibua hisia za kiroho za umoja wa jamii na kuonyesha kwamba mapambano yao si ya kisiasa tu bali yana haki za kimungu. Haya yanaunga mkono wazo la Thiong'o (1986) kwamba waandishi na wanamuziki wa Kiafrika mara nyingi hutumia lugha ya kidini ili kuimarisha ushirikiano wa kimaadili na kuhimiza uwajibikaji wa viongozi katika jamii. Kama wanavyoeleza Draper na Duffy (2021), wanamuziki hutumia mikakati ya kimtindo kama vile urudiaji, viwakilishi vya nafsi ya kwanza wingi na ushawishi wa kiroho ili kujenga ushirikiano na utambulisho wa pamoja kwa kusisitiza ufahamu wa pamoja na tafakari za kimaadili katika jamii.

4.5 Hitimisho

Sura hii imewasilisha na kuchambua data kwa mujibu wa madhumuni ya utafiti huu na kwa kuzingatia viwango vya nadharia ya umtindo. Matokeo yameonyesha kuwa waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba hutumia mikakati mbalimbali ya kimtindo katika viwango vya udhihirikaji, umbo na semantiki. Vipengele vilivyobainika ni pamoja na uakifishaji wa beti, uradidi, urari, usambamba, tautolojia, kinaya, tamathali za usemi na mifumo tofauti ya kisintaksia. Mikakati hii imetumika kuimarisha ujumi wa aina mbalimbali, kama vile ujumi wa kisiasa, kigothiki na kihalisia. Pia mikakati imetumika kujenga athari mahsusi kwa hadhira lengwa kwa kuchochea hisia, kuhamasisha na kuhimiza ushirikiano wa kijamii. Kwa hivyo, uchanganuzi huu umeweka msingi muhimu wa kuelewa nafasi ya mtindo katika uundaji wa maana na athari za kijamii katika muziki wa Benga wa jamii Wakamba

SURA YA TANO

MAJADILIANO, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.0 Utangulizi

Katika sura hii, majadiliano kuhusu matokeo ya utafiti pamoja na hitimisho za utafiti huu zimewasilishwa. Vilevile, sura hii imetoa mapendekezo ya tafiti za baadaye kuhusiana na utafiti huu.

5.1 Majadiliano Kuhusu Matokeo ya Utafiti

Katika sehemu hii, mjadala kuhusu matokeo ya utafiti umetolewa kwa kuzingatia malengo ya utafiti huu. Malengo ya utafiti yalikuwa; kubainisha mikakati ya kimtindo wanayotumia waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba kuwasilisha ujumbe, kuchanganua jinsi waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba wanavyotumia mikakati ya kimtindo kuimarisha ujumi katika muziki wao na kueleza athari lengwa ya mikakati ya kimtindo wanayotumia waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba.

5.1.1 Mikakati ya Kimtindo

Utafiti huu ulilenga kubainisha mikakati ya kimtindo inayotumika katika muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba kwa kuongozwa na nadharia ya umtindo kama ilivyoelezwa na (Leech, 1969). Ilibainika kuwa katika kiwango cha kifonolojia waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba hutumia vipengele vya kimtindo kama vile urudiaji, urari takriri na uradidi. Katika nyimbo za Benga zilizochanganuliwa vipengele hivi vimejitokeza katika kiwango cha silabi, neno na sentensi. Vipengele vilivyobainika katika kiwango cha grafolojia ni ugawaji wa beti, uakifishaji na ugawaji wa mishororo ya muziki wa Benga. Umuhimu wa matumizi ya vipengele vya kigrafolojia na kifonolojia ni kutoa maelezo ya kina na kuongeza wizani katika muziki ili kuvutia hadhira. Hata ingawa vipengele vya grafolojia na fonolojia huongeza mvuto wa muziki kwa njia ya usanii wa lugha, pia vinaweza kudhoofisha uwasilishaji wa ujumbe ikiwa vitatumika kupita kiasi; hivyo, wasanii wanapaswa kuwa waangalifu ili kuvilinganisha kwa ufanisi na maudhui wanayolenga kupitisha.

Katika kiwango cha umbo ilibainika kuwa uteuzi wa msamiati unaofanywa na waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba ni wa kimakusudi. Ili kuwasilisha ujumbe kwa hadhira yao, waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba wanatumia vipengele mbalimbali vya kimtindo kuteua msamiati.

Vipengele hivyo ni kama vile kuchanganya ndimi ambapo maneno ya Kiswahili na Kiingereza yameingizwa katika muziki wa lugha ya Kikamba. Kwa mfano maneno kama vile “raha”, “kusema kweli” na “airport” yametumika. Pia maneno ya kubuni, kukopa na visawe yametumika katika muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba. Uchaguzi wa msamiati katika muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba umetumika kuhifadhi lugha na utamaduni wa jamii hii, pamoja na kudumisha uhusiano kati ya mwimbaji na hadhira lengwa kwa kujenga ujumi wa kisanaa. Hata hivyo, vipengele hivi vya kimsamiati vinaweza kusababisha changamoto za uelewekaji wa ujumbe kwa upande wa wasikilizaji endapo havitafasiriwa vyema.

Katika kiwango cha sintaksia waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba wametumia sentensi ndefu, sentensi fupi, sentensi za maswali na sentensi tongole. Sentensi ambazo zimetawala muziki huu kwa kiwango kikubwa ni sentensi ndefu na sentensi tongole. Waimbaji wa muziki huu hutumia sentensi ndefu na tongole kueleza zaidi au kuongeza ujumbe ili kupitisha dhamira zao kwa hadhira lengwa. Waimbaji wa Benga wa jamii ya Wakamba hutumia sentensi tongole mwishoni mwa nyimbo zao ili kujenga kilele cha muziki wao kwa wasikilizaji. Haya ni kulingana na Wambua (2001) kama alivyobaini alipokuwa akichunguza mtindo katika nyimbo za Kakai Kilonzo. Mikakati mingine iliyotumika katika kiwango hiki ni ukiushi wa kisintaksia na usambamba. Usambamba ulitumika kuongeza wizani na mdundo wa muziki nao ukiushi ukatumika kwa lengo la kusisitiza ujumbe. Ingawa matumizi ya vipengele vya kisintaksia katika nyimbo za Benga za jamii Wakamba huongeza mvuto wa kisanaa na kusaidia kufikisha ujumbe kwa kina, pia yanaweza kuwa na changamoto. Sentensi ndefu na tongole zinaweza kuchanganya hadhira na kupunguza uelewa wa haraka wa ujumbe hasa kwa wasikilizaji wasiokuwa na muda wa kutafakari kwa kina. Vilevile, ukiushi wa kisintaksia huenda ukavuruga miundo sahihi ya lugha na kuathiri matumizi bora ya lugha sanifu, hivyo kudhoofisha mawasiliano wazi na ya moja kwa moja.

Katika kiwango cha kisemantiki ilibainika kuwa nyimbo za muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba zimesheheni matumizi ya tamathali za usemi. Tamathali hizi ni kama vile chuku, tafsida, tashbihi, sitiari na tashihisi. Vilevile, mbinu za tautolojia, ukinzani, kinaya na paradoksia zilibainika kama mikakati inayotumiwa na waimbaji katika kiwango hiki. Matumizi ya tamathali za usemi na mbinu za kisemantiki katika muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba yanaongeza ubunifu na ujumi wa kisanaa, huku yakisaidia kuwasilisha hisia na hoja tata kwa njia ya kuvutia. Hata hivyo,

mikakati hii inaweza kusababisha changamoto za uelewakaji kwa wasikilizaji wasiokuwa na uelewa wa kina wa lugha au muktadha, hivyo kusababisha haja ya uwiano kati ya urembo wa kisanaa na uwasilishaji wa ujumbe kwa njia wazi.

5.1.2 Uimarishaji wa Ujumi

Utafiti huu ulibainisha kuwa waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba hutumia mikakati mbalimbali ya kimtindo kama nyenzo ya kuimarisha ujumi. Mikakati hii hujitokeza katika matumizi ya tamathali za usemi, mbinu za kisemantiki, mitindo ya kisintaksia na uundaji wa taswira za kisanaa ambazo huakisi mitazamo ya ujumi wa kigothiki, kihalisia, kimapenzi, kisiasa, kitamaduni na kiishara. Kupitia aina hizi za ujumi, waimbaji huweza kuwasilisha hisia za huzuni, mapenzi, usaliti, matumaini na hata ukosoaji wa kijamii na kisiasa kwa njia ya kisanaa yenye mvuto na athari za kudumu kwa hadhira.

Matokeo yanaonyesha kwamba umuhimu wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba si tu burudani, bali ni chombo cha mawasiliano chenye uzito wa kijamii na kisanaa. Mikakati ya kimtindo inayotumiwa huchangia katika kudumisha lugha na utamaduni wa jamii ya Wakamba, kutoa fasiri mbadala za maisha halisi, na kuimarisha ushiriki wa hadhira kwa kuwahusisha kihisia na kiakili. Kwa hivyo, uchanganuzi wa ujumi katika muziki huu unatoa mchango muhimu kwa taaluma ya isimu na fasihi na kuchangia uhifadhi wa urithi wa lugha na utamaduni wa Kiafrika kwa jumla. Hata hivyo katika jitihada za kuimarisha ujumi, waimbaji wanaweza kuficha au kupotosha ujumbe wa kimsingi, kuchochea matumizi mabaya ya lugha au kupunguza uhalisia wa hisia. Pia, hadhira isiyoelewa mbinu za kifasihi zinazotumika huenda ikakosa kuelewa ujumbe.

5.1.3 Athari Lengwa za Matumizi ya Mikakati ya Kimtindo

Utafiti huu ulichunguza athari lengwa za mikakati ya kimtindo inayotumika katika muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba. Ilibainika kuwa mikakati hii ina athari kubwa katika kuhamasisha na kuwasilisha masuala mbalimbali kwa jamii. Baadhi ya masuala yanayojitokeza katika muziki huu ni pamoja na:

Masuala ya wanawake katika jamii: mwanamke anachorwa kwa njia hasi, kama kiumbe asiye na utu, msherati na chombo cha kufurahisha mwanaume. Hii inadhihirisha jinsi jamii inavyomtazama mwanamke na nafasi yake katika jamii.

Masuala ya siasa na jamii: muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba pia unazungumzia masuala ya kisiasa, ikiwemo changamoto zinazoikumba jamii kutokana na uongozi na utawala mbovu.

Suala la dawa za kulevya: maudhui ya matumizi ya dawa za kulevya ni mojawapo ya mambo yanayoangaziwa katika muziki huu, pamoja na kuonyesha athari za tabia hizi kwa jamii. Baadhi ya athari za uraibu wa dawa za kulevya ni kama vile ubadhirifu wa fedha na kuzorota kwa tabia katika jamii.

Pia, waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba hulenga kuwasilisha hisia za kibinafsi na za kijamii. Hisia hizi ni kama vile mapenzi, huzuni na hisia za kukata tamaa. Isitoshe, waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba hulenga kuhamasisha, kukuza ushirikiano katika jamii na kuendeleza utamaduni.

Mikakati ya kimtindo kama vile urudiaji, matumizi ya tamathali za usemi na uradidi, husaidia kuhamasisha na kusisitiza masuala haya, hivyo kuboresha ufahamu wa hadhira kuhusu changamoto na hali za kijamii zinazozungumziwa. Athari hizi zinasaidia jamii kuelewa na kushughulikia masuala yanayowasilishwa katika muziki huu.

Hata hivyo, licha ya faida za mikakati ya kimtindo katika kuwasilisha ujumbe katika muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba pia ina changamoto mbalimbali. Kwanza, uchoraji wa mwanamke kwa njia hasi unaendeleza mitazamo ya kijinsia yenye ubaguzi na kuhalalisha dhuluma au unyanyasaji wa wanawake katika jamii. Pili, ingawa masuala ya siasa na dawa za kulevya yanawasilishwa, baadhi ya waimbaji wanawasilisha ujumbe huu kwa namna ya kejeli au mzaha, jambo linaloweza kupunguza uzito wa hoja au kuacha wasikilizaji bila mwongozo sahihi wa maadili. Aidha, matumizi ya hisia kali kama huzuni au kukata tamaa huenda yakaathiri kisaikolojia baadhi ya wasikilizaji, hasa iwapo hayajaelekezwa kwa suluhisho. Hivyo, ni muhimu kwa waimbaji kutumia mikakati hii kwa tahadhari ili kuhakikisha ujumbe unafika kwa njia wazi na yenye ufanisi.

5.2 Hitimisho

Utafiti huu umechunguza jinsi waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba wanavyotumia vipengele vya mtindo ya isimu kuwasilisha ujumbe. Umeongozwa na viwango vya nadharia ya umtindo kama vilivyoelezwa na (Leech, 1969). Imebainika

